

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ

از الديز عن دل الله الاسلام

UONGOFU WA TAFSIRI YA KURANI TUKUFU

NA HUSUDA YA
SH. ABDULLAH SALEH

UPINZANI UMEJIBIWA

**UONGOFU WA TAFSIRI YA KURANI TUKUFU
Na Husuda ya Sheikh Saleh, Upinzani umejibiwa**

Mtunzi: Sheikh Kaluta Amri Abedi

© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

Chapa ya Pili 1967 Nakala 5,000
Chapa ya Tatu 1981 Nakala 5,000
Chapa ya Nne 2010 Nakala 1,000

Kimeenezwa na:

**Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.**

Simu: +255 22 2110473
Fax: +255 22 2121744

Kimechapwa na:

**Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam,
Tanzania
Simu: +255 22 2111031**

ISBN 9987 - 438 - 10 - 5

Tafadhali soma haya kwanza

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya inafanya kazi ya kuuinua Uislamu katika nchi hizi tangu miaka 30 (sasa 75). Maelfu ya vitabu na magazeti yanayopigwa chapa kila mwaka yanashuhudia kwa uwazi kwamba Jumuiya hii peke yake imejitolea kuitumikia dini ya Kiislamu katika Afrika ya Mashariki. Hakuna Jumuiya nydingine ya Kiislamu iliyoanza kazi mapema tangu 1934 wala hakuna Jumuiya nydingine iliyo na mpango wa kuulinda Uislamu na mashambulio ya maadui zake.

Nabii Isa a.s.alisema,”Mti hujulikana kwa matunda yake”. Hivyo, msomaji mpenzi, usiendelee kudanganywa na wapinzani wa Jumuiya hii ambao wamekula fedha yingi ya Waislamu wa nchi hii na wa nchi zingine bila kuleta matokeo mema. Tafadhali zinduka. Usikubali kupumbazwa na watu werevu wasioelewa dini vizuri wala hawana moyo wa kuusaidia Uislamu. Fanya haraka kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya nawe utaona kuwa unatembea katika mwangaza na umeshika mpango maalum kwa kuiendeleza mbele dini yako. Ushindi wa Islamu utapatikana kwa kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya tu.

Wako;

Sheikh Mohammad Ishaque Soofi (BA).
Amir na Mbashiri Mkuu,
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.
Kenya.

Ahmadiyya Mosque,
Fort Hall Road,
Nairobi.
Disemba, 1966.

YALIYOMO

MLANGO WA KWANZA: (1 - 8)

UNABII ULIAMINIWA TOKA MWANZO

Sh. Abdallah ameshindwa kuvunja dalili.

Sheikh Muhyiddin alisadiki kuendelea utume.

Sheikh Jilani na Imam Shaarani pia walisadiki.

Ukaramsi wa kitoto wa Sh. Abdallah.

Ni kutapatapa kwa Sh. Abdallah.

Bibi Aisha hakusingiziwa:

Sh. Abdallah amehini.

Kama Mtume ni wa mwisho mbona Nabii Isa atakuja?

Sh. Abdalla ndiye mmeguzi si sisi.

Sh. Abdallah kamega maneno ya Sahaba.

Anatusingizia kuitupa hadithi.

MLANGO WA PILI: (9 - 13)

SI HADITHI DHAIFU WALA SI BATILI.

Shaukani anaamsahihisha Nawawi.

Al-Qari pia anaonyesha kosa la Nawawi.

Shihaab kinamsahihisha Nawawi.

Sh. Abdallah anaropoka tena

Kusema kwao Ibrahimu alikufa ili asiwe nabii ni batili.

MLANGO WA TATU: (14 - 22)

ALHAMDU INABASHIRI WAISLAMU

KUNEEMESHWA

Sh. Abdallah amerukiza maelezo yetu.

Sh. Abdallah amemkwepa Imam Raghib.

Tafsiri ya kosa iliwakwaza baadhi ya wafasiri.

Neema zilizoahidiwa.

Waislamu wamepewa neema hizo.

Upinzani wa Sh. Abdallah wajiishia. Anajivunja.

Tafsiri ya neno ma'a.

Waislamu watakuwa na ubora gani wasipopata vyeo?

Elimu ndogo inampoteza Sh. Abdallah.

MLANGO WA NNE:.... (23 - 33)

**ABDALLAH ANATATIZWA NA MANENO YA
MAWALII**

Sh. Abdallah amepotoa maneno ya Ruhul Maani.

Kubatilisha maneno yake yasemayo kuwa utume unaendelea lakini atakayeupewa asiiitwe mtume.

Sh. Abdallah anapenyeza maneno matano.

Usemi wa Sheikh Abdul Qadir Jilani.

Usemi wa Seyidna Ahmad.

Ubishi wa Sh. Abdallah ni wa kijicho.

Sh. Abdallah alikwepa maneno.

Wanataka kuzima nuru ya Mungu.

Ni nani wanaotumikia Uislamu zaidi

MLANGO WA TANO:.... (34 - 37)

AHADI YA NABII IBRAHIMU

Sh. Abdallah anamzulia Mungu.

Wadhalimu ndio hawapewi utume.

Sh. Abdallah haelewi Kurani.

Nabii Ibrahimu ni baba ya Waislamu.

MLANGO WA SITA: (38 - 41)

MAAGIZO KWA WANADAMU WOTE

Sh. Abdallah anatusingizia kimachomacho.

Sh. Abdallah hajui maana ya *yaqussuna 'alaikum*.

MLANGO WA SABA:.... (42 - 43)

NABII ISA BIN MARYAM NDIYE MASIHI

Uadui ukizidi (shairi).

Hatukumsingizia Razi wala Jarir wala ye yote.

Anaapa viapo vya kuchekesha.

MLANGO WA NANE:.... (44 - 56)

SHEIKH ABDALLAH ANAKUBALI NABII ISA

KISHA KUFA

Tumeshinda.

Hoja ya Wakristo.

Mufti wa Azhar na Almaraghi wanakubali kifo cha Isa.

Je Nabii Isa atashuka kutoka mbinguni?
Je waliokufa hurudi duniani?
Nini muradi wa kuja Nabii Isa.
Je, Isa huyo atafika kwa njia gani?
Ahadi ya kufika Mujaddidin.
Orodha ya Mujaddidin waliofika.
Waliomkubali Seyidna Ahmad.
Seyidna Ahmad hakuongeza wala hakupunguza wala
kubadilisha katika Uislamu.
Nyoyo za Kiyahudi (shairi la Kiarabu).

MLANGO WA TISA: (57 - 75)
KHAATAMANNABIYYIN LINA MAANA GANI?

Kubatilisha maneno yake yasemayo hakuna mfasiri ye yote
tangu Kurani ilipoanza aliyefasiri Khatamannabiyyin
kwa kuwa Muhuri wa Manabii.
Ametusingizia aliposema ya kwamba sisi tunadhanisha watu
maana ya Khatam ni moja tu ya muhuri.
Khatam linapokuwa mudhaf mudhaf ilaihi kwenye ismu za
wingi halijapata kuwa na maana ya mwisho katika lugha
nzima ya Kiarabu.
Ameshindwa kuleta hata mfano mmoja wa kuvunja dalili hii.
Mifano ya matumizi ya neno Khatam.
Ungekuwa mnyofu (shairi la Kiarabu).
Hoja madhubuti zimemtia kiwewe.
Ninamstaajabia (Shairi la Kiarabu).
Khatam kwa maana ya Muhuri katika Tafsiri F. Bayan.
Khatam kwa maana ya Mbora katika Tafsiri Kabir.
Muhammad ni Jua lenye anga (shairi la Kiarabu).
Ameshindwa na maneno ya Sh. Muhammad Qasim.
Ndaro za kujitutumua:
Tunapokea wito wake wa mashindano ya munadhara.
Tafsiri za vitabu vya Sh. Abdallah zina makosa mengi.

MLANGO WA KUMI: (76 - 88)

UBISHI MWINGINE ULIOMBAKI UNABATILISHWA

Mitume kupewa sifa mbaya na Mayahudi na Wakristo.

Namstaajabia kipofu (Shairi la Kiarabu).

Majinni: anatusingizia habari za majinni.

Shetani: anatusingizia habari za mashetani.

Waongo thelathini waliodai unabii.

Apewaye hapokeki (shairi).

Adam.

Mujiza ya Nabii Isa: anatusingizia kuwa hatuiamini.

Mti aliaokatazwa Nabii Adam ni mti gani?

Maana ya *auraaq* (majani) kuwa vijana.

Kuomba dua katika sala.

Tafsiri yetu imesafisha taka taka nyingi.

Tafsiri fulani za Kiarabu kumsingizia uovu Mtume.

Nabii Yusuf na Nabii Daud wanasingiziwa uovu.

Barua ya Sh. Abdallah inamsuta.

Husuda ndiyo imewachochea kina Sh. Abdallah kulaumu Tafsiri yetu iliyo safi kabisa kwa kuchelea kuanguka biashara ya vitabu vyao vidogo vidogo vya tafsiri zisizo na maelezo ya maana.

MLANGO WA KUMI NA MOJA: (89 - 95)

WAISLAMU WENYE ROHO SAFI WAMEIPOKEA

TAFSIRI YETU KWA SHANGWE NA SHUKRANI

Nakala za barua zao.

Kazi ya Mungu itakwenda mbele.

NENO LA MBELE

Kitabu hiki kilipigwa chapa mara ya kwanza katika mwaka 1954; watu wengi walinufaika kwacho na ubishi na ulalamishi wa Sheikh Abdallah Farsy ulinyamazishwa usisikike tena. Hakuthubutu kutoa majibu yake. Tangu miaka kadha kitabu hiki kilikuwa kimekwisha na ndugu wengi walionyesha hamu ya kukipata bila kufaulu. Nakumbuka safari moja mtungaji wake marehemu, Mwenyezi Mungu amweke pema peponi, alikisahihisha kipigwe chapa mara ya pili; lakini vikapatikana vizuizi hata kazi hii ikaakhirika kwa muda mrefu.

Mnamo mwaka 1964 mtungaji aliitika wito wa Mola wake na akatuachia huzuni na uchungu mwingi. Wengine kati yetu waliduwaa kwa pigo hili kali na wakafikiri huenda kazi ya Jumuiya ya Ahmadiyya ingepata hasara kwa sababu ya kifo cha marehemu. Huo ulikuwa ni wasiwasi tu wa muda, kwa maana matokeo ya baadaye yalihakikisha kwa nguvu tena kwa uwazi ya kuwa Jumuiya ya Ahmadiyya ni pando lililopandwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe na hakuna shida, iwe kubwa namna gani, inayoweza kuzuia maendeleo yake.

Hapa Tanzania tu katika muda wa miaka 2 iliyopita tumeona kazi ya Jumuiya ya Ahmadiyya imekuwa na maendeleo ya haraka haraka kana kwamba Mwenyezi Mungu amekuja mwenyewe kutuimarisha na kutusaidia. Baada ya marehemu kuondoka tumeweza kujenga msikiti mzuri huko Tanga pamoja na nyumba ya mbashiri. Tumepeleka mbashiri mmoja Mwanza ambako kulikuwa hakuna mbashiri zamani. Huko Bukoba nako tumefungua tawi jipyä na mbashiri anafanya kazi kama kawaida. Katika kijiji chake marehemu, yaani Ujiji, tulikuwa hatuna mbashiri. Sasa yupo na kazi ya Jumuiya inazidi kustawi huko pia.

Vitabu vipyä vimepigwa chapa na kutangazwa. Magazeti yameenezwa kwa wingi na yameleta manufaa kwa wasomaji. Wananchi wamekuwa na shauku kubwa ya kununua vitabu na magazeti yetu na uuzaji wa vitabu na magazeti umezidi mara kumi kuliko ulivyokuwa hapo zamani. Siwezi kuhesabu kazi zote tulizofanya baada ya marehemu kutuaga ila napenda kuwadokezeeni kidogo, ndugu waheshimiwa, kwamba kazi ya Mungu hairudi nyuma ikiwa Mwenyezi Mungu

anataka kuikuza. Bado kuna mipango mikubwa ya kupanua kazi ya kubashiri dini na kuelimisha vijana. Kijana mmoja hivi karibuni aliondoka hapa kwenda Rabwah, Pakistan, kwa mafunzo ya dini kwa miaka 6. Kijana mmoja anatazamiwa kurejea hapa baada ya masomo ya miaka 13. Kila mwezi watu wapya wanajiunga na Jumuiya na imani yao inazidi kutakasika. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu juu ya msaada wake mkuu anaotufanya.

Kitabu hiki nimekisoma na kusahihisha upya. Mbashiri wetu wa Kenya, Sheikh Muhammad Ishaque Soofi, ameshughulika mno na kazi ya kukipigisha chapa vizuri zaidi na matokeo yake mnayaona wenyewe. Bei ya kitabu imezidi kwa sababu ya kutengenezesha upya maneno mengi ya Kiarabu yaliyotumika humo na kwa sababu ya gharama ya uchapishaji kuongezeka. Lakini ilikuwa hakuna budi maneno ya wanazuoni wa Kiislamu yaandikwe vile vile walivyoandika wao ili msomajji asibaki na shaka hata kidogo moyoni mwake juu ya maneno hayo yenye maana sana.

Ama mtu kutaka ubishi au kuleta maswali yoyote juu ya kitabu hiki, basi mimi niko tayari kujibu maswali yake yote au kubishana naye popote juu ya mas'ala yanayotuhusu katika dini yetu tukufu ya Kiislamu. Msifikiri kwamba maadamu mtungaji amefariki, basi mwenye kujibu maswali yenu hakuna. Tulishirikiana mimi na marehemu kwa kutunga kitabu hiki na mpaka sasa nipo hapa kuondoa shida zenu zote, Inshaallah. Na nikiondoka Mwenyezi Mungu atainua wengine msitindikiwe na tumaini hata mara moja. Kazi ya Dini ya Kiislamu itakwenda mbele siku zote wala hakuna kurudi nyuma mpaka Uislamu uwe umeshinda ulimwengu mzima.

Wasalaam;

Ndugu yenu na Mtumishi wenu,

Sheikh Muhammad Munawwar H.A.
1st January, 1967
P.O. Box 376,
Dar es Salaam, Tanzania.



Mtungaji wa Kitabu hiki Sheikh Kaluta Amri Abedi

*(Baada ya Kitabu hiki kupigwa chapa mara ya kwanza,
mtungaji alituaga. Mola amstareheshe peponi. Amin)*



Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema na ukarimu.

UTANGULIZI

Namshukuru Mheshimiwa Sheikh Mubarak Ahmad Ahmadi H. A. Rais na Amir wa Jumuiya ya Ahmadiyya katika Afrika Mashariki kwa kunipa nafasi niandike kijitabu hiki cha kumjibu sahibu yangu Sheikh Abdallah Saleh Farsy wa Unguja juu ya kijitabu chake alichoandika kiitwacho “Upotofu wa Tafsiri ya Makadiani.”

Mara tu Sh. Abdallah alipomaliza kuandika makala za kijitabu hicho zilipokuwa zikipigwa chapa katika “Mwongozi” nilikuwa Tanganyika, huko kwetu Ujiji, naye Sheikh Abdallah aliniletea barua ya kuniambia kuwa amelazimika kutupinga shingo upande kwa sababu “Ukimstahi mke-ndugu huzai naye.” Mimi nilimjibu mara moja ya kuwa nimesoma maneno yake kwa uangalifu, na ya kwamba lazima atashindwa katika jambo hili kwa kuwa maandiko yake hakuyatoa kwa uaminifu, na zaidi ya hayo alishindwa kuelewa mambo mengi alijojitia kuyajibu.

Sahibu yangu, Sheikh Muhammad Munawwar, H.A., alikuwa wa kwanza kutoa jawabu la Sheikh Abdallah katika gazeti letu la “Mapenzi ya Mungu.” Naye aliandika jawabu zuri lililotuliza shauku ya wasomaji wetu hata wakasifu sana na kupendezwa na majibu mafupi bali ya kutosha ya mwanachuoni huyu. Kwa hakika katika baadhi ya mambo alijoandika sikuwa na la kufanya ila kuhamisha makala zake na kuzifanya ziwe sehemu ya kijitabu hiki.

Sh. Abdallah alipopiga chapa maneno yake katika sura ya kijitabu, Sheikh Mubarak Ahmad akaona itafaa yatengenezwe majibu katika umbo la kijitabu, na akanikabidhi kazi hiyo mimi. Kwa bahati, kazi hii imenikuta katika mapumziko ya Kiangazi hapa Pakistan, na hivyo nikawa na wakati mwangi sana wa kukagua vipyta mavitabu yote ya marejeo niliyotaja katika kijitabu hiki, na yaliyotajwa katika Tafsiri ya Kurani, yaliyoko katika Library Kuu ya Jumuiya yetu hapa. Nimeridhika ya kuwa marejeo yetu yote yaliyoko katika Tafsiri ni sawa kama vile tulivyoyaandika, wala hakuna mstari uliotuponyoka. Kadhalika

nimekagua maneno yaliyoandikwa na Sheikh Abdallah, na habari zote mtasoma katika jawabu lenyewe.

Bwana Ali Muhsin Barwani aliyeandika utangulizi wa kijitabu cha Sh. Abdallah naye natumai atafaidishwa na majibu hayo. Nimeupuuza utangulizi wake nilipoona ameandika ya kuwa Seyidna Mirza Ghulam Ahmad alizaliwa mwaka 1889. Niliona ya kwamba alijandikia tu bila kuwa na habari sahihi. Ikiwa hajui mwaka aliozaliwa Seyidna Ahmad anawezaje kuandika cho chote kinachohusu habari za maisha yake? Hivyo nikayapuuza maneno yake kama ya mtu asiyeha na akili ambaye amekokotwa tu kutiwa ndani ya ngoma asiyojua kuicheza.

Natumai wote wawili pia watasoma maneno ya kijitabu hiki kwa fikira na uangalifu, wala wasifanye haraka kuyasoma juu juu kama walivyosoma maneno ya maelezo ya tafsiri yetu. Nami niko tayari maadamu ni hai kujibizana nao kwa kila hali na kusahihisha makosa yao. Mungu afunue macho yao, aondoe husuda miyoni mwao, na awaongoze na kuwatoa katika upotofu. - Amin.

1.	Tu katika jeshi, Na Amiri jeshi, Ujapo uzushi, Na kila utashi, Kiwingu cha moshi,	la Muhammadi, ndiye Mahadi, na ukaidi, wa mahasidi, kiwafisidi,	kwenye kitali. shujaa kweli. twaukatili. utadhalali. kwa yao zuli.
2.	Ndimi asikari, Sikhofu jeuri, Wajapo jasiri, Hushika hodari, Nikawakhasiri,	wa Asikari, khasa jeuri, kina ayari, yangu khanjari, kwa hoja nzuri,	Wake Jalali. za udhalali. kwa ufedhuli. penye kitali. zenye akili.
3.	Nihudhuriapo, Hugandama papo, Ndipo nishindapo, Haki ing'aapo, Ndipo wajutapo,	kwenye medani, hadi mwishoni, kwa kila fani, nani shetani, kina fulani,	zenye kitali. kama jabali. za kusaili. wa kukabili? kwa idhilali.

Missionary College,
Rabwah (W. Pakistan).
18th July, 1954.

K.A.A

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
نَحْمَدُ اللَّهَ وَنُصَلِّي عَلَى مُحَمَّدٍ الْمُصْطَفَى صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ

MLANGO WA KWANZA

UNABII ULIAMINIWA TOKA MWANZO

Sasa ninaingia kujibu kila lawama ilioletwa na Sh. Abdallah. Nina yakini kabisa ya kwamba kila atakayesoma majibu haya kwa kutaka kujua haki iko wapi, atajua. Na pia atajua bila taabu ya kuwa Sh. Abdallah amejiingiza katika neno ambalo hana elimu ya kulitosha.

Sh. Abdallah ameshindwa kuvunja dalili.

Ameandika katika ukurasa wa 1 wa kitabu chake akasema, “Islam wote wa kila madhehebu tangu Uislamu ulipoanza mpaka leo wanaitakidi na wanaandika katika kila kitabu kuwa Nabii Muhammad ndiye Mtume wa mwisho, hakuna atakayepewa Utume tena.”

Haya bila shaka ni maneno yanayoweza kusemwa na mtu anayejua habari kidogo tu za Waislamu na za Uislamu. Katika Tafsiri ya Kurani tumeeleza maneno ya maulamaa wengi wa zamani waliosadiki ya kwamba Mtume Muhammad s.a.w ni wa mwisho kwa kuleta Sheria ya Dini, Dini yake itaendelea mpaka siku ya Kiyama. Haji mtume mwingine kuleta dini mpya. Sh. Abdallah hakupata la kusema juu ya maulamaa hao ambao nitawataja tena hapa. Alikimbilia maneno aliyofikiri ni mepesi kujikinga nayo, lakini nayo yakamsumbuwa sana, asiweze kuyavunja.

Sh. Muhyid-Din alisadiki Unabii bila Sheria Unaendelea.

Walii maarufu Sheikh Muhyid-Din Ibni Arabi amesema katika kitabu chake kiitwacho Futuhati Makkiyya, jalada ya 2 uk. 3:

فَإِنَّ الشَّيْءَةَ الَّتِي انْقَطَعَتْ بِوْجُودِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَسَلَّمَ إِنَّمَا هِيَ الشَّيْءَةُ الَّتِي شَرِيعَ لَهُ مُنَّا مُهَمَّا . فَلَا شَرَعَ

يَكُونُ نَاسِخًا لِشَرِيعَهِ عَلَى اللَّهِ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَلَا يَبْرِدُ فِي
 حُكْمِهِ شَرْعًا أَخْرَوْهُهَا مَعْنَى قَوْلِهِ عَلَى اللَّهِ عَلَيْهِ وَ
 سَلَّمَ إِنَّ الرِّسَالَةَ وَالنِّبَوَةَ قَدْ اِنْقَطَعَتْ فَلَا رَسُولَ
 بَعْدِي وَلَا نَبِيَّ آتَى لَأَبْنَى بَعْدِي يَكُونُ عَلَى شَرِيعَهِ بِعِلْفَتُ
 شَرِيعِي بَلْ إِذَا كَانَ يَكُونُ تَعْتَدُ حُكْمِ شِرِيعَتِي -
 (فَتوحات مَكِيَّة جلد ٢)

Tafsiri ya maneno haya tuliiandika katika ukurasa wa 737 wa Tafsiri ya Kurani toka mstari wa 25, hivi: “Utume uliokatika kwa kufika Mtume s.a.w. ni utume wa Sheria, siyo cheo cha utume. Hivyo hakutakuwa na sheria itakayovunja Sheria ya Mtume Muhammad s.a.w., na hakutakuwa na sheria itakayozidisha hukumu yo yote katika Sheria yake. Hii ndiyo maana ya Hadithi ya Mtume s.a.w. aliposema, Hakika utume na unabii umekatika, basi hukuma Mtume wala Nabii baada yangu; yaani hakutakuwa na Nabii atakayekuwa kinyume cha Sheria yangu, bali akiwa, atakuwa chini ya hukumu ya Sheria yangu.”

Katika Kitabu hicho hicho, jalada ya pili, mlango wa 73, uk. 90, mstari wa 9-10, Sheikh Muhyiddin Ibni Arabi akasema tena:

فَالنِّبَوَةُ سَارِيَةٌ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ فِي الْغَنْقَقِ وَإِنْ كَانَ
 الشَّرِيعَةُ قَدْ اِنْقَطَعَ - (فَتوحات مَكِيَّة جلد ٢ مِحْبَفَةٌ ٩٥)

yaani, “Utume unaendelea mpaka siku ya Kiyama katika viumbi, ingawa (utume) wa kuleta sheria umekatika.” Maneno haya kadhalika tuliyasiria katika ukurasa huo huo wa tafsiri ya Kurani. Tukasema, “Utume umekatika kwa maana ya kuwa hataweza kuja Mtume wa kuleta sheria ya kuvunja Sheria ya Mtume Muhammad s.a.w. Utume

utaendelea mpaka siku ya kiyama.” Je, Sheikh Muhyiddin aliyeandika maneno hayo hakuwa Mwislamu?

Sheikh Jilani na Imam Shaarani pia walisadiki

Katika ukurasa huo huo wa Kurani Tukufu tulinakili maneno ya Seyid Abdul Karim Jilani yasemayo:

فَانْقَطَعَ حُكْمُهُ نِيَّةُ النَّبِيِّ بَعْدَهُ وَكَانَ مُحَمَّدًا مَوْلَى اللَّهِ عَلَيْهِ
وَسَلَّمَ خَاتَمَ النَّبِيِّنَ لَا تَرَهُ جَاءَ بِالْكَمَالِ وَلَمْ يَجِدْ أَحَدًا
بِذَلِكَ - (الإِنْسَانُ الْكَامِلُ صَحِيفَةٌ ٧٢ بَابٌ ٣٦)

yaani, “Hukumu ya unabii wa sheria imekatika baada ya Mtume s.a.w. hivyo amekuwa Khaatamannabiyyin” kwa kuwa ye ye amekuja na ukamilifu na hakuja ye yote namna hiyo (Al Insaanul Kamil, mlango 36). Je, Sheikh Abdul Karim Jilani hakuwa Mwislamu?

Tena tukaandika maneno ya Imam Abdul Wahhab Shaarani yasemayo:

إِعْلَمَ أَنَّ النَّبِيَّ لَمْ تَرْتَفَعْ مُطْلَقاً بَعْدَ مُحَمَّدٍ مَوْلَى اللَّهِ
عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَإِنَّمَا الْزَّنْجَ نِيَّةُ النَّبِيِّ -
(الْأَبْيَاقِيتُ وَالْجَوَاهِرُ جِلْد٢ صَحِيفَةٌ ٣٩)

Yaani, “Utume haukifungwa kabisa, Mtume ambaye hawezi huja ni wa kuleta Sheria.” Au unaweza kuyatafsiri hivi neno kwa neno: “Utume wenyewe haukuondolewa, ulioondolewa ni utume wa sheria tu.” (Alyawaqiu wal Jawahir, jalada 2; uk.39). Je, Imam Shaarani naye hakuwa Mwislamu kwa kuandika kuwa utume uliokatika ni wa Sheria tu? Je, Sh. Abbdallah atawatoa mawali hawa na maimamu hao katika Uislamu? Je, ye ye anajua hata nusu ya elimu yao?

Kwa ufupi haya ni maneno ya Waislamu mashuhuri yanayotusadikisha waziwazi kuwa Mtume Muhammad s.a.w. ni wa mwisho kwa kuleta Sheria ingawa cheo cha unabii usio wa sheria baadhi ya wafuasi wa Mtume wetu s.a.w. wanawenza, kukipata kwa sababu ya kumfuata yeye na kumtii yeye.

Ukaramsi wa kitoto.

Sh. Abdallah amefanya ukaramsi wa kitoto kabisa kutamka ya kwamba Islam wote waliandika katika “kila kitabu” toka mwanzo mpaka leo kuwa hakuna atakayepewa utume tena. Hata kauli yake hii “Kila kitabu” inatosha kutufahamisha jinsi Bwana huyu alivyo mwepesi wa kusema mambo yasiyoelekea. Je, ni kweli ya kuwa “kila kitabu” kilichoandikwa na Waislamu kililazimika kueleza hiyo itikadi yake - Je, hivyo juu si vitabu vya Waislamu? Mbona maneno ya vitabu hivyo ameyakwepa kabisa zama akijitia pambani za kutujibu ingawa tulivitaja waziwazi na maneno yao tukayaandika?

Ni kutapatapa.

Baada ya kushindwa na maneno hayo, hakupenda kumwogopa Mungu na kueleke haki. Yeye aliruka akayaacha maneno ya Sheikh Muhyiddin Ibni Arabi juu na pia ya Seyid Abdul Karim Jilani, akakimbia kifungu kilichofuata nyuma yao cha maneno ya Bibi Aisha. Alidanganyika kudhani ya kwamba maelezo yake ya “kuparanganya” yatatuponyoka hata na sisi tunaolala humo humo ndani ya mavitabu.

Sisi tuliandika katika ukurasa wa 737 wa Tafsiri ya kuwa “Bibi Aisha, mke wa Mtume s.a.w. alisema:

”قُولُوا إِخَانَهُمُ النَّبِيِّينَ وَلَا تَقْتُلُو الْأَنْبِيَاءَ بَعْدَهُ“
(*تفسيير الدر المنشور* جلد ٥، صحيفه ٢٤)

Yaani, “Semeni, Yeye ni *Khaatamannabiyyin* lakini miseme hakuna Nabii baada yake” (Tafsiri Durri Manthur). Maneno haya ni wazi kabisa yanayoonyesha kuwa *Khaatamannabiyyin* si maana yake’

“mwisho wa Mtume”, maana ingekuwa maana yake ni “mwisho wa Mtume” asingewaambia watu wasieme hakuna Nabii baada yake, bali angewaambia, “Semeni yeye ni Khaatamannabiyin na semenii haji Nabii baada yake.” Lakini maneno yake ni kinyume kabisa na hayo. Jambo hili ni wazi sana.

Maneno fasihi ya mama yetu Bi Aisha yamemlazimisha Sh. Abdallah ajaribu kufanya ujanja wa kupindua tafsiri ya maneno *La nabiyya baadahu* yasomeke “Hapana atakayepata Utume baada yake” Ili kumwachia mlango wazi Nabii ye yote aliyekufa zamani arudi duniani kuongoza Waislamu, lakini kumfungia Mwislamu ye yote kupata cheo hiki. Jinsi alivyobadilisha tafsiri ni wazi kabisa hata nashangaa hofu ya Mungu imeondoka kabisa katika moyo wa mtu huyu. Neno “Kupata utume” analoingiza Sh. Abdallah ni tafsiri ya neno gani la Kiarabu katika maneno hayo? Maneno hayo ya Kiarabu ni La (Hakuna) nabiyya (nabii) baadahu (baada yake). Hayo ni maneno yasiyokubali kugeuzwa. Na huku kusema, “Hakuna Nabii baada yake” ndio kumekatazwa na Bi Aisha na pia kukatazwa na Sahaba wa Mtume s.a.w. aitwaye Muughira bin Shu’ba.

Nabii Isa atakuja baada ya Mtume

Hivyo, tafsiri safi ya maneno *La nabiyya baadahu* ni kuwa Hakuna Nabii baada ya Mtume. Bibi Aisha alikataza watu kusema maneno haya, na Bwana Mughira akakataza watu kusema maneno hayo. Na Mtume mwenyewe s.a.w. akasema mara nyingi kuwa Nabii Isa atakuja, na watu wote wanajua jambo hili. Basi Mtume wetu angekuwa wa mwisho kwa maana ya kuwa haji nabii wa namna yo yote baada yake, angesemaje kuwa Nabii Isa atakuja?

Sh. Abdallah anasema, kuja Nabii Isa ni kwa sababu alipewa utume kabla ya Mtume, si utume mpya. Lakini maneno ya hadithi hayasemi habari za utume mpya au mkuukuu. Yanasema, *La nabiyya baadahu* (Hakuna nabii baada yake). hayasemi *La nubuwata baadahu* (Hakuna unabii baada yake). Je, tuache maneno ya Hadithi tufuate matamano ya kijana huyu yasiyo na dalili? Hivyo, hata kama Nabii Isa aje safari ya pili atasemwa amekuja baada ya Mtume. Kwa kuwa kwanza Nabii Isa alifuata Injili, itakuwa lazima atakapofika Mungu

ampe wahyi wa kufuata Kurani, na huo utakuwa ni utume mpya pia. Itakuwa lazima aya ile ya Kurani inayosema kuwa Nabii Isa alitumwa kwa Waisraeli (3:50) iongezewe maneno kuwa ametumwa na kwa Waislamu pia, hivyo hata Kurani italazimu kubadilika. Je utume wa kubadilisha hata na Kurani utakuwa ni mkuukuu huo? Ni wazi basi Isa ikiwa ni yule yule atakayekuja, kwa hali yo yote atasemwa kuwa kaja baada ya mtume, na kwa hali yo yote atasemwa kapewa utume mpya wa kufuata Kurani sio ule wa zamani wa kufuata Injili.

Hivyo, Sh. Abdallah anaposema Mtume wetu ni wa mwisho kwa maana ya kuwa haji nabii tena, kisha anakubali kuwa Nabii Isa atakuja, amekuwa kama mtu aliyekaa mtini juu huku anaukata shinani. Basi Sh. Abdallah kaanguka! Kaanguka mweleka wa kutia haya. Kwa hiyo, kauli ya kusema, “Hakuna Nabii baada yangu” na hali mwenyewe ameelleza kwa mkazo na mara nyingi kuwa Nabii Isa atafika, kauli hiyo itakuwa na maana gani ila ipewe tafsiri inayopatana? Na tafsiri hiyo tumeieleza katika maelezo ya Tafsiri ya Kurani, na pia tutaieleza tena ndani ya kijitabu hiki; nayo ndiyo tafsiri inayokubaliwa na akili kama ilivyokubaliwa na maulamaa ambao baadhi yao tumeandika maneno yao hapa juu.

Mmeguo wa Sh. Abdallah

Sh. Abdallah anatulaumu bure ya kwamba tumeacha kueleza maneno mengine ya kitabu Durri Manthur. Lakini tungakuwa tumeacha neno la maana katika maneno ya Bibi Aisha mwenyewe tuliyoyanakili, hapo tungelaumiwa. Lakini kauli tuliyotaja ni ya Bibi Aisha. Na kauli anayosema tumeacha ni fikira ya Bwana Qatada asemaye kuwa Mtume ni wa mwisho, ambayo inahitilafiana na kauli ya Bibi Aisha. Nasi tuliyagizwa na Mtume wetu s.a.w. tujifunze nusu nzima ye elimu ya dini yetu kwa Bibi Aisha. Na kauli ya kusema mtume ni wa mwisho kwa kila hali si ngeni na baadhi ya Waislamu, na ndiyo kauli isiyonyooka. Basi si kioja cha huyu Sh. Abdallah kututaka tueleze maneno ya kila mtu ambayo hayako katika shabaha ya usemi?

Ama kwa hakika ye ye Sh. Abdallah ndiye anastahili kulaumiwa kwa kuacha kutaja kipande cha mbele na cha mwisho cha maneno ya Bwana Mughira, ambayo kama angeyataja kwa ukamilifu watu

wangeona mara moja hiyana anayopitisha katika usemi wake.

Sahaba Mughira bin Shu'ba anakubaliana nasi

Maneno kamili ya Mughira bin Shu'ba yaliyomo katika Durri Manthur, ambayo ni sawa na yale ya Mwana Aisha (Mungu awe radhi nao) ni haya:

قَالَ رَجُلٌ عِنْدَ الْمَغِيرَةِ بْنُ شَعْبَةَ مَوْلَى اللَّهِ عَلَى مُحَمَّدٍ خَاتَمِ
الرَّسُولِ لَا يَتَيَّبُ بَعْدَهُ فَقَالَ الْمَغِيرَةُ حَسْبِكَ إِذَا قَاتَلَتْ خَاتَمَ
الرَّسُولِ فَإِنَّا كُنَّا نُعَذِّثُ أَنَّ عَيْسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ حَارِمٌ فَإِنْ حُوَ
خَرَجَ فَقَدْ كَانَ قَبْلَهُ وَبَعْدَهُ (الدِّرْرُ المُنْشُرُ جِلْد٤ صِحِيفَة٤)

Yaani, "Mtu mmoja alisema mbele ya Mughira bin Shu'ba, 'Mungu amsalie Muhammad Khaatamul Ambiya, hakuna Naabii baada yake.' Mughira akasema, 'Imekutosha uliposema Khaatamul Ambiya, maana tulikuwa tukisimuliwa ya kwamba Isa, amani juu yake, atatokea. Na kama akitokea, basi atakuwa wa kabla yake na baada yake.'" - (Durri Manthur).

Maelezo haya yanaonyesha waziwazi kuwa baadhi ya watu toka zamani hawakufahamu tafsiri ya maneno *Khaatamannabiyyin* na *La nabiyya baadahu*. Ingekuwa *Khaatamannabiyyin* maana yake ni Nabii wa Mwisho kwa maana ya Sh. Abdallah na jamaa zake, palikuwa haja gani yule mtu kukatazwa na Mughira asiseme hakuna Nabii baada ya Mtume? Maadamu Nabii Isa atakuja si vizuri hata kidogo kuwapoteza watu kwa kuwaambia kuwa haji baada ya Mtume hata nabii wa kufuata dini yake. Hakika Mtume wetu s.a.w. ni wa mwisho kwa kuleta dini, nayo Sheria yake itakaa mpaka Kiyama. Na hivi ndivyo tusemavyo, ndivyo sawa na akili nzima, ndivyo sawa na Kurani Tukufu, na ndivyo walivyokubali hata maulamaa wenye kumcha Mungu sana wa zamani na wa sasa ambao kila mara tunawataja.

Kadhalika ni kubabaika kwa Sh. Abdallah kusema kuwa tumeruka mistari ya juu iliyothibitisha hadithi sahihi ya *La nabiyya baadi*; kwani

maelezo ya hadithi hii tulikwisha yaandika kama yalivyoandikwa na Sheikh Muhyiddin Ibni Arabi, na hiyo hadithi yenyewe pia tukaiandika katika ukurasa ule ule wa 737 wa Tafsiri katika mstari wa 30. Sasa atasemaje kuwa tumeitupa hadithi tuliyokwisha itaja na kuieleza? Bila shaka Bwana huyu alivamia kusoma Tafsiri yetu kwa pupa ya husuda, hata bila kuelewa kitu akaanza kuandika kila lililomjia akilini. Kijitabu chake kizima ni upuuzi wa namna hii mtupu uliokijaza.

Usemapo neno
 pasi ujuzi mtimilifu,
Utauma meno
 ujaposutwa udanganyifu,
Nayo matukano
 mtukanayo na kukashifu,
Ndio msumeno
 utakereza zenu sharafu.

SI HADITHI DHAIF WALA SI BATIL

Sh. Abdallah amebaki kweupe aliporopoka kusema ya kuwa hadithi hii ya Mtume s.a.w.

لَمَّا مَاتَ إِبْرَاهِيمَ كَانَ نَبِيًّا - (ابْنُ مَاجَةَ صَحِيفَةٌ ٤٦)

“Angeishi Ibrahimu angekuwa Nabii mkweli” haina nguvu kisha ni batili. Amenakili maneno ya Imam Nawawi na watu wengine wawili ili yamsaidie. Tunampa pole, maana ujinga wa kiasi hiki ni ugonjwa. Kabla hatujabatilisha maneno yake, tunamwuliza swalii dogo. Hii Hadithi inayoonyesha kuwa utume bado uko lakini Ibrahimu mtoto wa Mtume hakupata kwa sababu alikuifa, ambayo anaisema ni ya uwongo, je ni nani huyo Mwislamu wa zamani aliyekuwa anasadiki kuendelea kwa utume hata akafika kuibuni? Kwa vyo vyote, inaonyesha kuwa kama hadithi hiyo ilibuniwa, basi aliyeibuni naye alikuwa anasadiki ya kuwa unabii ungaliko, maana asingejaribu kubuni hadithi inayokwenda kinyume na itikadi yake. Hapo basi, maneno yake ya kusema kuwa Waislamu wote toka mwanzo walasadiki Mtume wetu ndio mwisho kwa kila hali, hapa pia yanavunjika. Waahmadiyya wameikuta duniani hadithi hiyo inayoashiria kuwa unabii ungaliko ila Ibrahimu hakuupata kwa sababu alifariki.

Shaukani anamsahihisha Nawawi

Maneno ya Imam Nawawi ya kusema Hadithi hii ni batili yamevunjwa na ‘Allama Shaukani katika kitabu kiitwacho *Fawa'idul Majmu'a Fi Bayan Ahadith Maudhu'* a ukurasa 144 akasema:

**وَهُوَ عَجِيبٌ مِّنَ النَّوْرِيِّ مَعَ دُرْرُدَةِ عَنْ ثَلَاثَةِ مِنَ الصَّحَابَةِ
وَكَانَهُ لَمْ يَنْظُمْ لَهُ تَوْنِيهٌ - (فَوَاللهِ الْمَجْمُوعَةُ فِي بَيَانِ أَهَادِيثِ
الْمَؤْضُوعَةِ - صَحِيفَةٌ ١١٤)**

Yaani, “Hii ni ajabu ya Nawawi (kubatilisha hadithi hii) ingawa inatokana na Masahaba watatu. Ni kana kwamba maana ya hadithi hii haikumdhihirikia.”

Al-Qari pia anamsahihisha Nawawi

Maneno haya ya Allama Shaukani bila shaka yamemweka Sh. Abdallah kweupe, kwani Imam ambaye maneno yake anayateggeomelia aliikataa hadithi hii kwa sababu hakuilewa. Angalia mwingine aliyelewa muradi wa hadithi hiyo asemayyo. Sheikh Ali Al-Qari ambaye ni mwanachuoni mashuhuri wa elimu ya hadithi za Mtume s.a.w. ameandika katika kitabu kiitwacho *Maudhu'aat Kabir* uk. 68-69:

لَكِنْ لَهُ طُرُقٌ ثَلَاثٌ يَقُولَى بِعَصْمَهَا بِعَفْنِ -
(مَوْضُوعَاتٌ كَبِيرٌ صَحِيفَةٌ ٦٨-٦٩)

Yaani, “Lakini (hadithi hii) ina njia tatu kila moja ya njia hizo inaipa nguvu njia nyingine.” Na pia akasema:

فَلَآيَنَا قِضَى فَوْلَهُ خَاتَمَ الْبَيْتَنَ إِذَا الْمَعْنَى أَنَّهُ لَا يَأْبَى إِنْ يُبَيِّنَ
نَبِيًّا بَعْدَهُ يَسِّرُ مَلَّتَهُ وَلَمْ يَكُنْ مِنْ أَمْتَهُ -
(مَوْضُوعَاتٌ كَبِيرٌ صَحِيفَةٌ ٦٩)

Yaani, hadithi hii “haivunji kauli ya Mwenyezi Mungu ya Khaatamannabiyyin, kwani maana ya kauli hii ni kuwa haji Nabii wa kuvunja mila ya Mtume na (haji nabii) asiyekuwa katika umati wake” (uk. 69).

Hivyo, wale waliositasita kuipokea hadithi hii ni kwa sababu ya kosa la itikadi yao juu ya maneno khaatamannabiyyin, kama anavyobainisha mwanachuoni huyu ya kuwa maana yake maneno hayo ni kwamba akija nabii hatavunja mila ya Mtume na atakuwa katika umati wa Mtume, hataunda umati mpya au dini mpya. Kosa

hili la kutafsiri *khaatamanniyyin* na *La nabiyya baadi* kwa hakika limewafanya wafasiri wengi wapotoe hata maneno yaliyo wazi kabisa yanayoonyesha kuendelea unabii yaliyomo katika Kurani Tukufu.

Shihaab kinamsahihisha Nawawi

Katika kitabu kiitwacho *Shihaabu 'alaI Baidhawi*, juzu ya 7 ukurasa 175 mmeandikwa habari ya hadithi hii hivi:

أَمَّا صَحَّةُ الْحَدِيثِ فَلَا شُبُّهَةَ فِيهِ لَا تَرَأَفُ أَبْنُ مَاجِةَ
وَغَيْرُهُ كَمَا ذَكَرَ لِابْنِ حَجَرِ -
(شَهَابٌ عَلَى الْبَيِّنَاتِ جَلْدٌ ٧ صَحِيفَةٌ ١٧٥)

Yaani, “Ama usahihi wa hadithi hii hauna shaka, maana ameisimulia Ibni Majah na wengineo kama alivyotaja Ibni Hajar.”

Hapa ingefaa wasomaji wetu wajifunze neno moja. Katika elimu ya Hadithi za Mtume wetu s.a.w. inaposemwa Hadithi fulani ni dhaif (haina nguvu) muradi wake si kwamba haiwezi kuwa ya kweli, bali kama katika mnyororo wa walioipokea kuna hata mtu mmoja mwenye fahamu au kumbukumbu au ukweli usiotegemewa, basi hadithi hiyo inaitwa dhaif hata kama ni ya kweli.

Basi maneno haya ya maulamaa yanatosha kabisa kumrudi Sh. Abdallah na kumhakikishia upungufu wa elimu yake katika elimu ya hadithi. Lakini kwa ajili ya kulikamilisha jambo hili nitabatilisha hoja yake moja iliyobaki. Waidha mmekwisha ona ya kuwa maneno ya Imam Nawawi na watu wengine wawili waliotaka kuihafifisha hadithi hii yamebatilishwa na Allama Shaukani, hata akamstaajabia. Tena yamebatilishwa na Sheikh Al-Qari, na pia yakabatilishwa katika *Shihaabu 'alaI Baidhawi*. Na kadhalika yakabatilishwa na Ibni Abdul Bari katika Tamhidi yake.

Sh. Abdallah anaropoka tena

Sasa angalieni kuropoka kwingine kwa Sh. Abdallah. Anasema ya kuwa hadithi hii tumeitaja kwa ufupi wake tu hali imeandikwa kwa urefu wake na Ibn Majah ya kuwa “Lau angeishi Ibrahim nyuma ya Mtume angekuwa Mtume, lakini muhali kusalia hai baada ya Mtume, kwani Mtume wenu huyu (Nabii Muhammad) ndiye Mtume wa mwisho.”

Sasa kwa hakika maneno haya hayawezi kusemwa ni urefu wa hadithi hiyo, maana ni maneno yaliyoongezwa na rawi aliyeipokea hadithi hiyo, akasema, “Lakini hakubakia hai, kwani Nabii wenu ni mwisho wa Mtume.” Haya maneno yaliyoongezwa si maneno yaliyosemwa na Mtume s.a.w. Maneno yaliyosemwa na Mtume s.a.w. ni haya tu “Angeishi Ibrahim angekuwa Nabii mkweli.” Sasa kusema ya kuwa kwa sababu hakuna unabii ndiyo maana akafa, ni kufikiri tafsiri inayokwenda kichwa chini miguu juu. Maana, kama Mungu aliogopa kuwa Ibrahim akiishi atakuwa Nabii, hivyo akaona afadhali afe upesi, kwa nini tena alimfanya azaliwe? Je, kama Mungu asingetaka kumpa Ibrahim utume, Ibrahim angeunyang’anya kwa nguvu? Au ni lazima kila mtoto wa Nabii awe Nabii? Mbona mtoto wa Nabii Nuhu hakuwa Nabii? Mbona watoto kumi na moja wa Nabii Yakubu hawakuwa manabii? Basi kama Ibrahim mtoto wa Mtume s.a.w. angeishi na asiwe Nabii kungekuwa sheria gani ambayo ingesemwa imevunjwa? Sasa kusema kuwa Mungu alimfisha ili asije kuwa Nabii siyo maneno yasiyo na maana? Je Mungu alisahau kuwa Mtume wetu ni wa mwisho alipomfanya Ibrahim azaliwe? Maneno gani haya yasiyo na wajiji anayoweka Sh. Abdallah mbele za watu wenye akili?

Ni wazi basi ya kuwa wanataka wapotoe kila neno lililonyoka lipatane na itikadi zao za matata-matata, hata kwa namna kama hii inayokwenda waziwazi kichwa chini miguu juu. Hadithi hii pia imeandikwa katika kitabu Tarikh Ibn ‘Asakir jalada 1 uk. 295 na hapo haina maneno hayo ya “urefu wake” yanayodaiwa na Sh. Abdallah. Tena imeandikwa katika kitabu hicho hicho cha Ibn ‘Asakir ukurasa 294 na hapo pia haina huo “urefu” wa Sh. Abdallah. Basi jamani, Sh. Abdallah akosapo neno huropoka tu na kila neno lisilo na sura?

Tafsiri ya hadithi hii iliyoelezwa na Sheikh Ali Al-Qari ni kuwa:

لَوْمَاتُ شَابِرَاهِيمَ وَصَارَتِيَّاً وَكَذَالِكَ لَوْمَاتُ عَمِرَتِيَّاً لَكَانَ
مِنْ أَتَبَاعِهِ عَلَيْهِ السَّلَامُ فَلَوْلَيْنَا قُضِيَّ قَوْلَةُ خَاتَمِ
النَّبِيِّنَ إِذَا الْمَعْنَى أَنَّهُ لَأَيَّاً فِي بَعْدِهِ يَسْخُمُ مِلَّتُهُ وَلَمْ
يَكُنْ مِنْ أُمَّتِهِ - (مَوْضُوعَاتٍ كَبِيرٍ صَحِيفَةٌ ٤٩)

Yaani, “Angeishi Ibrahimu na akawa Nabii, na pia Umari angekuwa Nabii, wote wawili wangkuwa katika wafuasi wa Mtume s.a.w Basi haipinzi kauli Yake *Khaatamannabiyyin*, kwani maana ya kauli hiyo ni kwamba hatakuja baada yake Nabii wa kutangua mila yake na asiyekuwa katika umati wake” (Maudhu’at Kabir uk. 69).

Je, siyo “dhahiri shahiri” ya kuwa hadithi hii inaonyesha kwamba utume ungaliko lakini Ibrahimu alikufa ndiyo maana hakuupata? Hii ni hadithi sahihi kabisa, na tulivyoieleza ndivyo hasa ilivyonotakiwa ileenze. Wala sisi sio tulioibuni; wala si sisi tulioibuni maelezo hayo. Maelezo hayo ndiyo yanayoonekana waziwazi ndani ya hadithi yenye, ndiyo yanayokubaliwa na akili, nayo ndiyo yaliyokubaliwa hata na maulamaa wakubwa wakubwa kama Al-Qari wa toka zamani tuliowataja juu.

Elimu sikia
 Zinahitaji kwingi kusoma,
Si za kuibia
 Kijanja-janja na kunguruma,
Unachotambua
 Ndiyo fikihi kuumaua,
Vipi kujitoma
 Katika jambo usilojua?

MLANGO WA TATU

ALHAMDU INABASHIRI WAISLAMU KUNEEMESHWA

Sh. Abdallah anasema ati sisi tumepachika na kutafunia maneno katika maelezo ya aya za mwisho za Alhamdu. Anaonekana kuwa mwingi wa maneno ya machachari na ndaro; lakini maskini yamekatika kichwa, hayana miguu.

Wote waliosoma tafsiri yetu wanajua kuwa sisi ni mafasihi na maneno yetu hunyoka kama miali ya nuru; kisha hatuna haja ya kupachika kwani tu wajuzi na kila neno hulitoa kwa ushahidi wazi unaowapumbaza wenye kijicho, na kuwachangamsha wapendao haki na kuzinawirisha akili zao.

Maneno haya ya Alhamdu:

**إِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ۝ صِرَاطَ الْذِينَ أَنْعَمْتَ
عَلَيْهِمْ ۝ عَنِّيرِ الْمُتَضَرِّبِ عَنْهُمْ وَلَا الصَّالِبِينَ ۝**

tuliyatafsiri hivi, “Utuongoze njia iliyonyoka, njia ya wale uliowaneemesha; siyo ya (wale) waliokasirikiwa, wala ya (wale) waliopotea. (uk. 4-5). Hakuna mtu ye yote duniani anayejua Kiarabu na Kiswahili anayeweza kusema kuwa tafsiri hii ni kosa.

Sh. Abdallah amerukiza maelezo yetu

Maneno hayo tuliyaeleza muradi wake. Na kueleza muradi si kupachika. Watu wote na wafasiri wote wanafasiri na kueleza muradi wa maneno. Kueleza tafsiri si kupachika. Aya hizi tumezieleza kwa namna nzuri sana na nyepesi. Na hata kama Sh. Abdallah angeyaandika maneno yetu vile tulivyoyapanga wenywewe watu wangeona mara moja uhafifu wa mawazo yake. Amepangua mpango wa maneno yetu, akaweka wake mwenywewe; kisha akauliza maswali ambayo yamekwisha jibiwu ukurasa ule ule wa tano juu. Yeye amerukiza maelezo yanayoanza na mstari wa kwanza wa fungu, akaanza na mstari wa 22. Je, kutupa na kumegua siko huku kunakomsuta Sh. Abdallah?

Maelezo tulioanza nayo ni haya: "Walioneemeshwa ambao Mwislamu anafundishwa kuomba apewe neema zile walizopata wao, ni watu ambao wametajwa katika sura 4: 70, yaani Manabii, Masiddik, Mashahid na Masalih (watu wema). Kadhalika katika sura 5: 21 neema hizo zimesemwa kuwa ni unabii na ufalme. Aya hii inadhihirisha ya kuwa neema hizo zote zitaendelea kupatikana.

Manabii wataendelea kufika, Mawali kadhalka. Mashahidi na Masalih pia watafika. Hii ndiyo dalili inayohakikisha kuwa dini ya Kiislamu iko hai, na inaendelea kuangaliwa na Mwenyezi Mungu"

Tafsiri hii ndiyo inayoonekana bayana katika aya hizi, wala mjuzi wa Kurani hana haja ya kuitafuta kwa umuli wa moto, maana haiko gizani. Kisha basi tafsiri hii ni moja katika tafsiri zilizokubaliwa na Imam Raghib Asfahani kwa kuhusiana na aya 70 ya sura ya 4, kama tulivyotaja; nayo imebainishwa, kama tulivyokwisha taja katika Tafsiri ya Kurani, katika kitabu Al-Bahrul Muhit, jalada ya 3 uk. 287, ambacho ni kimoja katika vitabu alivyovikwepa Sh. Abdallah. Imeandikwa:

وَقُرْنَةً مَعَ الدِّينِ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ تَفْسِيرٌ لِفُولَمْ صِرَاطٌ
الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ وَهُمُ الَّذِينَ ذُكْرُوا فِي هَذِهِ الْأِيَّةِ
وَالْغَلِيلُ هُرَانٌ فَوْلَهُ مِنَ الشَّيْئَنَ تَفْسِيرٌ لِلَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ
عَلَيْهِمْ فَكَانَهُ قَتْلًا مَنْ يُلْعِنَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ مِنْكُمْ أَرْحَقُهُ
اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَدُّهُنَّ تَفْدِيمُهُ مِمَّنْ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ قَاتَ
الرَّاغِبُ مِمَّنْ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنْ الْفِرقِ الْأَرْبَعَ فِي التَّزَكَّةِ
وَالشَّهَابَ الْأَنْجَى بِالنَّبِيِّ وَالصَّدَقَةِ بِالصَّدَقَةِ وَالشَّهَادَةِ بِإِيمَانِ
الشَّهِيدِ وَالصَّالِحِ بِالصَّالِحِ وَاجْزَاءُ الْأَنْجَى أَنَّهُ يَتَعَلَّقُ
مِنَ الشَّيْئَنِ بِفُولَمْ وَمَنْ يُلْعِنَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَىٰ مِنَ الشَّيْئَنِ
وَمَنْ بَعْدَهُمْ - (الْبَحْرُ الْمُجِيْط جَلْد٢ صَحِيفَة٢٨٢)

Tafsiri: “Na kauli Yake: *Miongoni mwa wale Aliowaneemesha* (4:70) ni tafsiri ya kauli Yake, *Njia ya wale Uliowaneemesha* (iliyoko katika Alhamdu). Nao ndio watu walijotajwa katika aya hii (ya 4:70). Na dhahiri ni kwamba kauli Yake *Miongoni mwa Manabii ni tafsiri ya (maneno) Ambao Amewaneemesha*. Ni kama kusema, mionganoni mwenu atakayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Mwenyezi Mungu atamwunganisha na wale walijotangulia, katika aliowaneemesha. Raghib akasema, Katika wale aliowaneemesha katika Makundi manne katika cheo na malipo. Nabii kwa Nabii, Siddiki kwa Siddiki, na Shahidi kwa Shahidi na Salih kwa Salih. Naye Raghib akaruhusu kuunganisha (kauli) Katika Manabii na kauli Yake Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume yaani katika Manabii na walio baada ya hao.

Maneno hayo yanaonyesha wazi ya kuwa aya za mwisho za Alhamdu zinaelezwa katika aya 70 ya sura 4, kama ambavyo tumeeleza sisi. Tena tafsiri hii inaonyesha ya kuwa huko “kuwa pamoja” ni kuwa pamoja kwa kupata Waislamu vyeo na thawabu: Nabii kwa Nabii na Siddiki kwa Siddiki na kadhalika - kama vile watu wa zamani walivyopata vyeo hivyo. ndivyo Waislamu watavipata. Kisha inaonyesha mwishoni ya kuwa wanaosemwa kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume watakuwa Manabii watakaofika kumtii Mungu na Mtume Muhammad s.a.w. na pia walio baada ya Manabii yaani. Masiddiki. Mashahidi na Masalih.

Hiyyo, ingawa wafasiri wa zamani pengine tafsiri ya kosa juu ya Khaatamannabiyyin na hadithi La nabiyya baadi iliwakwaza sana, lakini tafsiri iliyo bayana ya aya hizi za kuendelea utume pia haikukosa kuwadhihirikia baadhi yao. Waliokuwa mashujaa wakazieleza kwa usawa bila kuogopa lawama na kelele za watu. Wengine wakaeleza maneno yenye ncha mbili - yanayokubali huku na huku. Tafsiri hii ya kuendelea utume ingekuwa si tafsiri iliyo bayana ya aya hizi haingeweza kupenya ndani ya kichwa cha mtu ye yote anayesadiki kuwa mlango wa utwne umefungwa. Lakini tafsiri hii iliwapenya wengi na wakaiandika.

Zaidi ya hayo, wafasiri wengine, ama kwa woga au kwa kutojua undani wa elimu hizi za Kiungu ambazo kuzielewa kwahitaji zaidi moyo uliotakasika, wao wakaenda kinyume na aya hizi. Wakazipa tafsiri ambazo dhahiri hazielekei akiliini mwa mwenye akili. Na

hizo tafsiri zisizoelekea ndiyo yake elimu anayojua Sh. Abdallah. Nina yakini kama Sheikh Abdallah aondoe woga na apende kumcha Mungu asijali heshima hiyo ndogo aliyopewa na watu ambaao sasa wanaonekana kumtawala yeye pamoja na elimu yake, kama ajiepushe tu na vuguvugu hili la dunia, kisha atakase moyo wake, hatakosa kuona ukweli na haki tulioiona sisi.

Neema zilizoahidiwa

Kama Sh. Abdallah angejali maneno haya asingeuliza, “Wapi katika maneno haya ya “Utuongoze njia iliyonyoka, njia ya wale Uliowaneemesha” panapoonyesha kuwa watu wengine watapata utume?” Kwani, ni wazi Mwenyezi Mungu ametufunza tuombe dua hiyo. Sasa swalii ni hili: hao walioneemeshwa ambaao sisi tumefunzwa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe tuombe kuongoka ndani ya njia yao, ni neema gani walizopewa hata wakasemwa wameongoka?

Tunapofunua sura ya 4:70 tunakuta maneno haya:

الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ الْبَيْنِ وَالْقِدِيقَيْنِ
وَالشَّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ - (الْإِسْرَاءَ ٧٠)

Yaani, “Ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha yaani Maanabii, Masiddiki, Mashahidi na Masalih.” Ndiyo kusema, hapa pametajwa neema namna nne za Mwenyezi Mungu: Unaabii, Usiddiki, Ushahidi na Usalih.

Na katika sura 5:21 Mwenyezi Mungu amesema:

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ يَقُولُمَاذْ كُرُوا إِنْ قَمَةً اللَّهُ عَلَيْكُمْ
إِذْ جَعَلْتُ فِي كُمَا أَبْيَأَ وَجَعَلْتُكُمْ مُؤْنَكَأً (الْمَائِدَةَ ٢١)

Yaani. “Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, Alipowafanya Manabii kati yenu na akakufanyeni wafalme.” Hapa Nabii Musa amewakumbusha watu wake neema za namna mbili

walizopewa, nazo ni baadhi yao kufanywa Manabii na taifa zima likafanywa lenye kutawala. Hizo ndizo neema zinazoelezwa waziwazi na Kurani, lakini Sh. Abdallah hazoni. Amefanana na mtu anayefumba macho mchana kweupe kisha anauliza, Jua liko wapi? Ewe! Kwanza fumbua macho yako kisha utaliona juu.

Na Mwenyezi Mungu amefundisha sura ya Alhamdu na amemtaka kila Mwislamu aombe kila siku katika kila raka ya sala kusema, “Utuongoze njia iliyonyoka, njia ya wale uliowaneemesh.” Na neema ambazo tumekwisha ziona walizoneemeshwa watu hapo zamani ni kufanywa Manabii, Masiddiki, Mashahidi na Masalih na pia kupewa ufalme wa kidunia.

Waislamu wamepewa Neema hizo

Hivyo kama Mungu Mwenyewe ametufunza kuomba tuitishwe njia ya waliopewa neema hizo, je ni muradi wake ya kuwa sisi Waislamu tutakapopita njia yao hatutapata neema walizopata wao? Je, ni maana yake kuwa Mwenyezi Mungu ametufunza tuombe neema ambazo hana haja ya kutupa? Na ya kuwa dua hii iliyooombwa na Mtume wetu Muuhammad s.a.w. mara maelfu na maelfu katika uhai wake, ikaombwa na Masahaba, ikaombwa na Mawali, ikaombwa na Waislamu wote, Mungu hakuwa na haja na kuijibu na kuwapa Waislamu neema walizorithishwa watu wa zamani? Je hii fikira ya Sh. Abdallah ya kukataa Waislamu kupewa neema hizi ni jambo ambalo Mwislamu ye yote na akili zake anaweza kulikubali? La! Bali Mwenyezi Mungu alijibu dua hii na Waislamu wakapata neema hizo. Seyidna Abu Bakar alipewa cheo cha Usiddiki na kadhalika mawali wengine. Waislamu waliokufa katika jihadi walipewa mara moja cheo cha Ushahidi, na hata wengine walio hai kama alivyofundisha Mwenyezi Mungu katika dua hii *Rabbana aamanna faktuubnaa ma'ash-shaahidiin* (Ee Mola wetu tumeamini, basi utuandike pamoja na Mashahidi). Na wengi Waislamu ni Masalih, yaani watu wema. Wengine walipewa ufalme pia na wako wanaotawala mpaka leo. Sasa neema ya Unabii ni moja katika neema hizo zilizoahidiwa, kwa nini Waislamu wasiipewe kama ambavyo wamezipewa neema nyinginezo?

Hivyo, Sh. Abdallah anapotuuliza na kusema, “Iko wapi kuwa

Mwenyezi Mungu katuahidi hapa au penginepo kuwa atawapa baadhi yetu utume?” bila shaka anauliza swalii lisilomfaa mtu kama yeze anayedhaniwa na watu kuwa ana elimu. Na anaposema, “Si wamejipachikia hayo?” anajifanya kichekesho. Mwenyezi Mungu alisema kweli aliposema:

أَمْ تَعْسِبُ أَنَّا كَنْتُمْ يَسْمَعُونَ أَوْ يَعْقِلُونَ إِنْ هُمْ
إِلَّا كَذَّابٌ نَّعَمْ بَلْ هُمْ أَضَلُّ سَبِيلًا - (الْفُرْقَانُ ٤٥)

tafsiri, “Au je, unafikiri kwamba wengi wao wanasiakia au wana akili? Hao sio ila ni kama wanyama, bali wao wameipotea zaidi njia.” (25: 45).

Upinzani wake unajiishia wenyewe

Itakaposomwa aya ile ya 70 ya sura ya 4 pamoja na maelezo haya, upinzani wa Sh. Abdallah utajiishia wenyewe. Juu ya hayo ni wajibu wetu kubatilisha lawama zake zote ili isibakie shaka hata kidogo katika miyo ya watu wenyewe akili wanaotaka kujua habari zote sawasawa.

Sisi tulitafsiri aya ya 70 ya sura ya 4 hivi: Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao ni mionganini mwa wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu - Manabii na Masidiki na Mashahidi na Masalih: na hao ndio marafiki wema.”

Sh. Abdallah ametulaumu kuwa tumepindua tafsiri ya tamko la *ma'a* tukatia la *minhum*, yaani maneno yale tulioandika *mionganini mwa anataka yangeandikwa pamoja na*.

Baada ya kutulaumu hivi katika uk. 5 wa kijitabu chake, ya kuwa neno *ma'a* tumelipa tafsiri ya neno *min*, roho yake ikaanza kumlaumu kuwa asemavyo si kweli, hivyo, hakukawia kusahihisha kosa lake kiujanjanjanja, kwa kujitutumua na makeke, akakubali kuwa neno *ma'a* wakati mwингine lina maana ya *min* katika lugha. Na kwa kauli yake hii lawama aliyotulaumu imebatilika.

Kwanza akatulaumu akasema, “Wanaigeuza tafsiri ya maneno na ule mweko wake wa lugha” na chini ya maneno yake haya akajivunja

mwenyewe kwa kusema, “Na huko kusema kwao katika mstari wa 29 wa sahifa 162 kuwa *ma'a* inakuja kwa maana ya *min*, tunawaambia, ndiyo wakati mwengine inakuja kwa maana ya *min*,” Sasa kukubali kwa makeke na kiujanja-ujanja namna hii ndio watu wamdhanije?

Kiasi hiki cha maneno yake kinampa kila mwenye akili kuona ya kuwa tulipotoa tafsiri ya neno hilo hatukuvunja kanuni ya lugha ya Kiaribu, hatukugeuza tafsiri ya mweko wa lugha wala hatukufanya ila sawa na kanuni ya lugha yenyewe, na jambo hili limekwisha kuwa wazi, amelikubali mwenyewe haraka haraka kabla sisi kumsuta.

Linalomfanya yeye akatae maana hiyo iliyo wazi kabisa katika lugha, kama asemavyo, ni kwamba “Mwenyezi Mungu kisha twambia kuwa haji Mtume mwengine - Nabii Muhammad ndiye Mtume wa mwisho” (mstari wa 13-14 uk. 6). Ndiyo kusema, sababu hasa inayompa kutulaumu juu ya neno hilo si “mweko wake wa lugha” kama alivyosema mbele, bali ametulaumu kwa sababu ya itikadi yake ya kuwa Mtume wetu ni wa mwisho. Ndiyo kusema, Kama, kwa mathali ya maneno, Mtume wetu angekuwa si wa mwisho, aya hiyo bila shaka ingekubaliwa kuwa na maana ya kufika Manabii, Masiddiki, Mashahidi na Masalih.

Sasa, nyote waungwana, mnajua ya kuwa, kama Mtume Isa aje tena duniani, ni nani atakayesemwa amefika duniani mwisho wa wote? Ni wazi ya kuwa Nabii Isa ndiye atakuwa wa mbele na wa mwisho. Sh. Abdallah anasadiki kuwa Nabii Isa atakuja kuwa kifunga mlango hapa duniani. Ndiyo kusema, aya ile tafsiri anayoibandika si tafsiri iliyo sawa na mweko wa lugha wala si tafsiri iliyo sawa na taawili anayotuambia ya kusabibishwa na umwisho wa Mtume. Ni tafsiri ya kuvungavunga, “ya kuparanganya” na “kuvungua”. Na jambo hili sasa limekuwa wazi kwenu nyote.

Neno *ma'a* lina maana gani?

Neno *ma'a* limekuja katika Kurani Tukufu mara zisizopungua mia na arobaini na mbili. Kuna mahali ukilifasiri kwa maana ya kuwa *pamoja na halikubali*; kwa mfano katika sura 3:194 Mwenyezi Mungu anapotufundisha kuomba dua hii:

وَنُوقَنَامَةُ الْأَبْرَارِ (آلِ عَمَّرَانَ ٤٤)

Yaani, “Utufishe pamoja na watu wema.” Sasa, siyo maana yake kuwa wanapokufa watu wema nasi tufe pamoja nao; bali maana yake ni kuwa nasi tuwe wema, tunapokufa tuwe mionganoni mwa watu waliokufa katika hali njema.

Mahali pengine kulifasiri “kuwa pamoja na” bila kushirikiana sifa, halikubali, kama lilivyo katika aya hiyo hiyo na katika aya hii ya 4:70 na 4:147 na pengine pengi.

Kama nilivyokwisha sema, vyeo hivi Waislamu wanavipewa hapa hapa duniani. Siyo kwamba Waislamu mionganoni mwao hawatakuwamo masalih au mashahidi masiddiki au Manabii, bali wawe tu peponi wakitembeleana na watu wa nyimati za zamani wenye vyeo hivyo, bila wao kuwa navyo hivyo vyeo, kama adhanivyo Sh. Abdallah. Basi ni heshima gani watakayokuwa wamepewa Waislamu? Watu wa zamani wawe na vyeo, na Waislamu wasiwe na vyeo, bali iwe kazi ya Waislamu kuwazuru na kuwatazama mabwana wa zamani wenye vyeo. Kama mfano wa watu tu kuhudhuria baraza la mfalme na kumwona bila kuwa na cheo, je hali yao itakuwa sawa na hali ya wafalme wengine na mawaziri na maliwali na makadhi waliohudhuria baraza ile? Je, ni nani wametukuzwa zaidi: Waislamu wasio na vyeo waliomo peponi au wale wenye vyeo waliomo humo amba ni watu wa nyimati za zamani? Fikirini hapa enyi mabwana wenye akili. Haya maneno anayofundisha Sh. Abdallah si upotofu dhahiri huu?

Isitoshe katika Kurani Waislamu wameitwa umati bora, kama asemavyo Mwenyezi Mungu.

كُتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتٌ لِّلنَّاسِ . (آلِ عَمَّرَانَ ٢٢)

“Ninyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya watu” (3:111). Sasa Waislamu watakuwa na ubora gani kama wasipewe vyeo hata kama vile walivyopewa watu wa zamani? Je, waungwana, yanaelekea haya? Hii ndiyo elimu anayojigamba nayo Sh. Abdallah? Mwenyezi Mungu

amesema:

وَالَّذِينَ امْنَوْا بِآيَاتِهِ وَرُسُلِهِ أُولَئِكَ هُمُ الْمُصَدِّقُونَ
وَالشَّهَدَاءُ أَعْلَمُ عِنْدَ رَبِّهِمْ . (الْأَحْدَى ٢٠)

“Na wale walioamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake hao ndio Masiddiki na Mashahidi mbele ya Mola wao.” (57:20). Aya hii inaonyesha ya kuwa kwa kuwafuata Mitume wa zamani watu waliweza kufikia cheo cha Usiddiki kama cheo cha juu kabisa. Lakini kwa kumfuata Mtume Muhammad s.a.w. ambaye ni Mfalme wa Mitume, cheo hata cha juu zaidi ya hivyo kinaweza kupatikana, yaani cheo cha Unaabii pamoja na vyeo vingine vitatu vya chini yake, kila mtu akitukuzwa sawa na heshima aliyo nayo mbele ya Mwenyezi Mungu. Hivyo Mwenyezi Mungu akasema:

وَمَنْ يُطِّهِرْهُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ فَأُولَئِكَ مَعَ الدِّينِ أَنَّمَا اللَّهُ
عَلَيْهِمْ مِّنَ النَّبِيِّنَ وَالصَّدِيقِينَ وَالشَّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ
الْجَيْلَيْنِ وَحَسْنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا . (الْإِسْتَأْمَارٌ ٢٠)

“Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao ni mionganii mwa wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu - Manabii na Masiddiki na Mashahidi na Masalih; na hao ndio marafiki wema.” Hivi ndivyo vyeo vinne kwa ajili ya wafuasi wa Mtume Muhammad s.a.w. lakini Sh. Abdallah anapotea kwa sababu ufupi wa elimu yake umefanya itikadi yake iwe fupi, na ndiyo maana anatangatanga ovyo na maneno yasiyo na kichwa wala mkia. Seyidna Ahmad (amani ya Mungu juu yake) akasema:

إِذَا قَلَّ عِلْمُ الْمَرْءِ وَقَلَّ اعْتِقَادُهُ وَمَا يَمْدُهُ حُسْنًا فَنِزِيرٌ مُعَذِّزٌ

Tafsiri:

Elimu ya mtu inapokuwa ndogo,
Itikadi yake pia inakuwa ndogo;
Na kipofu hasifii uzuri,
Kwani ana udhuru ya kuwa haoni.

MLANGO WA NNE

ABDALLAH ANATATIZWA NA MANENO YA MAWALII

Sisi tuliandika mzizi wa maneno ya Ruhul Maani yaliyoosema kuwa utume ni wa namna mbili: ‘*Aamnah (wa desturi) na Khaassah (wa maalumu)*’, yaani, utume wa kuleta sheria sasa haupatikani, lakini utume wa desturi bado unaendelea. Na kama usome maelezo ya Sh. Abdallah yaliyoko uk. 7-8 wa kijitabu chake, utaona ya kwamba ingawa amefanya juhudhi sana ya kutaka kuiepuka roho ya maneno hayo, haikuwezekana. Hakuweza kuyafasiri kwa kuyapambanua maaneno aliyoyanakili, bado akachomeka ndani ya tafsiri yake maneno yasiyokuwako katika Kiarabu. Nayo tutayaafichua.

Utume ni namna mbili

Sisi tuliporejea kitabu hicho *Ruhul Maani* tulichukua maneno yanayoonyesha kuwa Unabii ni namna mbili, moja inadumu na namna nyingine imekoma. Na kwa kiasi hiki sisi ni sahihi kabisa wala hakuna njia yo yote ya kutulaumu juuya roho ya maneno tulioichukua.

Lakini Sh. Abdallah alichukua vipande vipande vya maneno huko na huko akayaunga pamoja kwa namna ambayo hayakuunganishwa kitabuni, akirukiza maneno mengi ya katikati yanayojaza karibu ukurasa mzima ulio mkubwa. Sasa yote yale aliyomegamega na kuyaunga pamoja yamemharibikia vibaya hata ameyaacha hivyo hivyo tu bila kuyaeleza na kuyapambanua.

Yeye ameandika maneno haya ambayo, kabla hujayasoma ingefaa ujue ya kuwa katika Kiarabu cha maneno hayo, neno *nubuwwah* (yaani, Unabii au utume au ujumbe) lililotumiwa, Sh. Abdallah wakati akilifasiri mahali pengine kalifasiri “utume” na mahali pengine kalifasiri “ujumbe.” Hivyo kwa kuwa mtu asidhani kuwa maneno hayo mawili ya tafsiri yake pengine yana maana mbalimbali, mimi ninanakili maneno ya Sh. Abdallah kwa kutumia neno tu la “utume” alilotumia mwenyewe, na kila mahali penye neno *nubuwwah* nitatumia neno hilo “utume” ili mpate kuyaelewa maneno yake. Ameandika:

“Utume wa Mwenyezi Mungu ni wa namna mbili kuna ule anaoweza kuupata kila mtu na kuna ule wanaopata watu makhsusi tu. Ama ule Utume wa Mwenyezi Mungu anaoweza kuupata kila mtu unaendelea kwa watu wakubwa. Lakini mlango wa kuitwa mtu Mtume umefungwa. Tumezui liwa kulitumia mtu mw ingine baada ya Mtume tamko la Mtume japo kuwa unaendelea mpaka sasa utume wa Mwenyezi Mungu wa kuupata kila mtu. Anayepindukia daraja ya Masiddiki na anaingia kwenye Utume; lakini mlango huo umefungwa.”

Ukiwa ni mmoja wa wanaofikiri bila shaka utaona maneno haya yaliyoandikwa na Sh. Abdallah yana shaka. Ingawa shaka iliyoko iko wazi sana. Sh. Abdallah hakuona njia ya kuyasawazisha maneno haya yanayopinzana-pinzana. Sasa sisemi kuwa alikusudia kudanganya ingawa kama angekusudia hivyo asingekuwa na ujanja wa kufanya ulio bora kuliko huo. Ila nasema, kwa bahati yake mbaya usomaji wake bado ni mteketeke. Kwa ajili hii hakuweza kujua maneno hayo yametoka wapi na wapi, na yameandikwa kuwahusu kina nani, nayo yanaendelezwa wapi na vipi.

Sasa tafadhali rejea kijitabu chake ili tukuonyeshe mambo yaliyomtatiza. Funua ukurasa 7, mstari wa saba wa maandiko ya Kiaribu ambao ameutafsiri hivi: “Unabii wa Mwenyezi Mungu ni namna mbili.” Namna moja “ni ule anaoweza kuupata kila mtu,” na namna ya pili ni ule wanaopata watu makhsus tu.” Kwa maelezo haya ya Sh. Abdallah mtu hawesi kujua ni upi “unabii wanaopata watu makhsus tu”. Sababu ni kuwa Sh. Abdallah ameyakwepa maelezo ya Ruhul Maani yanayofuati kuonyesha utume huo ni wa jinsi gani. Ajabu ni kwamba, upande Sh. Abdallah anatulaumu sisi kumegua maneno ilhali mwandishi ye yote anapochukua maneno kitabuni huchukua yale tu yaliyo ni msingi. Lakini mmeguo ni huu wake unaofanya maneno aliyoandika yasilet maana. Maneno aliyoayaepa ambayo yanaeleza ni upi unabii wa namna ya kwanza ni haya:

وَالَّذِي لَمْ يَرَهُ مِنْهَا حَتَّىٰ نَبَرَّةُ التَّسْرِيرِ -

“Na (Unabii) ule ambao hawana sehemu ndani yake ndio wa maalumu (Khaassah) yaani unabii wa Sheria.” Na maelezo ya namna

hii yanayotaja neno “Unabii wa Sheria” kwa maana ya unabii wa maalumu ndiyo tulioandika katika tafsiri uk. 162. Hii ndiyo tafsiri ya neno Khaassah iliyotolewa na mwenye Ruhul Maani mwenyewe, ambayo sisi tuliinakili. Lakini Sh. Abdallah akaikataa, akasema, “Wala hii siyo tafsiri ya tamko la khaassah.” Kisha akaleta tafsiri ambayo siyo ilioandikwa na mwenye kitabu hicho, akasema, *Khaassah* “ni ule (utume) wanaopata watu makhsusi tu”, kisha asiweze kueleza huo ni utume wa namna gani kama alivyoueleza Mwenye Ruhul Maani mwenyewe kuwa huo ni “utume wa Sheria”, kama tulivyonyakili sisi.

Zaidi ya hayo sisi tuliandika, “Unabii wa maalumu, yaani utume wa kuleta Sheria, sasa haupatikani; lakini utume wa desturi bado unaendelea.” (Tafsiri ya Kurani Tukufu uk. 162-163).

Juu ya maeleo yetu haya Sh. Abdallah akasema, “Wameparanganya hivi makusudi ili wadhanishe watu kuwa mwenye tafsiri ya Ruhul Maani anakubalisha kuwa litawajuzia jina la Utume watu wengine. Nao ni uwongo kabisa

Alikataa nini na anakubali nini?

Kila mtu atakayesoma maeleo yetu yaliyoko uk. 162 ataona ya kuwa tumeeleza kanuni tu ya mas’ala, ya kuwa utume ni namna mbili unaoweza kupatikana na usioweza kupatikana. Na hili ndilo jambo ambalo Sh. Abdallah hajaweza kulivunja. Sisi tuliandika ya kuwa unabii wa namna moja umefungwa, na wa namna nyingine unaendelea. Sh. Abdallah hapa pia amekubali usemi huu aliojaribu. kwanza kuipinza; alipoandika maneno haya ya Ruhul Maani, “Ama ule ujumbe wa Mwenyezi Mungu anaoweza kuupata kila mtu unaendelea kwa watu wakubwa.” (uk. 7 mstari 17-18). Sasa alikataa nini na anakubali nini?

Sh. Abdallah halafu akaandika maneno ya Ruhul Maani yasemayo, “Lakini mlango wa kuitwa mtu Mtume umefungwa.” Hapa pia Sh. Abdallah ameshindwa kufahamu muradi wa maneno haya. Maana haiwezekani utume uendelee bila kukatika kisha anayeupewa asiiitwe Mtume. Maana kama vyeo vya usultani, uaskari, ukarani, udaktari, ualimu, ushekhe na vinginevyo vinaendelea katika watu wakubwa kama unavyoendelea Unabii katika watu wakubwa, je, ni

maneno ya maana kusema ya kuwa atakayepewa usultani asiitwe sultani? Atakayepewa uaskari asiitwe askari? Atakayepewa ukarani asiitwe karani? Atakayepewa udaktari asiitwe daktari? Atakayepewa ualimu asiitwe mwalimu? Atakayepewa ushekhe asiitwe shekhe? Na atakayepewa unabii asiitwe Nabii??? Je, ni maneno ya kusemwa na mtu mwenye akili hayo au ni maneno ya kutapatapa?

Kama nilivyokwisha sema, Sh. Abdallah usomaji wake ni mteketeke haujkomaa. Hajui maneno ya mawali yanayokatika yanaishia wapi. Mtu akitaka kuelewa maelezo hayo ayasome pamoja na maelezo yaliyobainishwa na Sheikh Muhyiddin Ibni Arabi yaliyoandikwa katika Futuuhat Makkiyya jalada 2 uk. 3, akasema:

**فَسَدَّدَنَا يَابْ إِلَّا فِي لَقْطِ النَّبِيَّ عَلَى هَذِهِ الْمُقَادِمَةِ مَعَ تَحْقِيقِهِ
لَئَلَّا يَتَغَيَّبَ أَنَّ الْمُلْكَ لِهَذَا الْلَّاقْطِ يُرِيدُ بِنَوْءَةَ
الشَّرِيعَةِ فَيَغْلِطُ (مُؤْخَدَاتٌ مَكِيَّةٌ جَلْدٌ ص٣)**

Yaani. “Tumefunga mlango wa kulitumia tamko la Nabii katika daraja hii, ingawa hakika yake (unabii) iko ili anayedhani asidhani ya kwamba anayelitumia tamko hilo anakuusudia unabii wa Sheria, akakosea.”

Huu ndio muradi wa kufungwa mlango huo kwa ajili ya mawali, na hii ndiyo maana ya maneno ya Sh. Abdul Kadir yaliyo uk. 7 wa kijitabu cha Sheikh Abdallah ambayo Sh. Abdallah ameyakata kwa namna ambayo kufungiwa huko kuonekane kana kwamba kunamhusu kila mtu. Baada ya kuyakata akachomeka ndani yake maneno matano ya Kiswahili yasiyokuwamo katika Kiarabu. Maneno aliyoyapenyeza ambayo yanabadilisha kabisa muradi wa maneno hayo, ni haya: “mtu mwininge baada ya Mtume”; naye kwa kutaka kuwaduwaza na kuwavuruga mafundi wa usomaji wa Kiswahili wasiojua Kiarabu, hakuyatia maneno hayo ndani ya vifungo hivi: () vya parenthesis ili kuonyesha kuwa hayo ni maneno yaliyoongezwa, si ya asili. Hakubainisha jambo hili ingawa maandiko yake yamepigwa chapa mara mbili, na hivyo alikuwa na nafasi ya kusahihisha ili watu wasidanganyike. Lakini kwa kuwa alikusudia kuwadanganya, hakuyasahihisha. Ajabu! ajabu! ya Bwana huyu. Watu wasiomwogopa

Mungu pengine huwastahi watu, lakini Bwana huyu hata hajali kama watu wanaweza kumdharausana watakapojuwa udanganyifu wake huu. Sisi tunajikinga kwa Mungu; naye asipotubu atajuta!

Hivyo, tunamrudishia mwenyewe hayo maneno yake matano aliyopenyeza, na tunakariri tafsiri ya maneno hayo kama alivyoitafsiri mwenyewe. Inasema: "Tumezuiliwa kulitumia tamko la Mtume japo kuwa unaendelea mpaka sasa ujumbe wa Mwenyezi Mungu wa kuupata kila mtu." Haya ndiyo maneno ya Sheikh Abdul Kadir (qaddasallahu sirrahu) yaliyoko katika Ruhul Maani. Maneno haya ni sawa na maneno ya Sheikh Muhyiddin niliyoyataja hapa juu; nayo yameelezwa kama hivyo, bali kwa uwazi zaidi katika kitabu *Al-Yawaqiu wal Jawahir*, jalada ya 2 uk. 35, akasema Sheikh Abdul Qadir:

أُوْفِيَ الْأَنْبِيَاءُ اسْمَ الْبَوْهَةِ وَأُوتِبَنَا الْلَّقَبَ أَىٰ حُجَّرَ عَلَيْنَا
اسْمَ النَّبِيِّ مَعَ أَنَّ الْحَقَّ تَعَانِي بِخَلْدٍ نَافِ سَكَرًا إِنَّا بِمَعَا
فِي كَلَامِهِ وَكَلَامِ رَسُولِهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَسِيمَىٰ صَاحِبِ
هَذَا الْمَقَامِ مِنْ أَنْبِيَاءِ الْأَوَّلِيَاءِ -
(الْيَوَاقِيْتُ وَالْجَوَاهِرُ لِعَبِيدِ الْوَهَابِ الشَّقَرَانِيِّ جِنْد٢ صِفْط٣٥)

yaani, "Manabii wamepewa jina la unabii, na sisi (mawalii) tumepewa Laqab (cheo), yaani tumekatazwa jina la unabii ingawa Mwenyezi Mungu, sawa na wao, anatueleza katika nyoyo zetu maana za maneno yake (ya Kurani) na za maneno ya Mtume wake (Muhammad s.a.w.), na mtu mwenye cheo hiki ni katika Manabii-Mawalii."

Maneno ya mawalii hao wote yanaonyesha waziwazi ya kuwa mawalii walijua kuna namna moja ya utume inayoeendelea, lakini wao, juu ya vyeo vyao vikubwa na kujua kwao siri nyingi, hawakuruhusiwa kulitumia tamko hilo, na mlango huo kwao ukafungwa. Lakini basi, kama Mungu Mwenyewe atamwita mtu Nabii, basi watu pia watalazimika kumwita mtu huyo Nabii.

Na hii hii ndiyo maana ya maneno ya Ruhul Maani yaliyonakiliwa na

Sh. Abdallah uk. 8 mwanzoni, yasemayo, "Anayepindukia daraja ya Masiddikina anaingia kwenye utume; lakini mlango huu umefungwa." Maana unabii hauchumwi bali ni kitu cha kupewa tu. Nabii huzaliwa na asifanye kosa lolote la dini kwa fadhili maalumu ya Mwenyezi Mungu, akapinduka madaraja yote mpaka kukabidhiwa daraja ya utume. Lakini Masiddiki, yaani Mawalii, kwa sababu maisha yao ya nyuma hayakuwa katika ulinzi maalumu, hivyo ingawa wanawenza kukipinduka cheo cha usiddiki au cha uwali - na hakuna cheo kingine baada ya hicho ila cha unabii - lakini Mungu akawazuilia wasitumie kwa ajili yao tamko la Nabii.

Maana, kama imeandikwa "Anayepindukia daraja ya Masiddikina anaingia kwenye utume; lakini mlango huu umefungwa" mtu ana haki ya kuuliza: anaingiaje kwenye utume na hali mlango umefungwa? Hivyo, jibu ni moja tu lilokwisha bainishwa na mawalii wenyewe ya kuwa mlango huo umefungwa kwa ajili ya Mawalii. Lakini Manabii kama Isa watakapofika hawatakatazwa kujitumilia tamko la Nabii; nao hawataleta dini mpya, bali watakuwa watumishi tu wa Mtume Muhammad s.a.w. Je, si heshima ya ajabu kabisa hii kwa ajili ya Mtume wetu? Hakuna Nabii ye yote aliyefadhiliwa kiasi hiki hapo zamani, na hata baadaye Nabii wa kumpita Muhammad s.a.w. hatatokea. Mpaka hapa tumebatilisha masingizio aliyotushtaki Sh. Abdallah kuwa tumemegua maneno, kwani maneno yote yanapatana kabisa na vile tusemavyo. Sasa tutaambiwaje tumemegua maneno na kuacha mengine hali yale yanayosemwa tumeyaacha ndiyo yanayotusadikisha zaidi. Yeye ndiye aliyeyamegua, akazidisha ndani yao matamko yasiyokuwako ndani ya Kiarabu chenyewe, na juu ya hiyana yote hiyo maaneno yakamchachia, yakamzungusha akili na yakapiga mafundo.

Mfuasi wa Mtume Muhammad s.a.w.

Lakini Seyidna Ahmad a.s. aliyepewa hasa cheo cha Unabii, alikitumia, nasi sote tunaomfuata tunasadiki kwa roho zetu ya kuwa yeye alikuwa Nabii mfuasi wa Mtume Muhammad s.a.w. Na kila mwene nia safi atakaposoma vitabu vya Seyidna Ahmad a.s. hatakosa kumsadiki. Lakini hawa wanaompinza wengi wao hata hawajui anasema nini. Wanampinga tu kwa sababu ya kijicho na kwa sababu ya uovu wa roho zao. Seyidna Ahmad a.s. hakudai lolote la kutisha au lililo

kinyume na Uislamu. Maneno aliyoyaeleza mara kwa mara katika vitabu alivyoandika kwa lugha za Kiarabu, Kifarsi na Kiurdu ni kama haya yanayotokea katika kitabu chake kiitwacho *Istiftaa*, *Dhamimah Haqiqatul Wahyi* uk. 64. Ameandika:

وَالنِّبُوَةُ قَدْ أَنْقَطَعَتْ بَعْدَ نَبِيًّا صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَلَا كِتَابٌ
بَعْدَ الْفُرْقَانِ الَّذِي هُوَ خَيْرُ الصُّحُفِ السَّابِقَةِ وَلَا شَرِيعَةٌ
بَعْدَ الشَّرِيعَةِ الْمُحَمَّدِيَّةِ بَيْدَ إِنِّي سُمِّيَتُ نَبِيًّا عَلَى إِسْلَامٍ
خَيْرِ الْبَرِّيَّةِ - وَذَلِكَ أَمْرٌ ظَلَّ مِنْ بَرَكَاتِ الْمُتَابَعَةِ وَمَا
أَرَى فِي نَفْسِي خَيْرًا وَجَدْتُ كُلَّمَا وَجَدْتُ مِنْ هَذِهِ
النَّفْسِ الْمُقَدَّسَةِ - وَمَا عَنِي اللَّهُ مِنْ تَبَوُّفٍ إِلَّا كُثْرَةٌ
إِمْكَانَةٌ وَالْمُحَاكَمَةٌ وَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى مَنْ أَرَادَ فَوْقَ
ذَلِكَ أَوْ حَسِبَ نَفْسَهُ شَيْئًا أَوْ أَخْرَجَ عَنْقَهُ مِنَ
الرِّقْبَةِ النَّبِيَّيَّةِ وَإِنَّ رَسُولَنَا حَاتَّمَ النَّبِيِّينَ عَلَيْهِ الْفَقْعَةُ
سِلْسَلَةُ الْمُرْسَلِيْنَ فَلَيْسَ حَقًّا أَحَدٌ إِنْ يَدْعِ النِّبُوَةَ
بَعْدَ رَسُولِنَا الْمُعْطَفِيَّ عَلَى الطَّرِيقَةِ الْمُسْتَقْلَةِ - وَمَا يَقِنُ
بَعْدَ إِلَّا كُثْرَةُ الْكَالَمَةِ وَهُوَ بِشَرِطٍ لَا تَبَاعُ لَا يُغَيَّرُ
مُتَابَعَةُ خَيْرِ الْبَرِّيَّةِ - وَإِنَّ اللَّهَ مَا حَصَلَ فِي هَذَا الْمَقَامِ
إِلَّا مِنَ الْوَارِاتِيَّةِ الْأَشْعَعَةِ الْمُضْطَغَوَيَّةِ -
(الإِسْقَاتَاءُ صَنِيمَةُ حَقِيقَةِ الْوَحْيِ ص ٦٤)

Yaani, “Unabii umekatika baada ya Mtume wetu, amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake; wala hakuna kitabu baada ya Furkan (yaani Kurani) ambacho ni bora ya vitabu vilivyo tangulia; wala hakuna sheria baada ya sheria ya Muhammad s.a.w. Ingawa mimi nimeitwa

Nabii kwa ulimi wa mbora wa viumbe (yaani Mtume Muhammad s.a.w.); na hila ni jambo la kivuli tu cha baraka za kumfuata, nami sioni katika nafsi yangu wema wo wote; na nimepata kila nilichopata kutoka kwa Nafsi hii iliyotakasika (yaani Muhammad s.a.w.). Wala si maana ya Mwenyezi Mungu katika unabii wangu ila kuzungumza na kusema nami kwa wingi. Na laana ya Mungu iwe juu ya anayetaka zaidi ya hayo, au anayejiona kuwa kitu au anayetoea shingo yake nje ya tanzi la Mtume. Na hakika Mtume wetu ni Khatamunnabiyyin, kwake imekatika silsila ya Mitume. Basi si haki ya ye yote kudai utume baada ya Mtume wetu Mteule kwa njia ya kujitegemea. Nao (utume) haukubakia baada yake ila wa kuzungumza kwa wingi (na Mwenyezi Mungu), nao ni kwa sharti ya ufuasi (kumfuata Mtume s.a.w.) sio wa kutomfuata mbora wa viumbe. Na waallah mimi sikufikia cheo hiki ila kwa nuru za kufuata mionzi ya Mustafa.”

Sheikh Abdallah ameyakwepa

Isitoshe, tuliandika pia maneno ya Ar-Raghib katika uk. 162 yanayoonyesha kuwa Waislamu wameahidiwa katika aya 4:70 vyeo vinne usalih, ushahidi, usiddiki na unabii. Lakini Sh. Abdallah, kama alivyoyakwepa maneno ya Sheikh Muhyiddin Ibni Arabi na ya maulamaa wengine tuliowataja katika ukurasa 737 yanayohakikisha tusemayo, ndivyo ambavyo ameyakwepa maneno ya vitabu vingi vingine tuliyoyasema. Yale anayofikiri anawenza kuipurukusha nayo, anajitia kuyajibu, nayo yanamshinda na kumchachia! Yale anayoyaona mazito, hayagusiki, anayakwepa kwa kusema, “Ni mijilio vile vile na mimegilio na mipachiko” bila kuthibitisha, watu wakaona ni mijilio gani na mipachiko au mimegilio gani. Anayapita pembeni kwa kusema ati yatakuwa mengi kuyaonyesha yote. Haya yote ni maneno ya uwongo kama ambavyo nimekwisha thibitisha, na ameyasema kwa sababu ya kijicho anachoonea tafsiri yetu. Labda alifikiri atawaridhisha watu kwa maneno matupu ya kuchekesha, yasiyo na dalili. Lakini, ikiwa anaridhika kwa kuwachechesha wajinga na wajuzi wamcheke yeye, basi ameridhika na jambo lisilomfaa. Watu siku hizi ni wenye akili sana wala sio wote watakaoghibiliwa na maneno ya kijicho. Kukanusha maneno bila dalili ni mfano wa debe tupu kupiga kelele nyangi hali ndani yake halina kitu. Hivyo, maneno hayo ya Sh. Abdallah ni michachariko tu ya kutumia maneno ya Kiswahili, nasi

tumemwona! Nanyi wasomaji wangu watukufu pia mmemwona!

Mpaka hapa tumekwisha batilisha upinzani wa Sh. Abdallah juu ya maneno ya *Durrul Manthur*; tumevenja upinzani wake juu ya hadithi zilizomo katika *Ibni Majah* na tumethibitisha makosa yake na uchache wa maarifa yake juu ya maneno ya *Ruhul Maani*; na tumemaliza makeke yake juu ya tafsiri ya aya za mwisho za sura ya Alhamdu, nanyi mmejionea wenyewe na kufurahi.

Sasa kila mtu aliyesoma kwa makini yote tuliyoyaeleza, ameona ya kuwa marejeo ya vitabu vya maulamaa tulioeleza katika tafsiri ni safi kabisa, na pia fikira na itikadi zote ni safi za Kiislamu, sawa na Kurani na sawa na Sunna ya Mtume wetu Muhammad s.a.w. Dini ya Kiislamu si dini ya kina Sh. Abdallah na rafiki yake na kwamba fikira zao zenye makosa zikubaliwe tu kama amri ya Mungu. Nyote mnajua vizuri hali za watu hawa. Basi mmeliwa si leo enyi Waislamu, nanyi hamtasalimika na kuliwa kusikopasa mnakoliwa kila mara mpaka mmejikinga kwa nuru ya elimu tuliyowatoleeni ndani ya tafsiri hii. Hii ndiyo sababu inayowafanya kina Sh. Abdallah kufanya husuda tafsiri ya Kurani ambayo inakata shingo za udanganyifu wa kila namna. Basi amkeni! amkeni! Enyi mnaopenda Uislamu.

Hali ya masheikh wa tumbo ni kutaka kuzimisha nuru ya Mungu ili watu wawe gizani kila siku wapate kuliwa na kutafunwa vizuri. Ni kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

بِئْتِيْدُونَ لِيْطَقِيْفُوا نُورَ اِلَّهِ يَا فَوَّا هِمْ مَا لِلَّهِ مُتَّمَدُ فُرِّيْه (الْمَنَّٰفٰ)

Yaani, “*Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, lakini Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru Yake.*” (61:9). Hivyo, tamaa ya dunia inawachochea, nao kwa kudhani wanatetea dini wanajaribu kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao juu ya maradio na ndani ya makaratasi, na kuwazuilia watu njia ya haki, kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

وَإِنَّهُمْ لِيَصْدَرُونَهُمْ عَنِ السَّبِيلِ وَيَحْسِبُونَ أَنَّهُمْ
مُّهَتَّرُونَ - (الزَّخْرُفٰ) ٣٧

yaani. “*Na kwa yakini hao wanawazuilia (watu) njia (ya haki) nao hudhani kuwa wameongoka*” (43:37).

Nani aliyeuonea Uislamu uchungu?

Toka Uislamu umeingia Afrika Mashariki ni miaka mingi; lakini ni nani aliyeuonea Uislamu uchungu zaidi kuliko sisi? Nyote mwaelewa ni kazi nyingi zisizo na idadi zinafanywa na Jumuiya yetu katika nchi hii na kila mahali duniani kuutetea Uislamu. Ni wafiasi wa Seyidna Ahmad waliokwenda Ulaya na Amerika kueneza Uislamu, hata maelfu na maelfu ya watu waliokuwa Wakristo sasa wanasema LA ILAHA ILLALLAHU MUHAMMADUR-RASULULLAH. Ni Jumuiya yetu inayopiga chapa magazeti katika lugha kadha wa kadha kuutetea Uislamu na kuulinda kwa namna ambayo hawa watu mpaka sasa hawajaweza kufanya hata thuluthi ya kazi tunayoifanya kwa ajili ya Uislamu. Je, inaelekeea ya kuwa wale wanaofanya kazi wawe hafifu na wale wasioshughulika na hawajui njia wawe ndio safi?

Je, ni sisi au ni wao waliopata kutangaza tafsiri ya Kurani nzima? Padre Dale alitangaza tafsiri ya kudharau kabisa Uislamu na kuutukana, na akaandika vitabu vingine vingi. Hawa kina Sh. Abdallah na Ali Muhsin hawana habari ya tafsiri ya Padre Dale? Watuambie, ni kitabu cha kurasa ngapi walichopata kuandika ili kuvunja upinzani wa Padre Dale. Je, Padre Dale hakuwa pamoja nao huko Unguja? Mbona hawakujibu hata hoja zake chache alizoandika katika kitabu chake “Maisha ya Muhammad”? Sh. Abdallah aliandika kitabu kiitwacho “Maisha ya Nabii Muhammad”, atuambie ni kurasa ngapi alizotumia kitabuni humo kurejesha lawama za Wakristo?

Lakini sisi tumeijibu tafsiri ya Padre Dale na kusahihisha kila upotofu wake ndani ya hii tafsiri tuliyotoa. Kina Sh. Abdallah wangekuwa watu wazuri, wenye kuupenda Uislamu kwa nia isiyokuwa ya kuufanya biashara na kutajirika, kwanza wangemjibu padre Dale. Waliposhindwa kumjibu, wangefurahi kama ambavyo wamefurahi maelfu na maelfu ya Waislamu wenye roho safi kwa kusoma tafsiri ya Kurani tuliyotoa, inayokata mizizi ya dini za uwongo na kuhakikisha ubora wa dini ya Kiislamu. Lakini vile tamaa ya turbo na heshima imewashika, wanaona kijicho kuwa sasa watu watapata elimu safi

na kudharau maneno yao yasiyonyooka waliyokuwa wakiwaambia. Hili ndilo hasa linalowachochea ndani kwa ndani kutupinza. Lakini, sisi hatujali. Uislamu ni dini ya Mungu, naye ataulinda; naye Mungu Mwenyewe atahurumia Waislamu na pia atawahurumia viumbe Wake wengine wanaopotezwa na hawa kina Sh. Abdallah. Sisi tunajua sana ya kuwa tafsiri ndogo-ndogo alizotoa Sh. Abdallah za sura za Kurani zimejaa makosa na ameshindwa mara kwa mara kutafsiri maneno ya Kiarabu sawasawa. Juu ya hayo tulikaa kimya ili tusimvunje moyo, kwa kuwa tulijua anawenza kusahihisha makosa yake tafsiri yetu itakapotokea. Lakini badala ya kusahihisha makosa ya vitabu vyake kwa kuiga tafsiri yetu iliyo safi, yeye akaona husuda akaanza kutulaumu” Basi naafanye apendavyo, lakini akumbuke ya kuwa kundi la watu wanaomdanganya kwa heshima ndogo ya kidunia hawatamfaa cho chote mbele ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu atamwambia:

ذُقْ أَنْتَ أَنْتَ الْحَزِيرُ الْكَرِيمُ (الْذُخْرَانُ ٥٠)

“Onja! Hakika wewe ni mtu azizi, mheshimiwa!” (44:50) zama za kuadhibiwa. Hivyo twampa nasaha atubu upesi, arejee kwa Mwenyezi Mungu, huenda Mungu atamhurumia na kumsamehe makosa yake.

MLANGO WA TANO
AHADI YA NABII IBRAHIMU

Sh. Abdallah anapotafsiri aya ya 125 ya sura Baqara anasema “Ibrahimu akasema, ‘Na katika kizazi changu wafanye viongozi pia Mungu akamwambia, ‘Ahadi yangu hii ya kuwapa uwongozi yaani Utume haitawapata wenye kudhulumu nafsi zao’.” (uk. 11).

Tafsiri yake hii inaonyesha ya kuwa anakubali ya kwamba kilichoahidiwa katika aya hii ni utume. Kisha anasema, Utume huu utaendelea mpaka zama za Mtume s.a.w. Alipofika yeche, asemavayo, “Amesema Mwenyezi Mungu kuwa sasa basi - ahadi hii imekwisha timia.” (uk. 11).

Anamzulia Mungu

Tamko hili la Sh. Abdallah, “Amesema Mwenyezi Mungu kuwa sasa basi - ahadi imekwisha timia” tungependa kujua Mungu amesema wapi maneno hayo. Naam, Mungu alipofanya ahadi na Nabii Ibrahimu, wakati wa kutimia ahadi ile, ililazimu Mungu aonyeshe kuwa ahadi imetimia. Naye Sh. Abdallah anasema, “Amesema Mwenyezi Mungu kuwa sasa basi ahadi imekwisha timia.” Katika sura gani na juzu gani ya Kurani maneno haya ya kwisha ahadi aliyopewa Nabii Ibrahimu yanapatikana? Bila shaka Sh. Abdallah atakiri kuwa amefanya ujasiri mbaya kutamka kauli hii na kumsingizia Mwenyezi Mungu kuwa kaisema hali Kurani nzima haina maneno hayo.

Aya *Khatamannabiyin* haielezi habari zo zote zinazohusu ahadi aliyopewa Nabii Ibrahimu ya kuendelea Utume kama adhanivyo Bwana huyu. Bali aya hiyo inawajibu makafiri waliomcheka Mtume kuwa hakuwa na mtoto mwanamume, kuwa yeche si baba ya yeoyote katika wanaume, lakini yeche ni Mtume na ni *Khatamannabiyin*. Je, kuna habari katika aya hii ya kufahamisha kuwa ahadi aliyopewa Nabii Ibrahimu ya kupewa utume wazao wake wema imekatika? Funueni Kurani wenyewe katika sura Ahzaab: 33 aya 41 mjionee.

Wadhalimu Hawatapewa Neema ya utume

Zaidi ya hayo inaonekana hata katika tafsiri aliyotoa Sh. Abdallah mwenyewe kuwa sharti aliyoiweka Mwenyezi Mungu ya kutopata utume siyo kuwa hawatapata utume watakaozaliwa baada ya Muhammad s.a.w. bali ni hii aliyotafsiri Sh. Abdallah mwenyewe kuwa “Ahadi yangu hii ya kuwapa uongozi yaani utume haitawapata wenye kudhulumu nafsi zao” (uk. 11). Yaani wenyewe kujidhulumu nafsi zao, wawe kabla ya Mtume s.a.w. au baada yake, hao ndio haitawahusu ahadi hii. Ni wazi ya kuwa tafsiri aliyotoa ya aya, na maelezo yake, ni mbalimbali, havipatani; na hii ndiyo desturi yake maarufu inayosababishwa na ujinga wake. Kila mtu na ajionee mwenyewe jinsi Sh. Abdallah aliviyotaka kuijweka juu ya Kiti cha Mungu, akaondoa yaliyosemwa na Mungu na kubandika matamanio yake. Je, umati wote wa Mtume Muhammad s.a.w. watakuwa “wenye kudhulumu nafsi zao” hata wanyimwe ahadi hii ya kupewa utume? Je, hii ndiyo baraka itakayopatikana kwa kumfuata Mtume Muhammad s.a.w.?

Sh. Abdallah Hailewi Kuran

Isitoshe, Sh. Abdallah anaposema, “Na hata lau kuwa kweli unaendelea utume wa ahadi aliyopewa Nabii Ibrahimu wa kupewa Utume baadhi ya watoto wake nao wasingekuwa na stish-hadi hapa Waahmadiyya ya kumdaia Utume huyu wanayemdaia, kwani huyo mtu wao wanayemdaia huo Utume si Mwarabu wala si Yahudi akapata kuwa katika kizazi cha Nabii Ibrahim kilichopewa ahadi hiyo ya kupata Utume” (uk. 11).

Maskini huyu hajui cho chote na anajifanya kama ameelia kitu. Kelele za bure kichwani hamna kitu, husemi debe tupu! Katika sura 22 Al-Hajj aya 79, Mwenyezi Mungu amesema:

وَجَاهُهُدُوا فِي أَبْلَهٖ حَقّ جَهَادٍ هُوَاجْتَبَكُمْ وَمَا جَعَلَ
عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ مِّنْهُ أَبْيَكُمْ إِبْرَاهِيمَ هُوَ
سَمِكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلِ ذَلِكَ هُدَى إِنَّكُمْ الرَّسُولُونَ

شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ فَاقْتِلُوهُمْ
 الْأَصْلُوَةَ وَاتُّو الزُّكُوَّةَ وَاعْتَصِمُوا بِاللَّهِ هُوَ مَوْلَكُمْ فَنَعَمْ
 الْمَوْتُ وَنِعْمَ النَّصِيرُ ٧٩ (آل جعفر)

yaani, “Na jitahidini katika (njia ya) Mwenyezi Mungu jitihada iliyo haki yake. Yeye Amewachagueni wala Hakuweka juu yenu udhia katika dini, (nayo) ni mila ya baba yenu Ibrahimu; yeye aliwaiteni Waislamu tangu zamani na katika (Kurani) hii pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu na ninyi muwe mashahidi juu ya watu. Kwa hiyo simamisheni sala na toeni zaka na shikilieni kwa Mwenyezi Mungu, Yeye ndiye Mola wenu, basi ni Mola Mwema aliyofanya, na Msaidizi Mwema aliyofanya” (22: 79).

Aya hii nimeinakili ili mwone maneno tunayoambiwa sisi Waislamu kuwa Ibrahimu ni baba yetu, na kwa hiyo sisi ni watoto wake. Mungu Mwenyewe ametuhalisisha Waislamu wote kuwa watoto wa Ibrahimu, haidhuru tuwe Wamanyema, Watanganyika, Waganda, Wakanya, Wahindi, Waarabu, Wazungu, Wafarisi na wengineo. Maadamu tu Waislamu mara moja Mwenyezi Mungu anatuweka katika kundi la watoto wa Ibrahimu na kutufanya tustahili ahadi ya kupewa Utume aliyopewa Nabii Ibrahimu.

Ama kudai kuwa watoto wa Ibrahimu ni watoto wa damu na khabila peke yao ni dai linalobatilishwa na aya hiyo; na pia linabatilishwa na aya hizi nyingine:

مَا كَانَ إِبْرَاهِيمَ يَهُودِيًّا وَلَا نَصَارَى وَلِكُنْ كَانَ حَنِيفًا
 مُسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ٥٠ إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ
 بِإِيمَانِهِمُ الَّذِينَ اتَّبَعُوكُمْ وَهَذَا الِّبَيْنُ وَالَّذِينَ أَمْتَرُوا
 دُرَالَلَّهُ وَفِي الْمُؤْمِنِينَ - (آل عمران ٤٨-٤٩)

Yaani, “*Ibrahimu hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu, mtii, wala hakuwa katika washirikina. Hakika watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye na Mtume huyu na walioamini; na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa waaminio*” (3:68-69).

Aya hizi zinaonyesha ya kuwa baada ya kufika Mtume Muhammad s.a.w. Waislamu ndio wamekuwa karibu zaidi na Ibrahimu kuliko watu wengine. Yaani zile neema na baraka alizoa hidiwa Ibrahimu na watoto wake sasa zitapatikana kwa kumfuata Mtume Muhammad s.a.w.; na ya kwamba Mayahudi waliotokana na Ibrahimu kwa njia ya mwili lakini hawakushika maagizo yake; na Waarabu waliokataa kumfuata Mtume s.a.w. na wale walioingia Ukristo siku hizi wote hao hawatakuwa na sehemu katika hiso baraka. Basi aya hizi zinadokeza ya kuwa neema zile pamoja na neema ya utume zitapatikana kwa kumfuata Mtume Muhammad s.a.w. na Waislamu wa kila kabilo, wa kila rangi na wa kila nchi wanaweza kuzipewa neema hiso maadamu watamfuata Mtume Muhammad s.a.w. sawasawa.

Waahmadiyya wanaamini ya kuwa Mtume wetu Muhammad s.a.w. ndiye Taa Kubwa inayowasha taa nyangi zinazogusana nayo. Lakini Sh. Abdallah amedharau dini ya Kiislamu aliposema ati Mtume s.a.w. alikuja kufunga mlango wa neema ya utume; neema ambayo imeendelea bila kukatika toka dunia kuumbwa, kama vile mvua inavyoendelea. Kuna methali isemayo, “Chura aliyomo kisimani hawezi kuelewa kiasi cha maji yaliyoko baharini,” Kama hawa kina Sh. Abdallah wangetakasa nafsi zao, wakamwelekea Mwenyezi Mungu, wakaondoa husuda na kijicho miyoni mwao, ingekuwa rahisi kwao kufahamu elimu hisi za kiroho. Sasa kwa hakika ni zamu ya maamuma kuwaombea dua masheikh hawa kama kina Sh. Abdallah, maana kupotea kwao kumeruka mipaka yote.

MLANGO WA SITA

MAAGIZO KWA WANADAMU WOTE

Aya ya 36 ya sura AI-A'raaf Sh. Abdallah ameitafsiri hivi, “Enyi watoto wa Adam! Wakikujieni Mitume wenu wanaotokana na nyinyi, wakakusomeeni Aya zangu, basi watakaoniogopa wakatengeza amali, hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika” (uk. 12).

Katika tafsiri ya Kurani uk. 278 aya hii tuliiandikia maelezo yasemayo hivi: “Aya hii pia inaweza kufasiriwa, Kama watawafikieni Mitume. Kwa tafsiri hii haitakuwa mradi wake kwamba Mitume wanaweza au hawawezi kufika. Bali inafanana na sura 2:39 isemayo: Kama utawafikieni mwongozo kutoka kwangu; ambayo haitakuwa kamwe mradi wake kudhania kuwa pengine mwongozo hauwezi kufika. Neno *immaa* linakusudiwa kuonyesha ya kuwa kama mtapata kuwa katika wakati ambao Mjumbe wa Mungu ametokea, msikose kumkubali.” Hivi ndivyo tulivyoileza. Hivi ndivyo tulivyolanganisha maana ya neno *immaa* linalotokea katika maneno *immaa ya 'tiyannakum* (watawafikieni au kama wakiwafikieni) lilivyo sawa na neno lililomo katika sura ya 2:39. Mtu ye yote atakayesoma maelezo hayo ya juu ataona kuwa mfanano tulifananisha aya hii na ya 2: 39 ni mfanano wa kauli moja tu - wakikufikieni.

Kutusingizia maneno Tusiyosema

Lakini ajabu ni hii ya kuwa huyu Sheikh mkubwa wa Unguja ameacha maelezo yetu na kuanza kutusingizia kimachomacho maneno tusiyosema kama ilivyo desturi yake toka mwanzo wa kitabu chake mpaka mwisho. Ameandika, “Hawakusema hata wao wenyewe katika hii hii sahifa 278 kuwa aya hii ni sawa sawa na aya 39 ya suratil Baqara?” (uk. 12). Maneno yake haya yanaonyesha kuwa ati sisi tumesema aya hizi mbili ni sawasawa. Hali sisi hatukusema hivyo, bali tulifananisha maneno ya pande mbili, na hayo maneno yenyewe yanayofanana tukayaandika kwa herufi za *italics* za namna mbali ili yajulikane mara moja. Hivyo Sheikh mkubwa wa Unguja amepoteza wakati wake bure kwa maneno yasiyomfaa.

Labda anadhani kuwa neno Bani Adama maana yake si wanadamu bali ni wale watoto wawili wa Adamu - Kain na Habil, ya kwamba hao wawili ndio waliahidiwa kuwa mitume wengi watawafikia wao uwili wao. Allahu Akbar! Ujinga wa kiasi hiki ni ugonjwa dhahiri! Na ya kuwa Mitume hao watatokana na wao hao hao wawili, wakawabashiri hao hao wawili! Ikiwa ndivyo adhanivyo hivi basi Sh. Abdallah amepotea ovyo, ingefaa jamaa zake wakamtafute na kumwokota. Ama huu ni mkasa wa elimu ya huyu Bwana mkubwa! Sasa amepamia miamba watu watamjua kuliko vile walivyokuwa wakimdhani.

Kwa hakika aya hizi zinazoanza na ya bani Adama “Enyi wanadamu” ni nyingi katika Kurani, naye Sh. Abdallah anakiri kuwa Mwenyezi Mungu anaposema, “Enyi wanadamu” huwa anawakusudia watu wote (uk. 31 mstari 6 kutoka chini wa kijitabu chake). Zaidi ya hayo, aya 28 ya sura hii hii Al-A’raaf inayoanza na maneno: “Enyi wanadamu” ambayo ndani yake ina maneno yasemayo kwamba Shetani na wazao wake anatuona sisi wanadamu hali sisi hatumwoni yeye, Sheikh Abdallah amekubali kuwa inawahusu wanadamu wote kama ulivyo muradi wa maneno yake katika kijitabu hicho uk. 31 (2). Na juu ya aya hii kuna aya ya 27 ambayo pia inaanza na maneno “Enyi wanadamu”. Sh. Abdallah hawezi kusema kuwa nayo inawahusu watoto wawili wa Adam peke yao. Kadhalika katika sura hii hii aya 32 inaanza na maneno, “Enyi wanadamu”, nayo Sh. Abdallah ameitoa katika kitabu chake cha “Sala na Maamrisho yake” uk. 18 kwa kuwahusu Waislamu. Sasa atasemaje basi kuwa aya 36 ya sura hii inayosema, “Enyi wanadamu, bila shaka watawafikieni Mitume kutoka mionganoni mwenu” kuwa haiwahusu Waislamu kama zilivyo hizo nyingine? Ikiwa aya hii inawahusu watoto wawili tu wa Adamu, kitu gani basi kimefanya zile zingine ziwahusu Waislamu pia? Ee Sh. Abdallah! Kurani si ya kuparamia kwa fujo namna hiyo, utakuja juta!

Anaposema ya kuwa aya hii “Ni sawasawa na aya ya 39 ya Suratil Baqara” anakosa sana. Asome tu mara moja aya 7:36 na 2:39 kisha aseme kama amepotea au hapana. Itamfunukia ya kuwa aya 2:39 waliambiwa Adamu na wafuasi wake na aya 7:36 wameambiwa watu wa zama za Mtume s.a.w. na watakaokuja nyuma yake. Hivyo, Manabii wataendelea kuondokea mionganoni mwa Waislamu ambao wataitilia nguvu Sheria ya Mtume s.a.w. na kusimamisha dini ya Islam; na bila

shaka Seyidna Ahmad ni mmoja wao.

“Kueleza” ni kinyume na “Kubainisha”?

Sheikh huyu ameona uchungu sana kusoma tafsiri ya kipande hiki cha aya 7:36 *yaqussuuna ‘alaikum aayaatii* tuliyotafsiri, “Watawaelezeni Aya Zangu.” Anasema ya kuwa tuna taka kupoteza watu makusudi kwa sababu maneno haya tumetafsiri “watawaelezeni” na maneno yayo hayo mahali pengine katika aya ya 6:131 tumetafsiri “kuwabainishieni”.

Je, mnaona ujuzi wa Sheikh mkubwa wa Unguja? Maskini, amefunikwa na husuda mbaya inayomfanya atapetape ovyo kutafuta kuutia ila kila uzuri wa tafsiri hii ya ajabu. Wacha kuchezea Kurani usije kushukiwa na balaa! Bado hujasoma, usidanganyike bure!

Tunawauliza waungwana wote wa Unguja, Je, “Kueleza” ni kinyume na “Kubainisha”? Basi jamani Sh. Abdallah ni Mwunguja wa wapi asiyelewa hata Kiswahili?

Lo! Mtego wake umemnasa mwenyewe! Kama kutumia maneno mbalimbali yenye maana moja ni kudanganya, basi Sh. Abdallah amekwisha danganya makusudi hata zaidi ya hapo. Maneno ya aya hii ameyatafsiri hivi, “Wakakusomeeni Aya zangu” (uk. 12); na katika uk. 14 maneno yayo hayo ameyatafsiri. “Wanakusimulieni mawaidha yangu”. Kwanza alisema “Wakakusomeeni”, kisha akageuka akasema, “wanakusimulieni”. Kusoma na kusimulia ni maneno mawili yaliyo mbalimbali. Kila anayefahamu Kiswahili habishii kuhitilafiana kwa maneno hayo mawili: kusoma na kusimulia. Na kila anayefahamu Kiaribu anaelewa ya kuwa neno “wakakusomeeni” siyo tafsiri hasa ya maneno *yaqussuuna ‘alaikum* bali ni tafsiri ya maneno *yatluna ‘alaikum*. Tena neno “mawaidha” ni tafsiri ya neno la Kiaribu mau’idhah au dhikr au dhikraa, lakini ye ye ameandika neno “mawaidha” ati kuwa tafsiri ya neno Aayaatii. Basi udanganyifu wake umeunganika na ujahili.

Twawasihi wasomaji wetu wasome tena aya hiyo ya 36 ya sura Al-A’raaf na pia wasome aya iliyotangulia na iliyofuata nyuma kisha wafikiri. Wataona aya hiyo imeteremshwa kwa ajili ya watu wa nyuma

tu, wala si habari ya watu wa zamani. Aya hii inatangaza habari njema ya kuja kwa Mitume chini ya Sheria ya Kiislamu, maana neno aayaatii hapa mradi wake ni aya za Kurani tu, siyo kuleta kitabu kipya. Basi Mitume watakaotumwa kwa mwafaka wa aya hiyo bila shaka kazi yao ni kutueleza aya za Kurani zinazowashinda hawa akina Sh. Abdallah na Ali Muhsin.

MLANGO WA SABA

ISA BIN MARYAM NDIYE MASIHI

Toka ukurasa wa 16 wa kijitabu chake, mistari ya mwisho, Sh. Abdallah ameleta mashtaka mengine juu yetu juu ya aya 7 ya sura 61 As-Saf. Lakini nawaombeni waungwana msome wenyewe tafsiri yetu ya aya hiyo, wala msifuate maneno ya mtu huyu kama kipofu, maana maandiko yake yamefunikwa na wingu la kijicho. Kisha msome maelezo yake na mtazame maelezo yetu, kisha mkate shauri wenyewe.

Amebabaika sana aliposoma maelezo yetu ya aya 10 ya sura 61. Kama tabia yake, amekataa kabisa hata akaapa mara tatu, kwamba maneno tulioandika hayamo katika kitabu cha mfasiri ye yote; kisha akakubali kuwa yamo. Sijui ye ye anafikiri huu ndio ujanja wa kusema au nini? Ni kweli imesemwa ya kuwa uadui ukimzidi mtu kimo, unampoteza vibaya, kama alivyoimba mshairi:

Uadui ukizidi
Humpofusha maizi;
Ukamfanya hasidi
Mzushi na mchongezi;
Ukamfikisha hadi
Ya ujinga na uozi;
Mtu huadui mwezi
Akausema ni nyota.

Adui haoni wema
Japo tenda njema kazi;
Aizulie kilema
Japo ye ye haiwezi;
Aipakaze lawama
Ya wongo na uchochezi;
Mtu huadui mwezi
Akausema ni nyota.

Katika maelezo ya aya hiyo tulandiaka, “Karibu mufasirina wote

wanakubaliana ya kuwa ushindi uliobashiriwa katika Aya hii utatimia katika wakati wa Masihi aliyeahidiwa.”

Sh. Abdallah amesema yakuwa tumesingizia Imam Razi na Jarir kwamba wao waliandika tamko la Isa na sisi tukasema tamko la Masihi Aliyeahidiwa. Lakini bwana huyu angekuwa anajua kanuni za usomaji asingesema upuuzi wa namna hii. Anasema ya kuwa “quotation” yetu si sahihi, na hali sisi hapa hatukutumia “direct speech”; bali tukachukua maana ya maneno ya watu wengi wanaopatana, katika mistari miwili mitatu. Kadhalika akasema ya kuwa hakuna mfasiri ye yote aliyetaja “Masihi Aliyeahidiwa” bali wanasema, hayo yatakuwa wakati atapoteremka Seyidna Isa mbinguni. Sasa kila mtu anayesoma maelezo yetu kwa makini atafahamu kuwa hatukunakili neno kwa neno maelezo ya mfasiri ye yote, bali tuliani dika mradi wa maneno yao. Hata hivyo hatukusema uwongo wala hatukudanganya. Sisi tumeandika “Masihi” na maneno aliyonakili yeye ni “Isa bin Maaryam.” Je, ni tofauti gani baina ya “Masihi” na “Isa bin Maaryam”? Mbona tunasingiziwa udanganyifu? Ebu mchungue Kurani, nanyi mtaona ya kuwa katika aya 46 ya sura Ali ‘Imraan Mwenyezi Mungu amesema jina lake ni “Masihi Isa bin Maryam.” Hakika inachekesha kuona sheikh mzima kuapa mara tatu ya kuwa Isa bin Maryam siye Masihi.

Tumeandika “aliyeahidiwa” kwa sababu Mtume Muhammad s.a.w. alitoa bishara ya kuwa Masihi atakuja, kwa kusema:

كَيْفَ أَنْتُمْ إِذَا نَزَلَ أَبْنَ مَرْيَمَ فِيمَا كُنْتُمْ مِنْكُمْ (مُسْلِمٌ كِتَابُ الْإِيمَانُ)

yaani, “Mtakuwaje atakapofika kati yenu Mwana wa Maryam na atawaongozeni, atatokana nanyi”? (Muslim Kitabul Iman). Mtume alihimiza ya kuwa atakapofika Masihi ni juu ya watu kumsaidia na kumtii. Basi kulikuwa jambo gani la kudanganya katika kumwita Isa bin Maryam aliyesemwa kuwa atakuja “Masihi Aliyeahidiwa”?

MLANGO WA NANE

SHEIKH ABDALLAH ANAKUBALI NABII ISA KISHA KUFA

Miaka tisa imepita, na mengi yaliyosemwa bila kuandikwa yamesahauliwa. Lakini yaliyoandikwa na kuhifadhiwa ni mapya kama yaliyosemwa leo.

Katika barua yake ya tarehe 2 Januari 1945 Sh. Abdallah Saleh aliniandikia akasema, “Ama katika Kurani imekuja katika kutajwa Nabii Isa (1) Inni mutawaffika (2) Falamma tawaffaitani na tawaffa yote iliyomo katika Kurani nzima ni kwa maana ya kufisha, na kwa tafsiri hii ya kufisha ndiyo amefasiri Bukhari aya hizi mbili katika kitabu chake akiipokea tafsiri hii kwa Mujahid na Mujahid akiipokea kwa Abdallah bin Abbas. Hata Imam Ibni Jarir amepokea tafsiri hii kwa Abdallah bin Abbas. Lakini wanavyuoni wanaopokea hadithi za Israiliyat za wanavyuoni wa Kinasara na Mayahudi ndio wanaojitahidi kubadili tafsiri hii iwafiki hadithi zao.”

Kisha nilimwuliza Sh. Abdallah habari za kuzikwa Nabli Isa, naye akanijibu katika barua yake ya tarehe 11 Julai 1945 akasema, “Ndio tunaitakidi Mitume yote imezikwa kama wanavyozikwa watu wengine, ingawa hazikuja hadithi za kutajwa kuzikwa kwa kila Mtume.”

Barua hizi zote za Sh. Abdallah Saleh Farsy ninazo, zimeandikwa kwa hati yake ambayo inajulikana. Nami nafikiri hawezi kupinduka kuwa hakuziandika yeye kwa kuogopa watu. Kuna ushahidi wa kila namna wa nje na ndani wa kuhakikisha kuwa barua hizi ni zake mwenyewe za kuandika kwa mkono wake, naye atafanya ujinga mkubwa akijaribu kuzikanusha.

Tumeshinda

Toka mwaka 1889 Seyidna Ahmad alipotangaza kuwa Nabii Isa amekufa, tuligombezwa na baadhi ya Waislamu kila upande, hata wengine wakatoo fat’wa za kututukana kuwa makafiri zilizotiwa sahihi na mashekheshekhe wa pande mbalimbali.

Ingawa jambo la kufa Isa si geni katika Waislamu, kama lilivyo si geni jambo la kuendelea unabii, na mara kwa mara tuliwatajia vitabu, lakini walitulaumu kuwa tunapindua maneno na kuyamega na kupachika. Hawakutaka kusikia aya za Kurani zisemazo Nabii Isa kafa, wala hadithi za Mtume, wala maoni ya wanazuoni. Kila mara walituletea vitabu kama Jalaleni kutuonyesha kuwa Nabii Isa hakufa bali yuko mzima mbinguni pamoja na kiwiliwili chake.

Na sisi Waahmadiyya kusema haki ndiyo kazi yetu. Haki tunaisema tu hata kama iwachukize watu, hata kama tuuawe. Basi neno hili la Nabii Isa tulikaza bila kulegeza.

Seyidna Ahmad alijua ya kuwa dini ya Kikristo haiwezi kutetereka mpaka watu wamesadiki kuwa mungu wao Isa amekufa. Alijua ya kwamba imani hiyo haiwezi kuvunjika mpaka watu wamesadiki kuwa Nabii Isa hakufa juu ya msalaba. Basi dalili za kila namna alizikusanya na akawafunza wafuasi wake, na kazi ya kuuandama Ukristo ili kuuvunja msalaba kama ilivyotabiriwa ikaanzishwa. Na sasa kwa fadhili za Mungu maelfu na maelfu ya Wakristo wameingia Uislamu.

Wakati wote huo masheikh hawakuacha kutulaumu kwa sababu walithaminisha maneno ya mashekhe wa tafsiri zaidi kuliko maneno ya Kurani yenye. Ndiyo kusema, Kurani husema jambo kwa namna moja, lakini wao kwa sababu ya masimulizi ya kuokoteza, huanza kulieleza jambo lile sawa na masimulizi hayo likawa namna mbali kabisa na yalivyo maneno ya Kurani yenye. Na kwa sababu ya wafasiri hao dini ya Kiislamu ikalaumiwa kuwa yenye mafundisho mabaya. Mtume wetu Muhammad s.a.w. akalaumiwa kuwa mwenye sifa mbaya. Haya yote tutayabainisha mbele ya safari katika kijitabu hiki. Hivyo, Waislamu kusadiki kuwa Yesu yuko mbinguni mzima kwa miaka elfu mbili, likawa jambo lililowapa Wakristu nguvu ya ajabu, na wakasema: Twambieni ni mwanadamu gani anayekaa pamoja na Mwenyezi Mungu mbinguni katika arshi kwa miaka 2,000. Kama hakuna mwanadamu wa namna hiyo, basi Yesu atakosaje kuwa mwana wa Mungu ambaye alipaa mbinguni mzima-mzima?

Hata Masheikh wa Al-Azhar Wanasadiki

Hoja hii ya Wakristo haikuweza kujibiwa sawasawa ila na Wafuasi wa

Seyidna Ahmad ambao walihakikisha kuwa Yesu hayuko mbinguni bali kafa kama walivyokufa Manabii wote. Basi pole pole haki ikaingia ndani ya vichwa vya watu. Katika mwaka 1942 Mufti wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar Misri, Sheikh Mahmud Shaltut, akaulizwa swalii na Bwana Abdul Karim juu ya kifo cha Nabii Isa. Mufti huyo akatangaza fat'wa yake katika gazeti kuwa Nabii Isa kafa, akatoa dalili zile zile tunazotoa sisi siku zote kuhakikisha kuwa Nabii Isa kafa. Baadaye mashekhe wenyewe fitina wakamlaumu kuwa amesema maneno ya kuwasaidia Makadiani, na wengine wakamwita Kadiani. Hata imekuwa siku hizi neno Makadiani linawafahamisha watu wengi kuwa muradi wake ni watu wasemao kweli na wajuao dini vizuri, na watetezi wa Uislamu. Jina hasa la Waislamu hawa la umoja wao ni Ahmadiyya, yaani, watu wafuatao sawasawa dini ya Mtume Muhammad s.a.w.

Sh. Abdallah, kabla sijamwuliza swalii lile aliquwa kisha soma fat'wa ya Sheikh Mahmud Shaltut, naye nilipomwuliza, akakubali kuwa Nabii Isa kafa.

Sheikh mwingine wa Misri aitwaye Ahmad Mustafa El-Maraghi naye ameandika hivi karibuni tafsiri ya Kurani na ameonyesha kuwa Nabii Isa amekufa.

Sasa ni wazi ya kuwa katika jambo la Nabii Isa ambalo zamani tulitukanwa kuwa makafiri kwa kuamini kuwa kafa, sasa watu wengi sana katika Waislamu wanasadiki kabisa kisirisiri kuwa Nabii Isa kafa, kwa kuogopa fitina ya mashekhe na waalimu. Wengine wanakubali kifo chake kiujanja-ujanja na kinafiki kwa kusema, akifa, asife, tuna haja gani? au wanasemwa, ukiamini kafa ni sawa au ukiamini hakufa ni sawa. Basi dini ingekuwa sawa na fikira za waoga hawa ingekuwa kitu cha upuuzi kabisa. Ni lazima shauri likatike upande mmoja. Kama Mwenyezi Mungu alisema Isa yuko mbinguni pamoja na mwili wake naye hakufa basi nawatusadikishe kwa dalili na burhani. Lakini kwa kuwa amesema Isa kafa, basi ni lazima tuamini kifo chake.

Hivyo, hata katika jambo hili la unabii usio na sheria mpya kuendelea, maadamu sisi ndio tusemao kweli, bila shaka tutashinda pia. Nalo jambo hili litawafunukia watu wote wenyewe akili nyeupe. Kwa mfano,

waalimu wa Sh. Abdallah walisadiki kuwa Nabii Isa ni mzima mbinguni lakini Sheikh Abdallah anasadiki imani hii ya waalimu wake wameipata kwa kufuata hadithi za Kiyahudi na Kinasara. Basi kama si leo, kesho wanafunzi wengine wa Sh. Abdallah watasadiki kuendelea utume na watasema shekh wao alifuata masimulizi na tafsiri za kijinga.

Je, Nabii Isa a.s Atashuka kutoka mbinguni?

Sasa baada ya kujua kuwa Nabii Isa alikufa, naye hakwenda mbinguni, sasa ni nini maana ya ahadi ya kwamba Nabii Isa atatokea? Ni wazi hakuna hata aya moja ya Kurani isemayo Nabii Isa alipaa mbinguni. Kadhalika hakuna hata hadithi moja sahihi ya Mtume wetu Muhammad s.a.w. inayosema kuwa Nabii Isa alipaa mbinguni mzima-mzima. Bali Kurani na Hadithi vyote vyasema Nabii Isa alikufa. Sasa atarudi duniani namna gani?

Neno lilowafanya wenye ujuzi mdogo wadanganyike, ni neno nuzul lililotumiwa kwa kufika Nabii Isa ambalo pia lina maana ya “kushuka”. Lakini hakuna mahali po pote katika Hadithi za Mtume wetu paliposema kuwa atashuka kutoka mbinguni. Neno la Kiarabu nuzul limetumiwa hapo kwa maana ya kufika kwa namna ya heshima, kufika kwa mtu mkubwa. Kadhalika limetumiwa katika Kurani pia kwa maana isiyokuwa ya kushuka kutoka juu, Mwenyezi Mungu asemapo:

وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنَافِعٌ لِلنَّاسِ -
(الْحَدِيد ٢٤)

Yaani, “Na Tukakiteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu” (57:26).

Sasa hatuwezi kusema hapa ya kuwa kuteremshwa chuma maana yake kinashuka kutoka mbinguni, ilhali tunajua ya kuwa kinachimbwa ardhini. Hivyo neno nuzul linalotumiwa kwa kufika Nabii Isa, halina maana ila ya kutokea au kudhihiri au kufika kwa namna ile ile waliyokuwa wakifika Mitume wote toka zamani.

Je waliokufa hurudi duniani?

Swali bado lipo: atafikaje Nabii Isa'? Kama tukisema ya kuwa kiwiliwili chake kilichozikwa kitafukuliwa kipae mbinguni, kisha kishuke pamoja na roho ya Isa ndani yake, tutakuwa tumesemi maneno ya chendawazimu.

Zaidi ya hayo Mwenyezi Mungu amesema ya kuwa, wanaokufa anawazuia wasirudi duniani, naye Nabii Isa ni mmoja katika waliokufa. Inasema Kurani:

اللَّهُ يَتَوَفَّ الْأَنْفُسَ حِينَ مَرْتَمَا وَالَّتِي لَمْ تَمْتَ فِي
مَنَامَهَا فَيُمِسِكُ الَّتِي فَضَيَ عَلَيْهَا الْمُرْتَ وَيُرْسِلُ
الْأُخْرَى إِلَى أَجْلٍ مَّسْمَىٰ - (الزُّمُر ٤٣)

Yaani, “Mwenyezi Mungu Hutakabadhi roho wakati wa mauti yao, na zile zisizokufa, katika usingizi wao. Basi Huzizuia zile alizozikidhia mauti na Huzirudisha nyingine (ambazo zilikuwa usingizini) mpaka wakati uliowekwa” (39:43).

Hivyo Nabii Isa maadamu alikufa hawezi kurudi na kubatilisha wakati uliowekwa” (39:43).

Maneno haya yanaonyesha ya kuwa wanaokufa hawarudi duniani.

Tena Mwenyezi Mungu amesema:

حَتَّىٰ إِذَا حَلَّتِ أَحَدَ كُمُّ السَّوْءَاتِ قَالَ رَبُّ إِنِّي حُشُونَ لِعَذَابِي
أَعْمَلُ صَالِحًا فِيمَا تَرَكْتُ . لَكُمْ آنَّهَا كَلْمَةٌ هُوَ قَائِلُهَا
وَمِنْ قَرَائِبِهِمْ بَرَزَ خَلَىٰ بَيْرَهُ يُعْجِلُونَ (الْمُؤْمِنُون ١٠٠)

Yaani, “Hata yanapomfika mmoja wao mauti, husema: Mola wangu, Unirudishe: ili nifanye mema katika yale niliyoyaacha. Hapana!

Hakika hili ni neno tu analolisema; na nyuma yao iko kinga mpaka siku watakapofufuliwa” (23: 100-101).

Ni wazi ya kuwa wanaokufa hawarudi duniani. Kwa hiyo Nabii Isa maadamu alikufa hawezi kurudi na kubatilisna aya zote za Kurani zinazosimamisha kanuni hii na pia zile ambazo zinazitegemea aya hizi zilizo Muhkam.

Zaidi ya hayo, kama Nabii Isa mwenyewe akirudi, kuja kwake kutafanya aya nyingi za Kurani zitanguke au zigeuzwe (Mungu apishe mbali). Kwa mfano aya 47 ya sura 5 inasema ya kuwa Nabii Isa alipewa Injili; na pia aya 28 ya sura 57 inasema Nabii Isa alipewa Injili. Sasa mgogoro ulioko ni kwamba akirudi Nabii Isa, atatumia kitabu gani: INJILI AU KURANI? Ikiwa atatumia Injili, basi Kurani haitakuwa kitabu kitu, na maneno ya Mungu yasemayo kuwa Kurani ndicho Kitabu kikamilifu yatakuwa (Mungu apishe mbali) si ya kweli. Hivyo ni wazi hawezi kutumia Injili. Na kama atatumia Kurani, italazimu aya hizo za Kurani zinazosema aliipewa Injili zibadilishwe, ziseme atapewa na Kurani pia. Na haiwezekani maneno ya Kurani kubadilishwa.

Kadhalika Kurani imesema kuwa Nabii Isa alibashiriwa kuwa Mtume kwa umati wa Bani Israil:

وَيُعِدُّهُمْ أَنْكَابَ وَالْحِكْمَةَ وَالْتُّورَةَ وَالْأُنْجِيلَ وَرَسُولًا إِلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ - (الْعِصْرَانَ ٤٩-٥٠)

Yaani, “Na (Mwenyezi Mungu) Atamfunza (Isa) Kitabu na hekima na Taurati na Injili. Na (Atamfanya) Mtume kwa wana wa Israeli” (3: 49-50).

Hakuna maneno yo yote katika aya hii wala katika Kurani nzima yasemayo kuwa Nabii Isa atakuwa ni Mtume kwa Waislamu pia. Hivyo ikiwa ni yeye mwenyewe Isa atakayerudi, maadamu utume wake aliupata kwa kujitegemea pasipo kuwa mfuasi wa Kurani na Mtume Muhammad s.a.w., aya hii italazimu iongezewe maneno kusema ya kuwa ni Mtume kwa Waislamu pia. Na jambo hili ni muhali kwani Kurani haibadilishwi.

Hivyo, ikiwa Nabii Isa atarudi kwa kufuata Kurani au Injili yote mawili ni mambo yatakayoleta hukumu zilizo nje ya Kurani na kuivuruga dini; ikiwa ni Nabii Isa wa zamani atakayerudi.

Nini muradi wa kuja Nabii Isa?

Jibu la swalii hili si gumu kwa watu wasomaji na wachunguzi wa mafumbo ya bishara za dini. Mara nyingi muradi wa bishara za dini hauwafunukii watu mpaka jambo lililobashiriwa linapotimia, na karibu kila mara bishara za dini zimetimia kwa namna ambayo watu hawakuwa wakiitazamia. Kwa mfano, ingawa zamani Mayahudi walikuwa wameahidiwa kufikiwa na Masihi, Nabii Isa, waliendelea kumngoeja kwa namna waliyodhani wenyewe. Nabii Isa alipofika kwa namna wasiyotazamia, karibu wote walimkataa isipokuwa watu kidogo; lakini wanazuoni na mashekhe wote wa Kiyahudi walimkufurisha na wakajaribu kumwua.

Kadhalika Kurani inatwambia ya kuwa katika Taurati na Injili mna bishara za kufika Mtume Muhammad s.a.w. Lakini Mtume alipofika kwa namna ambayo Mayahudi na Wakristo hawakuwa wakiitazamia, karibu wote walimkataa mpaka leo, na kumtukana na kumsingizia. Hivyo, Waislamu nao walikuwa wanamngoja Masihi na Mahdi kwa namna walivyokuwa wakizielewa bishara za kuja kwake wao wenyewe, lakini mpango wa Mwenyezi Mungu kumbe ulikuwa mbali na vile walivyokuwa wakitazamia Waislamu. Juu ya hayo, tukisoma Hadithi za Mtume tunakuta alama-alama zinazoweza kutufahamisha ni nini muradi hasa wa kufika Nabii Isa.

Je Isa huyo atafika kwa njia gani?

Mtume Muhammad s.a.w. alisema:

كَيْفَ أَتَتُمْ إِذَا نَزَّلَ أَبْنَى مَرِيمَ فِتِيكُمْ وَإِمَامَكُمْ فِنْكُمْ (مُجَادِل)

Yaani, “Mtakuwaje atakapofika Mwana wa Mariamu kati yenu, naye atakuwa Kiongozi wenu kutoka mionganini mwenu.”

Maneno haya “Kutoka mionganini mwenu” yanaonyesha ya kuwa huyo Bin Mariamu atatokana na Waislamu wenyewe, si mtu wa umati mwingine kama ambavyo Nabii Isa alikuwa mtu wa umati mwingine wa Bani Israeil. Hivyo ni wazi ya kuwa Masihi wetu si mtu wa kutoka po pote bali wa kuzaliwa na Waislamu wenyewe. Na mtu mwenyewe aliyedai kuwa Masihi huyo ni Seyidna Ahmad (amani ya Mungu juu yake), nasi tuna yakini kabisa kuwa madai yake ni haki na kweli, yalivyo madai ya mjumbe ye yote wa Mwenyezi Mungu ambaye alitangaza ujumbe wake lakini watu zaidi wakamkataa.

Ahadi ya kufika Mujaddidin

Kadhalika Mtume wetu s.a.w. alisema:

إِنَّ اللَّهَ يَبْعَثُ لِهَذِهِ الْأُمَّةِ عَلَىٰ رَأْسِ كُلِّ مِائَةٍ سَنَةٍ
مَنْ يُعِدُّ لَهَا دِينَمَا - (أَبُو دَاوُدْ جَدْ ٢٤)

yaani, “Mwenyezi Mungu atatoa kwa ajili ya umati huu mwanzo wa kila miaka mia watu wa kuwatilia nguvu dini yao” (Abu Daud).

Hadithi hii pia inaonyesha ya kuwa viongozi wa Waislamu lazima watakuwa mionganini mwa Waislamu wenyewe, na kazi yao itakuwa ni kutia nguvu dini, nao watakuwa wafuasi wa Mtume wetu s.a.w. Basi ililazimu Masihi na Mahdi wetu awe naye mionganini mwa viongozi hao, ingawa cheo chake ni kikubwa kuliko wao.

Sh. Abdallah Saleh ameandika hadithi hiyo katika kitabu chake kiitwacho “Tarehe ya Imam Shafi” akieleza ya kuwa Imam Shafi alikuwa mujaddid wa karne ya pili; wa karne ya kwanza akiwa Omar bin Abdul Aziz. Maneno haya ni kweli, tunayajua vema na pia tunawajua viongozi hao ambao walifika mwanzo wa kila karne kwa ajili ya kuutia nguvu Uislamu. Idadi yao mpaka karne ya 13 imetajwa katika kitabu kiitwaacho Hujajul Karamah, kwa mpango ufuataao, na hivyo ukweli wa kauli ya Mtume umetimia na kuthibitika.

1. Hadhrat Omar bin Abdul Aziz.
2. Hadhrat Imam Shafi.
3. Hadhrat Abu Sharh na Hadhrat Abul Hasan Ash Sha'ri.
4. Hadhrat Abu Ubaidullah Neshapuri, na Qadhi Abu Bakar Bakalani.
5. Hadhrat Imam Ghazali.
6. Hadhrat Seyyid Abdul Qadir Jilani (qaddasallahu sirrahu).
7. Hadhrat Imam Ibn Taimiyah na Hadhrat Khwaja Muinuddin Chishti.
8. Hadhrat Hafidh Ibn Hajar Asqalani na Hadhrat Saleh bin Omar.
9. Hadhrat Imam Suyuti.
10. Hadhrat Imam Muhammad Tahir Gujrati.
11. Hadhrat Mujaddid Alf I Thani Sarhandi.
12. Hadhrat Shah Waliyullah Muhaddith Dehelwi.
13. Hadhrat Seyid Ahmad Barelwi.

Kudhihiri kwake Seyidna Ahmad

Hao ndio Mujaddidin wa karne kumi na tatu zilizopita. Mwanzo tu wa karne ya 14 Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (alaihissalaam) akatangaza ya kuwa yeye ndiye Mujaddid wa karne hii, na ya kwamba yeye ndiye Masihi aliyesemwa atafika, na ya kwamba yeye ndiye Imam Mahdi aliyebashiriwa kutokea. Ilikuwa lazima apingwe kama ilivyo desturi ya Wajumbe wote wa Mwenyezi Mungu kupingwa. Alipingwa Mtume wetu Muhammad s.a.w. sembuse nabii mwenye cheo kidogo kama yeye. Ilikuwa lazima apingwe, na hili peke yake latosha kuonyesha ya kuwa hakuwa mtu mdogo.

Juu ya hayo watu waliokuwa karibu zaidi naye na waliomjua mwenendo wake na makarama yake mara moja walasadiki madai yake wakamfuata. Ikawa wengi wanaokuja kumtazama na kuzungumza naye lazima wanapata athari ya ukweli wake na wanamkubali na kumfuata. Wengine wenye roho safi walio nchi za mbali wakaona

njozi na ndoto za kuuhakikisha ukweli wake wakamfuata. Ikawa watu wanaendelea kumfuata tu kila siku: mmoja, wawili mpaka leo watu wanaendelea kuingia Jumuiya yake.

Baadhi ya maulamaa wa India walikuwa watu wa kwanza kumkubali. Katika hao nitataja mmoja aliyekuwa mcha Mungu mkubwa wa ajabu, Hadhrat Al- Haji Hakim Nuruddin ambaye kabla ya kutangaza Seyidna Ahmad ujumbe wake, ye ye alisadikiwa na waliomjua kuwa walii mkubwa na mwanachuoni mkuu. Alijua Kurani yote kwa moyo na alikuwa Muhaddith; mtu wa kabile la Kureish katika ukoo wa Al-Faaruq. Mtu huyu mtukufu amesifiwa na Seyidna Ahmad kwa namna ya ajabu kabisa katika kitabu kiitwacho Hamaamatul Bushra. Hili latosha kwa wenyewe kuuliza kutambua ulikuwa ucha Mungu ulioje wa Hadhrat Hakim Nuruddin. Bwana mkubwa huyu ndiye alikuwa mtu wa kwanza kufanya bai'at kuwa mfuasi wa Mujaddid wa karne hii. Bwana huyu alikuwa tajiri, akifanya kazi ya utabibu maalumu wa kumwangalia afya mfalme wa Kashmir, akisifika sana kwa elimu ya utabibu pia.

Bwana huyu, mara ya kwanza tu kufika kwa Seyidna Ahmad na kumwona, alikaa hapo hapo pamoja naye mpaka kufa. Kazi kwa mfalme hakurudi kuifanya. Alikuwa akijenga jumba lake la fahari katika mji wake, hakurudi kulimaliza likakaa gofu mpaka mwisho. Mali nydingi alizokuwa nazo akazitumia katika dini na kuishi kimaskini pamoja na Seyidna Ahmad. Alipofariki Seyidna Ahmad, maelfu ya watu waliokuwa wamekwisha mkubali Seyidna Ahmad wakamchagua kuwa Khalifa wa Kwanza; naye akashika Ukhilifa toka mwaka 1908 mpaka 1914, akafariki dunia.


Seyidna Ahmad akapata wafuasi toka watu wakubwa kabisa katika vyeo vya elimu, mawakili, madaktari, maulamaa mpaka watu tu wa kila aina wakamkubali.

Kurudisha Uislam ulio safi

Seyidna Ahmad hakuongeza wala hakubadilisha chochote katika Uislamu ulioletwa na Mtume Muhammad. Ni wazi Seyidna Ahmad alihitilafiana na baadhi ya masheikh maana Waislamu walikuwa wamekwisha gawanyika katika madhehebu nydingi zinazopinzana,

na wako katika hali hiyo mpaka leo. Shia wanawaita Suni makafiri; Suni wanawaita Shia makafiri. Na hivyo, makundi 73 ya Waislamu wako katika hitilafu kila kundi likijidhani lenyewe ndilo lenye kuongoka. Hivyo, alipokuja Seyidna Ahmad kama hakimu, ilikuwa lazima mashekhe ambao walikwisha ikatakata dini ya Kiislamu katika madhehebu mbalimbali waone kuwa aliyoyasema ni kinyume na madhehebu zao. Lakini kazi ya Seyidna Ahmad ilikuwa ni kurudisha ule ule Uislamu safi uliokuwa siku za Mtume Muhammad, usio na ila wala doa, ambao sasa umefujika katika vuguvugu la madhehebu zinazokindana.

Ama wafanyao shaka juu ya kuwa Seyidna Ahmad Mujaddid wa karne hii, basi nawatuambie ni nani mwingine Mujaddid aliyedhihiri kwa amri ya Mungu kutia nguvu dini katika karne hii? Haiwezekani ya kwamba kauli ya Mtume wetu itimie katika karne kumi na tatu zilizopita lakini isitimie katika karne hii tulio nayo, ambayo sasa inakaribia kwisha.



سیدنا حضرت اقدس میرزا غلام احمد مسیح موعود و مهدی معہود
علیہ الصلوٰۃ و السلام

Mtume s.a.w. alisema ya kuwa Mujaddidin hao watatokea mwanzoni mwa kila karne, na sasa karne ya 14 inakaribia kwisha. Hivyo ni jambo moja tu lililobaki kwa ajili ya Waislamu wa kila madhehebu: ama wamkubali Seyidna Ahmad kuwa Mujaddid wa karne hii au waseme kuwa hadithi hiyo ya Mtume (Mungu apishe mbali) katika karne hii haikutimia.

Basi hivi ndivyo ilivyotimia ahadi ya Mtume wetu ya kufika Nabii Isa. Haikuwa muradi wake kwamba atafika Nabii Isa mwenyewe ambaye alikwisha kufa. Bali muradi wake ni kwamba hali ya Waislamu siku za mwisho itafanana sana na Mayahudi na Wakristo, na jambo hili limebashiriwa pia katika hadithi za Mtume wetu s.a.w. Hivyo, ikawa Mjumbe atakayewafikia apangwe jina la Isa bin Maryam katika bishara zilizotabiriwa. Na hii ndiyo hakika ya habari hii; na Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo; naye ataiingiza hakika hii katika roho zote zilizo safi; nao watamkubali Kiongozi wao na kumtii. Seyidna Ahmad mwenyewe amelieleza hivyo jambo hili mara nyingi na pia katika beti hizi mbili: yaani,

وَلِئِنْ قُلْوَبٌ بِالْيَهُودِ تَشَابَهَتْ وَهَذَا هُوَ النَّبَاعُ الَّذِي جَاءَ فَإِذْكُرُوا
فِصْرُتُ لَهُمْ مُّسِيَّ إِذَا مَأْتُمُوهُمْ وَهَذَا كُلُّ مِنْيَ لِقَوْمٍ نَفَرُوا

Tafsiri: “Lakini nyoyo za watu
Zimefanana na za Mayahudi;
Na hii ndiyo habari
Iliyofika basi kumbukeni.
Hivyo nimekuwa kwa ajili yao
Isa, walipogeuka wao kuwa Mayahudi;
Na hili latosha kutoka kwangu
Kwa ajili ya watu wenye kufikiri.”

MLANGO WA TISA

KHAATAMANNABIYYIN LINA MAANA GANI?

Sheikh Abdallah amesema katika ukurasa 19 wa kijitabu chake maneno haya, “Hakuna mfasiri yo yote tangu Qurani ilipoanza kufasiriwa hizo zama za Mtume na Masahaba mpaka hivi sasa (ila wao) aliyefasiri Khaatamannabiyyin kwa kuwa ‘Muhuri wa Manabii’.”

Kisha pole pole katika ukurasa 20 akaanza kushuka kujivunja mwenyewe kabla hatujamsuta kwa hoja yake hii ya kijinga, alipokiri ya kuwa neno Khaatam lina maana ya Muhuri; Pete; Kizibo; wa mwisho na kadhalika.

Jibu lake la kwanza lililo fupi ni kuwa tulipotafsiri *Khaatamannabiyyin* kwa maana ya “Muhuri wa Manabii” tumetoa tafsiri iliyo sawa na lugha tena ambayo ni ya asili ya neno Khatam na tena ni tafsiri yenye sifa bora.

Waama kutulaumu kwake katika mstari wa 3 wa uk. 20 ya kuwa “Wameandika hivi ili kudhanisha watu kwamba maana ya Khatam katika Kiarabu ni hayo tu ya muhuri” ni uzushi wake tu usio na haya; maana katika tafsiri tumeeleza maana tatu za Khatam, si maana moja kama atusingiziavyo, ambazo ni mashuhuri katika lugha; na maana hizo tu ndizo zinazoweza kuwa sifa njema za kusifiwa Mtume wetu Muhammad s.a.w. Maana nyaginezo za neno Khatam kama alizozitoa Sh. Abdallah haziwezi kuwa sifa njema za kusifiwa Mtume, kwa hiyo hazihitajiwi katika aya hiyo. Kwa mfano, Sh. Abdallah amesema, neno Khatam pia lina maana ya “weupe wa miguu ya farasi.” Je, itakuwa sifa njema kumsifu Mtume kwa kufuata maana hiyo ya neno Khatam kwamba yeye ni “weupe wa miguu ya farasi wa Manabii”? Kadhalika amesema neno Khatam lina maana ya mwisho.

Lakini je, kuja mwisho wa watu wengine ni sifa njema? Kwa mfano, watu watakaokuwa hapa duniani siku za mwisho watakuwa bora kuliko Waislamu wote wa zamani kwa sababu ya kwamba wao ni wa mwisho? Lo! kufikiri hivi ni kukosa kulioje! Hivyo kufasiri ya kuwa Mtume ni “weupe wa miguu ya farasi, au ni kizibo, au ni mwisho au

ni kidimbwi cha nyuma ya shingo” ni upuuzi ulioje huo!

Juu ya hayo, sisi hatukuandika kuwa Khatam maana yake ni moja tu ya Muhuri kama anavyotulaumu bure huyu Sh. Abdallah. Kwa mfano, katika uk. 735 tumeeleza maana ya kwanza ya neno Khatam tukasema, “Katika lugha ya Kiarabu lina maana ya Muhuri.” Kisha tukaonyesha kwa ushahidi wa Hadithi za Mtume kuwa neno hilo lilitumiwa toka siku za Mtume kwa maana ya muhuri.

Pili, katika uk. 736 mstari wa 20 tukaandika, “Neno Khatam pia lina maana ya pete. Kisha tukaleta ushahidi kutoka katika Hadithi kuonyesha ya kwamba neno hilo lilikuwa toka zamani likitumiwa kwa maana ya pete pia.

Kisha tukaeleza hekima ya Mtume wetu kuitwa Khatam kwa maana ya muhuri na pete chini ya kila kifungu.

Tatu tukaeleza ya kuwa kwa kanuni ya matumizi ya Kiarabu, maneno yanapoundwa kama ulivyo mwundo wa maneno *Khatamannabiyyin* ambayo kwa sheria ya nahau au sarufi yanasemwaa kuwa *mudhaaf-mudhaaf ilaihi* (possessive case au kauli ya kumiliki), neno Khatam likifuatwa na majina ya wingi (plurals), neno hilo khatam halijapata kutumika kwa maana ya mwisho. Tukasema, “Wala hakuna mfano hata mmoja katika lugha ya Kiarabu ulio kinyume na kanuni hii”

Sheikh Abdallah Kashindwa

Sisi tulitazamia ya kuwa Sh. Abdallah atabatilisha maneno yetu kwa kututolea mfano wa matumizi ya neno hilo katika Kiarabu mahali pengine po pote linapofuatana na majina ya wingi lilipopata kutumiwa kwa maana ya “mwisho”. Kuleta tu idadi ya watu wanaosema neno hilo lina maana ya mwisho si hoja. Kwani neno moja linaweza kuwa na maana nyingi na ni mpango tu wa maneno unaojulisha limetumika katika maana gani. Hoja ni kwamba neno Khatam linapopata kuwa katika mwundo huo limepata kuwa na maana ya “mwisho” katika lugha? Akijibu ndiyo, aonyeshe maandiko ya Waarabu yenye neno hilo kwa mpango huo lilipotumika kwa maana hiyo.

Jambo hili litafahamika vizuri kwa mfano huu wa neno la Kiswahili “paa”. Linaweza kuwa na maana ya mnyama wa pori aitwaye paa; maana ya paa la nyumba; maana ya kupaa moto jikoni; maana ya kupaa hewani, maana ya mshindo wa Paa! na kadhalika. Zote hizo ni maana za neno “paa”, na kila maana inajulikana kwa kuangalia maneno yaliyofuatana na neno hilo imbele na nyuma. Sasa tunaposema, “Ndege anapaa”, fikira ya kwanza tutakayopokea ni kwamba anaruka angani. Hatuwezi kudhani kuwa ndege huyo anakaa jikoni akipaa moto chini ya chungu cha wali au cha mbaazi, kwani hiyo si sifa ya ndege.

Kadhalika neno Khatam. Linapofuatana na majina ya wingi halijapata asilan kutumiwa kwa maana ya mwisho. Hivyo Sh. Abdallah anaposaili kwa mshangao kusema ulamaa “hawakuweza kujua maana ya Khatamannabiyyin ila imejulikana sasa na Wahindi wa Kiahmadiyya!” Kwanza amekwepa swali letu. Pili, Waahmadiyya wote, Wahindi, Waafrika, Waarabu na wa kila taifa wanasadiki maana hii ya mwundo wa lugha kwa kuwa ndiyo maana inayokubaliwa na lugha ya Kiarabu. Tatu, ilikuwa juu ya Sh. kuleta kutoka kwa hao maulamaa wake neno tulilotaka liletwe. Ilikuwa juu yake alete mfano wa matumizi ya neno hili ulio kinyume na kanuni ya Kiarabu tuliyoleza. Isitoshe, hayo maneno yake hayawezi kuwa hoja, kwani ulamaa wengi waliojua lugha, yeze Sh. Abdallah amekwisha walaumu kuwa wanapindua tafsiri ya aya za kufa Nabii Isa ili wazipatanishe na hadithi za Kiyahudi na Kinasara walizokuwa wakizisadiki. Na maneno haya ya Sh. Abdallah tumeyaeleza katika mlango wa nane wa kijitabu hiki. Hivyo, swali hili la Sh. Abdallah analouliza kwa mshangao ilikuwa ni mahali petu sisi kumstaajabia yeze kuona anakwepa swali tuliloweka kwa mkazo sana na badala yake analeta jambo mbali kabisa lisilopatana na mas’ala tuliyotoa.

Mwisho kabisa wa ujinga wake - bali uerevu wake, amesema, “Na huko kutia kwao ... tamko la mudhof na mudhof - ilayhi ni vunganyizo tu hizo za kufanya maneno hayo yana kima: kumbe hayana kima cha pesa mbili - kama kelele za goma bovu. Na goma bovu ndilo lenye kelele nyingi.” (uk. 28 mstari 16). Je, maneno yake haya yamejibu swali letu? Yameleta mfano wa matumizi ya neno hilo kwa Kiarabu kama lilivyo katika *Khatamannabiyyin* likapata kuwa na maana ya mwisho? Ameleta? Angeleta, kisha baada ya kutuvunja akasema kuwa maneno yetu yalikuwa goma bovu, hapo watu wangemsikia. Lakini

haleti ila anasema tu kuwa maneno yetu ni goma bovu, si ndiko kukubali kushindwa kipumbavu huku? Kwani maneno yasiyo na dalili kama hayo yake ndiyo yanaweza kusemwa goma bovu, maana ni mabovu hayana dalili, yasiyo na thamani wacha ya pesa mbili, bali hata ya senti moja.

Kwanza ndani ya tafsiri tuliiitaja habari hii kwa kifupi. Na mtu mwenye elimu fupi haelewi maneno ya mkato. Hivyo, natoa dalili zile bayana za kuhakikisha ya kwamba neno Khatam linapokuwa mudhaf-mudhaf ilaihi kwenye majina ya wingi halijapata kutumiwa kwa maana ya mwisho. Na itakuwa juu ya Sh. Abdallah kukubali waziwazi kuwa ameshindwa jambo hili au alete mfano ulio “figure of speech” katika Kiarabu neno hilo lilipopata kutumika kwa maana ya mwisho linapokuwa katika mwundo huu.

Mifano Inahakikisha Tafsiri Yetu

Sasa nitaeleza mifano michache tu katika kundi kubwa la mifano ya aina hii neno Khatam lilipotumika kwa mwundo huo. Nanyi mtaona waziwazi kuwa halina maana ya mwisho. Hivyo haliwezi kung’ang’anizwa kimachomacho maana ya “mwisho” linapokuwa katika Khatamannabiyyin ila kwa kufuata taawili tuliyokwisha ileenza.

- (1) Mtume s.a.w. alilitumia neno Khatam akasema:

اَطْمَئِنْ يَا عَمِّي فَإِنَّكَ حَانَتُمُ الْمُهَاجِرَةَ
كَمَا اَنَا حَانَتُمُ النِّسْبَتَ فِي النَّبُوَةِ - (كَنزُ الْعِمَالِ جِدْل٦ ص١٣)

Yaani, “Uwe na utulivu Ee baba mdogo (A bbas), kwani hakika wewe ni Khatamul Muhajirin katika Kuhamma kama mimi nilivyo Khatamunnabiyyin katika Unabii” (Kanzul ‘Ummal, jalada 6 uk. 178).

Je, Seyidna Abbas kuwa Khatam wa Wahamaji ni maana yake alikuwa mhamaji wa mwisho?

- (2) Tena Mtume wetu s.a.w. akasema:

أَنَا خَاتَمُ الْأَنْبِيَاءِ وَأَنْتَ يَا عَلِيٌّ خَاتَمُ الْأَوْلَيَاءِ -
(تَفْسِيرِ صَافِيُّ الْأَخْزَابِ رُكْوَعٌ ۲)

Yaani, “Mimi ni Khatamul Anbiya na wewe Ee Ali ni Khaatamul Auliya”, (Tafsir Safi, Ahzab rukuu 2).

Je, Seyidna Ali kusemwa Khatam wa Mawalii maana yake alikuwa walii wa mwisho? Mawalii kama Ghauthul A’dham Seyyid Abdul Kadir Jilani (quddisa sirruhu) walitokeaje baada yake?

- (3) Juu ya Hafidh Muhammad Al-Jazri imesemwa:

خَاتَمُ الْحُفَاظِ شَمْسُ الدِّينِ أَبِي الْغَيْرِ مُحَمَّدِ بْنِ
مُحَمَّدِ بْنِ مُحَمَّدِ الْعَزْرِيِّ الدِّمَشْقِيِّ -
(مُفَذَّةُ تَجْزِيهِ بَغْرَىِ صَ ۵)

Yaani, “Khatam wa Wanaohifadhi Shamsud-Din Abul Khair Muhammad bin Muhammad bin Muhammad Al-Jazri Ad Dimashki”. Je, huyu Bwana Muhammad bin Muhammad Dimashki kuitwa Khatam wa Wanaohifadhi, tuseme maana yake ni mhifadhi wa mwisho?

- (4) Sheikh Muhyiddin Ibni Arabi ameitwa:

خَاتَمُ الْأَوْلَيَاءِ

Khatam wa Mawalii) katika anwani ya kitabu chake Futuhat Makkiiya. Je, tuseme yeye ndiye aliyekuwa walii wa mwisho kuja duniani?

- (5) Imam Suyuti amesemwa:

خَاتَمُ الْحُفَاظِ وَالْمُجْتَهِدِينَ مُجَدِّدُ الْمِائَةِ التَّسْعَةِ

**الشَّيْءَةُ أَبِي الْفَضْلِ جَلَدُ الَّذِينَ عَنِ الدِّرْخَمِ السَّعَادِيِّ
بَنْ أَبِي بَكْرٍ الشَّهِيرِ بِالسَّيْرِ طَهِ - (الْمَقْوُمُ فِي الْأَحَادِيثِ الْمُضَوَّعِ مَسَ)**

yaani. “Khatam wa Wanaohifadhi na Wanaojitahidi, Mujaddid wa kame ya tisa, Sheikh Abil Fadhli Jalaluddin Abdur-Rahman As-Sakhawi bin Abi Bakar aitwaye Assuyuti” (Almadhu’ fi Ahadithil Maudhu’ uk. 3). Je, Imam Suyuti alikuwa Hafidh na Mujitahid wa mwisho?

(6) Abu Tammam At-Tai, mtungaji wa kitabu cha mashairi kii twacho Hamasa alipofariki, mshairi mmoja wa Kiarabu aitwaye Hasan bin Wahab akaandika ubeti huu:

**فُجُّهَ الْقَرِيبُ بِخَاتِمِ الشُّعَرَاءِ وَغَدِيرُ رَضِيَّهَا حَبِيبُ الْعَالَمِ
(وَنَيَّاثُ الْأَعْيَانِ لِابْنِ خَلْكَانِ جَلَدًا مَسَ)**

yaani, “Mashairi yamepata hasara (kwa kufa) Khatam wa watungao mashairi na bwawa la bustani yake, ndiye Habibu Tai” (Wafayatul A’yan Ii Ibni Khalikan, jalada 1 uk. 123 chapa ya Misri).

Je, huyu Habibu Tai mshairi hodari wa zamani ambaye amesifiwa kuwa bwawa linalonywesha maji bustani ya ushairi kuitwa kwake Khatam wa watungao mashairi, tuseme ye ye ndiye mshairi wa mwisho katika Waarabu?

Je, tutasema hawakuwako waliohamia Madina baada ya Abbas? Tutasema hakukuwa walii baada ya Ali? Tutasema hakukuwa Hafidh baada ya Muhammad bin Muhammad Dimashki? Tutasema hakukuwa Hafidh na mujitahid baada ya Imam Suyuti? Tutasema hakukuwa walii baada ya Ibni Arabi? Au hakukuwa mshairi baada ya Abu Tammam Tai? Ni wapi atakakojificha Sheikh Abdallah? Ni wapi atakakokimbilia kuzikwepa hoja hizi? Tunacho kijinga cha moto kinachounguza kila uzushi na kila ujinga, angalieni jinsi kinavyombabua Sh. Abdallah!

Sh. Abdallah kama anajua cha kwao Kifarsi labda ataelewa vizuri jambo hili, akijua jinsi mshairi maarufu wa khabila yake aitwaye

Anwari alivyoliewa neno Khatam. Huyu Anwari, akimsifu mfalme Ghayathud-Din akaandika kwa lugha ya Kifarsi ambayo ni lugha tamu sana kwa mashairi. Alisema:

بِرَقْوْسُدْطَانِيَّتِ خَتَمٍ وَبِزَمَنِ مِسْكِينٍ سُخْنٌ
چُون شُجَاعَتْ بَرْعَلِيٍّ وَبِرْبَرِيٍّ پَيْغَمْبَرِيٍّ

yaani, kwanza, kabla ya ubeti huu Anwari alisema ya kuwa mama yetu ardhi hajapata kuzaa chini ya mbingu hii ya kibuluu mfalme mtukufu kama Ghayathud-Din na maskini hohe hahe kama Anwari; kisha akaendelea na ubeti huo usemao: “*Kwako ufalme umekuwa khatam, na kwangu umaskini umekuwa (khatam) hivyo; kama ushujaa ulivyo (khatam) kwa Ali na unabii ulivyo (khatam) kwa Mtume s.a.w.*”

Hivyo, Anwari amemfanya Ghayathud-Din khatam wa wafalme, ye ye mwenyewe kajifanya khatam wa watu maskini, kama alivyo Seyidna Ali khatam wa watu mashujaa na alivyo Mtume wetu s.a.w. khatam wa Manabii. Je, tuseme hakukuwa mfalme baada ya Ghayathud-Din; au hakukuwa maskini baada ya Anwari; au hakukuwa shujaa baada ya Ali? Basi ni ulalamishi ulioje tena kudhani ya kuwa hakuna nabii baada ya Mtume wetu?

Sh. Abdallah naangalie maneno haya ya Farsy mwenzie aliye kuwa na maarifa zaidi juu ya matumizi ya neno Khatam kwa Kiarabu, kisha akitaka ajisahihishe kosa lake, na ajue toka sasa ya kuwa neno Khatam linapokuwa mudhaf mudhaf ilaihi kwenye ismu za wingi, kama lilivyo katika *Khatamannaabiyyin*, halijapata katika maandiko yote ya Waarabu kuwa na maana ya “mwisho”. Ubishi wa kupiga kelele tu kwa maneno ya kusema oo, ni goma bovu; oo, hayana kima; oo, hayafai pesa mbili, ni ubishi na ulalamishi unaokaribia maneno ya kihuni; wala haumpi mtu ye yote mwenye akili kudhani ya kuwa hivyo ndiyo Sh. Abdalla kisha jibu. Tunataka alete *figure of speech* ulio ni mfano wa matumizi ya mwundo huu wa neno Khatam likifuatana na maneno ya wingi ambapo limepata maana ya mwisho; lakini kono! hatapata ingawa afe katika kutafuta.

Mpaka hapa imekwisha julikana ya kwamba tulieleza maana tatu za

neno Khatam, si maana moja tu kama anavyotusingizia bure bwana huyu. Kwa hakika hana dalili yo yote ya kutuvunja, ila basi tu, ni pambani za Mtonga maji ya dafu kuoshea donda.

وَرَأَنَّهُمْ بِلِ تَالِلَهِ لَوْكَنَتْ مُخْلِصًاٌ أَرْتَيْكَ أَيَّاٍٍ وَلِكِنْ تُزَوَّرُ
وَلَوْقَبَ الْكُفَّارِيَ سَانَتْ أَمَانَةًٌ لَعَمْرِيْ هُدِيَّتْ وَمِنْتْ شَيْغَانَيْ عَيْمَرُ
وَلِكِنْ فَلَنَتْ نُنْسُونَ سُوِّيْ بَعْجَلَةٍ كَغُولِيْ هَوَىٰ وَالْغُولُ لَاهِيَّطَهَرُ

yaani:

Na wallahi bali tallahi ungekuwa mnyofu.

Nimekuonyesha dalili lakini wafanya ujanja.

Na lau kabla ya kunikufurisha ungeuliza kwa uaminifu,

Naapa kwa umri wangu ungeongozwa na
ungekuwa Shekhe mwenye busara.

Lakini umedhani dhana zilizo mbaya kwa pupa

Mfano wa pepo wa hewani, naye pepo hatakasiki.

Hoja madhubuti zimemtia kiwewe

Mmekwisha ona jinsi daima anavyotusingizia, anavyokosea na anavyodanganyika. Hayakuisha hapo, yanaendelea moja kwa moja kijitabu chake chote. Naam, hasidi haoni wala haelewi. Tazameni anavyokosea kufahamu maneno yetu.

Katika ukurasa 25 mistari ya mwisho, na pia uk. 27 mistari ya mwisho ameandika kutulaumu ya kuwa, “Si moja hii katika alama ya uwongo wa tafsiri yao hiyo kuwa kaitwa *Khatamannabiyyin* kwa ajili ya muhuri alioufua zama za kuwapelekea barua wafalme,”

Kadhalika akababaika tena kukosa kuelewa maneno yetu anaposema katika uk. 26, “Basi mlango huo ... Imam Muslim ... hakuuweka kwa kuonyesha kuwa kaitwa Khatamaannabiyyin kwa ajili ya hiyo pete ya muhuri wake anayoivaa.”

Sasa, mtu ye yote mwenye macho wazi yasiyofunikwa na kijicho, kama

asome maneno tuliyoandika, ataona ya kwamba hatujasema mahali po pote kuwa Mtume wetu s.a.w. "kaitwa *Khaatamannabiyyin* kwa ajili ya muhuri alioufua" wala istidlali kama hii haiwezi kuchukuliwa kwa hali yo yote kutokana na maneno tuliyoandika. Kadhalika hatujasema mahali po pote kuwa Mtume wetu "kaitwa *Khatamannabiyyin* kwa ajili ya hiyo pete ya muhuri wake." Sijui anatafuta nini huyu kwa uwongo ulio bayana kabisa kama huu. Je, haogopi ya kwamba watu wasasoma tafsiri yetu nao wataamlamu watakapokuta hakuna maneno yanayoweza kupewa maana hiyo? Au hii ndiyo sababu alitangaza watu wasisome tafsiri yetu ili wasing'amue uwongo huu lundo zima anaotulundikia? Angalia zilivyo dhalili hila za mtu hasidi!

Maneno tuliyoandika mwanzoni hayana ila kuonyesha maana ya neno Khatam tu binafsi yake.

Katika uk. 735 mstari 6 kutoka chini tumeandika,"Neno Khatam katika lugha ya Kiarabu lina maana ya Muhuri" Kisha tulitaja Bukhari na Muslim Kitabullibas kuonyesha ya kwamba neno la Khatam limetumiwa hapo kwa maana ya muhuri. Kadhalika katika ukurasa huo huo wa 736 mstari wa 20 tuliandika kama kwanza maana ya neno khatam kama linavyotumika katika lugha, na kutoa ushahidi wa matumizi hayo ya lugha katika Bukhari, tukasema, "Neno khaatam pia lina maana ya pete. Imesimuliwa na sahaba mmoja ya kuwa Mtume s.a.w. alikataza kutumia vyombo vya fedha na khatam (pete) ya dhahabu na nguo za hariri." Kisha katika mstari wa 27 tukasema, "Ni dhahiri katika hadithi hizi mbili ya kuwa neno la khaatam limekuwa na maana ya pete. Mtume alitumia pete ya fedha na akawaruhusu Waislamu kutumia pete ya fedha kwa wanaume, na ya dhahabu pia kwa wanawake, na kila mara alitumia neno la khaatam kwa pete." Je, hapa pana maneno anayosema huyu Sh. Abdallah kuwa tumesema Mtume "kaitwa *Khaatamannabiyyin* kwa ajili ya hiyo pete ya muhuri wake anayoivaa"? Ni wazi Sh. Abdallah hakuisoma tafsiri yetu kwa nia safi. Bali aliisoma kwa haraka ya husuda ili kutafuta maneno ya kuwadanganyia watu akifikiri wataacha kuinunua wapate kuendelea kununua vitabu vyake vidogo vidogo. Lakini ni fedheha kwa mtu kama yeche kuanekana mlaghai na hasidi:

عَجِبْتُ لَهُ مَا يَتَّقِيَ اللَّهُ ذَرَرَةً أَشْقَوْتُهُ حَذَّ الْمَرَأَةِ أَمْرٌ مُقْدَرٌ
 فَخَزَرَ رَأْيَهُ الْبَيْنَاتِ وَتَارَةً بُعْرَفُ قَوْلَ الْمُصْطَفَى وَيَغْزِرُ

yaani:

Ninamstaajabia: hamwogopi Mungu hata kidogo!
Je, uovu wa mtu huyu ni jambo lililokadiriwa?
Mara anazikanusha dalili zilizo bayana,
Mara anaipotoa kauli ya Mtume na anaigeuza!

Kuna methali isemayo, “Akumulikaye mchana usiku atakuchoma”. Sh. Abdallah anatumulika mchana kweupe. Ni wazi ya kwamba ama hakuelewa maneno yetu au alitaka maksudi kuyapotoa ili adanganye watu. Naye ana elimu gani basi ya kushindana nasi? Naam, kwa uwongo na masingizio bila shaka anaweza kutushinda; lakini kwa elimu ya Kitabu cha Mungu na Mtume Wake ye ye hawezu kusimama mbele yetu ila muda kidogo tu.

Sh. Abdallah hanyoshi usemi

Kurejea tena maneno yake ya uk. 19 wa kijitabu chake, amesema, “Hakuna mfasiri ye yote tangu Kur'an ilipoanza kufasiriwa hizo zama za Mtume na masahaba mpaka hivi sasa (ila wao) aliyefasiri *Khaatamannabiyyin* kwa kuwa Muhuri wa Manabii.”

Maneno yake haya, kabla hatujayavunja sisi, ameyavunja mwenyewe na kuyapunguza sana nguvu aliposema uk. wa pili yake tu, “Hawataona katika kamusi lolote la lugha ya Kiarabu lililofasiriwa tamko la *Khatamannabiyyin* kwa muhuri wa Manabii tu, si Mtume wa Mwisho.”

Kauli yake hii anaposema halikufasiriwa kwa “Muhuri wa Manabii tu” inaonyesha ya kuwa “Muhuri wa Manabii” ni mojawapo katika tafsiri ya maneno hayo ingawa wameyafasiri pia kwa maana ya “mwisho”. Kwa tamko hili kabatilisha mwenyewe porojo la kusema ya kuwa hakuna ye yote aliyefasiri maneno hayo kwa kuwa “Muhuri wa Manabii”.

Tena kaandika hapo hapo ya kuwa wanazuoni hao wa kale “au wamelifasiri kwa kuwa yeye ndiye aliyewapamba Mitume kwa utukufu wake na kwa kuwa yeye Mtume wa mwisho au kwa kuwa yeye ndio muhuri aliofungia Mwenyezi Mungu Utume kuwa hapana tena.”

Haya maneno yake ebu yavalie miwani uyaangalie, mwungwana. Neno Ja “muhuri” linakubaliwa hapo kiujanja-ujanja likivungwavungwa pamoja na neno la mwisho. Kadhalika tafsiri ya “aliyewapamba Mitume” ambayo anaikubali hapa pamoja na kuivungavunga, sisi tumeieleza katika Tafsiri ya Kurani tukufu uk. 736 toka mstari wa 32 mpaka chini.

Jambo la ajabu ni hili, hapa Sh. Abdallah hakuleta nakala ya Kiarabu kama alivyofanya mahali pengi pengine. Sijui ameogopa nini? Mwungwana, yachungue wewe hayo.

Kisha yaangalie tena hayo maneno yake, anasema, “Yeye ndiye aliyewapamba Mitume kwa utukufu wake na kwa kuwa yeye Mtume wa mwisho.” Je, kuja mwisho mabwana kuna utukufu gani? Je, watu wa akheri zamani (zama hizi za mwisho) ni bora kuliko watu wa zamani kwa sababu wao ni watu wa mwisho? Maneno gani haya anayohangaika nayo Sh. Abdallah?

Muhuri una kazi gani?

Tena amesema, “Yeye ndio muhuri aliofungia Mwenyezi Mungu Utume kuwa hapana tena.” Toka lini, mabwana, kazi ya muhuri ikawa ni kufunga kitu? Je, muhuri umekuwa kamba au kufuli? Kazi ya muhuri ni kuhakikisha au kuthibitisha kitu kuwa kimetokana na mamlaka fulani, au kimetokana na chama fulani. Siyo kufunga asilan-muhuri si kazi yake kufunga. Basi huo muhuri utasemwaje Mungu kautumia kufunga utume? Liwali au Mtemi anapopiga muhuri wa ofisi yake juu ya barua inayokwenda kwa Bwana D.C. je, ni maana yake anaifunga barua ile? Au anaonyesha kuwa imetoka katika ofisi yake? Anapotaka kuifunga anaitia ndani ya bahasha. Lakini anapoipiga muhuri anahakikisha kuwa barua imetoka kweli katika ofisi yake maana hakuna mtu mwininge mwenye muhuri wa namna ile. Hivyo,

muhuri si kazi yake kufunga kitu bali kukithibitisha. Basi huo muhuri utasemwaje kuwa Mungu kautumia kufungia Utume; Maana Mtume mwenyewe ameitwa Muhuri wa Manabii. Yaani yeye ndiye Muhuri na Manabii wamepata chapa yake. Sasa kufunga utume kunatokea wapi katika maneno haya?

عَجِبْتُ لِغَنْمِ اللَّهِ كَيْفَ أَمْلَأَ
بِرْدَ النَّصْوَقَ كَانَهُ لَا يُبَصِّرُ
خَيَالَتِهِ كَالثَّاَمِبَنْ صَنْعِيفَةَ نَعْوَمَ فَيَغْفُضُ كُلُّ مَنْ هُوَ شَرِّ

Yaani:

Ninastaajabia kupiga muhuri kwa Mungu kunampotezaje!

Anayapinza maneno mazima kana kwamba haoni!

Mawazo yake hayana nguvu kama ya wanaolala

*Ni mtu mlalaji sana, basi humkasirikia kila anayemfanya
kukaa macho.*

Basi hivyo ndivyo Sh. Abdallah alivyobomoa maneno yake kabla sisi hatujayabomoa. Ee tuhoja twa kujifundisha tutafaa nini mbele ya haki?

Kama ambavyo maneno yake yamekwisha ashiria kuwa wako waliofasiri Khatamannabiyyin kwa maana ya Muhuri wa Manabii na ya mapambo na ubora. Kwa mfano, Mwenye tafsiri ya Fathul Bayan jalada ya 7 uk. 286 katoa tafsiri ya “muhuri” aliposema:

صَارَ كَانِغَاتِمْ لَهُمُ الَّذِي يَغْتَمُونَ بِهِ وَيَتَزَبَّؤُنَ بِكُونَهِ
مِنْهُ - (التَّفْسِيرُ الْفَتْحُ الْبَيَانُ جَلْدُ ٧ ص٢٦)

yaani, “Mtume s.a.w. akawa kama khatam kwa ajili yao ambayo kwayo wanapigia muhuri; hao (Mitume) wanapata mapambo kwa kuwa kwake (Mtume) mionganini mwao.” Ikumbukwe ya kuwa zamani mihuri mingi ilichongwa juu ya pete wanazovaa watu, wakiitumia kama pete pia na kama mihuri pia.

Ingawa maneno haya ya tafsiri ya Fathul Bayan yanayojibu hizo ndaro zake yako katika tafsiri ya Kurani Tukufu uk. 736 mstari wa 42, lakini kwa pupa yake ya kijicho hakuyaona, waila asingefedheheka kwa kudai ya kuwa hakuna mfasiri hata mmoja aliyetoa maana ya muhuri kwa neno Khatam.

Imam Razi Anasemaje

Ama tafsiri ya mbora pia tuliiandika kwa maneno ya Imam Fakhruddin Razi yaliyoko katika kitabu chake kiiwaacho At-Tafsirul Kabir jalada 2 uk. 31 chapa ya Misri yasemayo:

عِنْدَهُذِهِ الدَّرَجَةِ فَإِذَا وَلِيَ الْخَلْقَ الْأَرْبَعَةَ الْوَجْدَدِ وَالْعَيْنَاتِ
وَالْقُدَّرَةِ وَالْعَقْلِ فَالْعَقْلُ حَاتَمُ الْكُلِّ وَالْخَاتَمُ يَعِيبُ أَنْ
يَكُونَ أَفْضَلَ أَنَّهُ تَرَى أَنَّ رَسُولَنَا سَلَّمَ إِلَيْهِ وَسَلَّمَ لَمَّا
كَانَ حَاتَمُ النَّبِيِّنَ كَانَ أَفْضَلَ الْأَنْبِيَاءِ عَلَيْهِمُ السَّلَامُ
وَالْإِنْسَانُ لَمَّا كَانَ حَاتَمُ الْمَخْلُوقَاتِ الْجَسَمَانِيَّةِ كَانَ
أَفْضَلَهَا - كَذَلِكَ الْعَقْلُ لَمَّا كَانَ حَاتَمُ الْغَلِيمِ الْفَاعِيَّةِ
مِنْ حَضُورَةِ ذِي الْعِبَادِ لَكَانَ أَفْضَلَ الْغَلِيمِ وَالْمَدِّهَا -
(التَّقْسِيرُ الْكَبِيرُ جَلْدُ ٢ ص ٣)

Yaani, “Katika daraja hii wamepewa mambo manne: kuwapo, na uhai, na uwezo na akiIi. Na akili ni Khatamul kulli (bora ya vyote). Na khatam ni wajibu liwe na maana ya ubora. Je, huoni ya kwamba Mtume wetu s.a.w. alipokuwa khatamannaabiyyin amekuwa Mbora wa Manabii, amani na rehema za Mungu ziwe kwao. Na mtu alipokuwa khatamul makhlumat amekuwa mbora wa viumbe vyenye miili? Kadhalika akili ilipokuwa khaatamul khila'i imekuwa bora na yenye sifa kamiili kuliko sifa na heshima nyingine zinazotoka kwa Mwenyezi Mungu.”

Je, mwanadamu kuwa “khatam wa makhluku” atasemwa ni kiumbe wa mwisho? Maneno hayo ya Imam Razi tuliyatafsiri, nayo yako juu ya uk. 737 wa Tafsiri ya Kurani Tukufu toka mstari wa nne. Lakini Sh. Abdallah kwa hakika amejitia ndani ya ujinga dhahiri kuyakwepa maneno hayo yote na kuanza porojo ndefu-ndefu zisizomfaa kitu.

Akili safi inakubali ya kuwa lazima utume wa kumfuata Mtume wetu Muhammad s.a.w. uendelee, maana tutahakikishaje kama yeye ni Mbora wa Manabii kama hakuna nabii hata mmoja aliyoetokea katika wafuasi wake na kusema:

“Muhammad ndiye Bwana wangu, ndiye Mfalme wangu, nisingepata cheo cha Unabii ila kwa kumfuata yeye?” Kudai tu kuwa yeye ni Mfalme wa Manabii waliopita zamani hakuwezi kuwa na hoja yenye nguvu zaidi kuliko kama watokee manabii wenyewe vyeo vikubwa vikubwa kwa Mwenyezi Mungu waseme, “Muhammad ndiye Mfalme wetu na ndiye Mfalme wa Manabii wote waliopita zamani”. Seyidna Ahmad ni mmoja katika Manabii hao naye kwa hakika amehakikisha ya kwamba Mtume Muhammad ni Mtukufu ajabu hata kwa kumfuata barabara mtu anaweza kupewa na Mwenyezi Mungu hata cheo cha unabii.

Mtume Muhammad s.a.w. kwa hakika ni juu la uongofu, baada yake giza la upotevu limeingia. Nyota, yaani mawalii na maulamaa watukufu wanatoa nuru ndogo-ndogo kuongoza watu. Na mwezi, yaani Manabii wanaopokea nuru kubwa zaidi kuliko mawalii na maulamaa pia watatokea kuongoza watu na kuwafikisha katika neema zilizoletwa na Mtume Muhammad s.a.w. Seyidna Ahmad amelieleza jambo hili vizuri sana katika beti hizi tatu:

وَإِنْ رَسُولَ اللَّهِ شَهِيدٌ مُّبَيِّنٌ
وَبَعْدَ رَسُولِ اللَّهِ مَدْحُودٌ وَكُفَّابٌ
جَرَتْ عَادَتْ إِلَيْهِ الَّذِي هُوَ سَيِّءٌ
يُرِي وَجْهَ نُورٍ بَعْدَ نُورٍ يَدِهِ حَبٌ
كَذَّالِكَ فِي الدُّنْيَا قَرِئَ قَانُونَهُ
نَعْوَمَ السَّمَاءَ تَسْبِحُ وَإِذَا الشَّمْسُ مُنْقَرِبٌ

yaani:

*Na kwa hakika Muhammad Mtume wa Mungu ni jua
lenye anga;*

*Na baada ya Mtume wa Mungu ni mwezi na nyota;
Desturi hii ya Mwenyezi Mungu ambaye ni Mola wetu
inaendelea;*

*Akituonyesha uso wa nuru baada ya nuru kuondoka;
Kadhalika katika dunia waionna kanuni Yake;*

*Nyota za mbingu zinadhishirika wakati jua
linapokuchwa.*

Ni uwongo kwa njia gani?

Waidha sisi tulitaja maneno ya mwanachuoni wa hivi karibuni, Sheikh Muhammad Kassim Nanutwi aliyeanzisha madrasa maarufu ya Kisunni ya Deoband - India. Sheikh huyo wa Kisunni alisema katika kitabu chake kinachoitwa Tahdhirun-Nas maneno haya:

“Watu wasio na maarifa wanafahamu ya kuwa Mtume s.a.w. ni Khatam kwa maana ya kuwa amekuja mwisho wa Manabii wote kwa majira, na hivyo amekuwa mwisho wa Manabii wote. Lakini wenye maarifa wanajua ya kuwa kuja mbele au nyuma katika zama si jambo la heshima au ubora, na katika hali hii kutamka Khatamabiyyin kuwa sifa nzuri itakuwaje sawa?”

Sh. Abdallah ameshindwa kabisa kutoa dalili ya kubatilisha kauli hiyo ya Sh. Muhammad Kasim. Yeye anatupindukia sisi na kutulaumu akisema, “Na katika maneno yao ya uwongo kabisa ni haya yalisemwa katika mstari 40 wa sahifa 738 kuwa watu wasio na maarifa wanafahamu kuwa Mtume s.a.w. ni Khatam kwa maana ya kuwa amekuja mwisho wa Manabii” (uk. 28).

Sh. Abdallah hajaeleza maneno haya ni uwongo namna gani. Je, hayakusemwa na Sheikh Muhammad Kasim? Na kama yalisemwa na Sheikh Muhammad Kasim tutaambiwaje kuwa sisi ndio waongo kwa kuyataja? Je, amehakikisha ya kuwa maneno hayo hayakusemwa na Sheikh Muhammad Kasim? Bila shaka amekasirika kuona ameingizwa ndani ya kundi la watu wasio na maarifa. Na kwa hakika yu mmoja wa watu hao. Hajui lolote ila ulalamishi usio na faida.

Ndaro za kujitutumua

Sh. Abdallah amesema, “Sisi tuko tayari saa watakayo wakutane na sisi mbele ya khalaiki ya watu, watuonyeshe nafsi za ibara za maimamu hawa zinazosema kuwa Nabii Muhammad si Mtume wa mwisho.”

Tuko tayari kukutana naye ila tu aunyoshe vizuri wito huu, kwani maneno ya wito huu yamepotoka. Sisi Waahmadiyya tunakiri kuwa Mtume Muhammad ni wa mwisho wa mwisho kuleta dini na Sheria. Lakini Sheikh Abdallah upande mwininge anasadiki kuwa Mtume si wa mwisho kwa sababu anasema ya kuwa Nabii Isa atakuja baada ya Mtume wetu. Hivyo, hitilafu iliyoko baina yetu sisi na yeze ni hii ya kuwa, yeze anasema Nabii aliyezeka zamani ndiye atarudi duniani kuja waongoza Waislamu. Sisi twasema, si Nabii Isa wa zamani atakayekuja, bali ni mfuasi wa Mtume Muhammad s.a.w. atakayekuja kwa jina hilo na kwa cheo cha Nabii Isa. Hii ndiyo hitilafu baina yetu sisi na yeze. Asijisingizie bure kusema Mtume wetu ni wa mwisho hali anasadiki Nabii wa umati mwininge kurudi hapa duniani kuhubiri dini, Basi tuko tayari kushindana naye katika munadhara juu ya hitilafu hizi, yeze aje na dalili zake nasi tutaleta zetu. Naatuarifu tu ni lini anatutaka na mahali gani na kwa masharti gani ya kuendesha mashindano hayo.

Basi, imani yetu ya kuwa utume kama wa kufika kwa Nabii Isa unaendeleahaitegemei maneno yamaimamu ingawa wako wanaopatana nasi, bali imani yao na yetu inategemea maneno ya Kurani na Hadithi za Mtume. Wo wote wanaokwenda kinyume na Kurani na Sunna sisi hatutakubaliana nao, maana Mtume alituagiza akasema:

“Nimewaachieni mambo mawili, hamtapotea mkiyashika: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna ya Mtume wake.”

Hata baadhi ya maimamu wakaeleza ya kuwa kama maneno yao yaende kinyume na Kurani au Sunna ya Mtume, basi watu wasiyafuate. Ndiyo kusema ya kwamba walijua inawezekana sana nao wakosee kufahamu maneno ya Mungu na ya kwamba kila mtu ana haki ya kuyafikiria maneno ya Mungu na Mtume wake ili kupata mwongozo, na siyo kufuata tu maneno ya maimamu kama vipofu.

Zaidi ya hayo katika uk. 8 mstari 14 Sh. Abdallah amesema, “Lakini watadanganyisha viyi na vitabu viko? Tunavyo kama walivyo navyo.”

Baada ya kujigamba hivi mtu alimtazamia kujibu maneno kwa njia ilio sawa na kurejea vitabu vyote tulivyotaja. Lakini sisi tulitoa dalili katika vitabu mbalimbali ishirini na mbili au hivi. Vyote hivyo kavikwepa isipokuwa vitabu saba tu ambavyo pia hakuweza kubatilisha hata tamko moja katika yale tuliyosema. Sasa majivuno ya namna hii si ndaro za bure?

Anapotutaka tumwonyeshe vitabu hivi na ibara hizi, hali yeye amekwisha kiri jambo hili la unabii kuendelea aliponakili katika uk. 7 wa kijitabu chake maneno ya Ruhul Maani yasemayo “Ama ule ujumbe wa Mwenyezi Mungu anaoweza kuupata kila mtu unaendelea kwa watu wakubwa;” kisha twaona ya kwamba vitabu kumi na mbili tulivyotaja hakuvigusa na kubainisha tuliyosema ni sawa au si sawa; ila tu anajigamba ya kuwa yeye naye ana vitabu; kisha anaanza kuandika maneno ya ulalamishi hali hakusoma vitabu kumi na mbili tulivyovitaja; na vile alivyojaribu kuvijibu vinamshinda na kumfedhehi kama ambavyo nimekwisha bainisha; ndipo twaona ya kwamba si nia yake kutafuta haki, bali kujifaharisha bure na husuda mbaya ndivyo vinamtuma kupiga kelele za kijahili kama za mtu aliyeshtuka kutoka usingizini.

Sio ajabu anatutaka tumwonyeshe ni wapi pameandikwa kuwa Mtume si wa mwisho, hali sisi tunasema Mtume ni wa mwisho. Kama kusema Nabii wa kumfuata Mtume Muhammad anaweza kufika, yeye pia anakubali kuwa Nabii Isa atafika kumfuata Mtume, na ndivyo tunavyokubali sisi, ila tu twahitilafiana taawili. Sisi twasema, huyo Nabii Isa si wa zamani naye anasema ni wa zamani. Yeye anakubali ya kuwa unabii wa waliokufa zamani ndio unaweza kurudi hapa duniani kana kwamba Mungu ni maskini wa kufanya manabii wapya. Nasi twasadiki ya kuwa Manabii wapya wanaweza kufika na mlango huo uko wazi lakini yeye anaacha mzizi wa habari hii tunayoleze kila mara waziwazi, anazuka na mengine.

Bwana huyu angekuwa mwenye nia safi angeona maneno tuliyoadhika

katika utangulizi uk. xx yasemayo, "Mwishoni ninawaomba ndugu zangu watakapoisoma tafsiri hii kama wataona kosa lolote watuletee habari, wala wasikae kimya, maana sisi ni wanadamu tu na tumefanya tafsiri hii iwe nzuri kwa kila hali. Juu ya hayo mnajua sana ya kuwa asiye na kosa ni Mwenyezi Mungu. Tutakuwa na furaha kujaribu kusahihisha katika chapa ya pili kama kutakuwa na kosa la kweli. Na ama wale watakaopata kujua ya kuwa kazi hii ni yenye manufaa kweli kwa watu, basi watuombee heri kwa Mwenyezi Mungu katika dunia na Akhera. Mola wetu awe radhi nasi, nasi tuwe radhi naye. - Amin."

Baada ya nasaha hii, kama Sh. Abdallah hangekuwa na kijicho, angekusanya kila neno analofikiri kuwa kosa akatuletea. Kisha akaona tutamjibu nini. Lakini husuda imemtia hamaki akaanza kuzua kila namna ya kutusingizia bure na kutulaumu bilashi.

Mbona sisi tunajua kuwa tafsiri za vijitabu anavyotoa zina makosa mengi yanayotokana na ujuzi wake mdogo wa lugha ya Kiarabu? Hata wakati mwingine mimi na wenzangu hufanyia mzaha namna yake ya kutafsiri ovyo ovyo ikatufanya tuangue kicheko. Tungetaka tungeweza kumpangia makosa chungu chungu ya vijitabu vyake. Lakini tuliona ya kuwa ni kazi ya Mwislamu anayejitahidi; hakuyaandika kwa nia ya kuiadui dini. Hivyo tukamwacha, na tukaona ya kuwa vita yetu tuiielemezze kwenye Ukristo.

Sheikh Abdallah haoni ya kuwa tunautetemesha Ukristo wenyе silaha za kila aina na mali. Ukristo ambaо wakati fulani umeishambulia dini ya Kiislamu kwa kasi hata Waislamu wasiweze kuwa na hoja za kujiteea, kila mahali duniani. Lakini sisi tunautetemesha kwa sababu ya haki na ujuzi wa Kurani wa namna ya ajabu tulio nao. Basi Sh. Abdallah angekuwa hakudanganyika angefikiri kabla ya kutupamia. Lakini kupamia kwake ni kama chungu kupamia jiwe.

Watu wanajua ya kwamba Sh. Al-Amini bin Ali alikuwa mkhaliwu wetu na kadhalika Sh. Abdallah Abu Bakar Bakaathir na wengi wengineo wanaokaa nyuma nyuma. Lakini je tulitikisika? Bali kila siku idadi yetu inazidi na nguvu yetu inakua. Je, hamjawa na macho ya kuona kuwa huu ni msaada maalumu wa Mwenyezi Mungu ulio pamoja nasi? Juu ya hayo hatukuandika cho chote kuwalaumu masheikh hao

waliotukhalifu zamani.

Yote hii ni nia yetu safi ya kwamba kama Waislamu wataanza kugombana wao kwa wao, nguvu yao itapungua na maadui watafanikiwa. Hivyo, mtaona katika maelezo yetu tumeeleza itikadi za Uislamu tunavyozielewa kuwa sahihi bila kumlaumu Sheikh ye yote kwa jina au vitabu vyo vyote vya Waislamu kwa kuvitaja majina. Hatukuijingiza ndani ya magomvi ya madhehebu chungu chungu za Waislamu. Sisi tulieleza tu njia iliyo safi kwa maneno yaliyo safi, manyofu.

Ingawa Sh. Abdallah alituandikia zamani kidogo, kama nitakavyobainisha, ya kwamba sasa tuache utesi baina yetu tuelekee vita vya Wakristo, lakini ye ye mwenyewe ameanzisha tena utesi.

Yeye ilikuwa mahali pake kueleza tu itikadi yake juu ya utume anavyouelewa yeye na kutoa dalili zake kwa namna tulivyotoa sisi bila kuyalaumu madhehebu yo yote kwa jina. Kisha watu wangeona kama yeye ndiye mkweli au hapana. Kila mtu ana hiyari kufuata kunakomwelekeza akili yake.

MLANGO WA KUMI

UBISHI MWINGINE ULIOBAKI UNABATILISHWA

Katika mlango huu tutabatilisha ubishi mwngine uliobaki wa Sh. Abdallah, nanyi mtaona wenye kiasi cha elimu ya mtu huyu.

Mitume kupewa sifa mbaya na Mayahudi na Wakristo

Waidha Sheikh mkubwa wa Unguja ameandika katika uk. 28 wa kijitabu chake mstari wa 12 akasema, “Hawawachi Waahmadiyya! Mitume wote wamepewa sifa mbaya katika vitabu vy'a Mayahudi na Wakristo? Wanajua kuwa haya ni uwongo; lakini basi tu ngwenjera!”

Hiki ndicho kiwango cha elimu yake. Hakika umaskini wa mtu ni kukosa elimu ya kutosha. Lau angekuwa amesoma tafsiri yetu kwa utulivu, si kwa kusudi ili kutafuta maneno ya kufanya ubishi na ulalamishi, bila shaka angeona ndani yake elimu ya kumfaa inayohusu aibu wanazopakazwa Manabii wote na Wakristo na Mayahudi. Tunaposema Manabii wote, basi tuna maana ya Manabii wote ya kwamba wamepewa sifa mbaya.

Kama Sh. Abdallah angesoma maelezo yaliyoko ukurasa 231 wa Tafsiri yetu kifungu cha mwisho mpaka ukurasa wa 233; kisha akasoma maelezo ya aya 5 yaliyoko toka uk. 1036 mpaka 1040, bila shaka angeona jinsi Wakristo wanavyowapa sifa mbaya Manabii wote; na pia angeona jinsi tulivyojaribu kusahihisha lawama zao hizi.

Kwa kifupi ni nani asiyejua itikadi maarufu ya Wakristo isemayo kuwa Adamu alikosa akapata dhambi, na dhambi ile imerithiwa na kila mwanadamu toka watu vivi hivi mpaka Manabii wote isipokuwa Yesu na mama yake? Juu ya hayo wanaeleza kuwa Yesu alilaaniwa kwa kufa kifo cha msalabani (Wagalatia 3:13), na aibu nyingi nyingine wametia ambazo tumezibainisha katika maelezo yaliyoko uk. 231-232 wa Tafsiri yetu. Sasa ni Mtume Muhammad aliyebarinsha sifa njema ya Manabii wote kwa kuleta mafundisho yasemayo kuwa Manaabii wote ni maasum hawana dhambi. Ni wazi ya kuwa Wakristo hawambagui Nabii ye yote ila Isa tu katika hii itikadi yao ya dhambi

ya asili, ingawa naye Yesu wametia lawama za namna nyingine kama nilivyokwisha sema. Sh. Abdallah hana habari ya jambo hili. Na kwa sababu ya ujinga wake mwenyewe anatulaumu ya kuwa tunasema uwongo. Hakika lamtoshea jambo hili kuwa fedheha juu yake na kuondolea mbali ile heeshima ndogo aliyopewa na watu wapendao haki. Kama Sh. Abdallah anatafuta kuwapendeza watu na kuzidisha mlo wake, basi siyo njia hii anayoshika ya uwongo na udanganyifu na kuwafanya mzaha watu wa haki. Naam, Seyidna Ahmad alisema kweli alipoandika beti hizi:

عَجِبْتُ لِدَعْهَى لَمْ يُدَاوِي مُعْبُنَةً
وَمِنْ كُلِّ ذِي الْأَنْهَارِ لَمْ يُنْجِرْ
أَرَى الْعَصَرَ مِنْ نَزَمِ الْبَطَالَةِ نَائِبًا
وَكُلِّ جَهَنَّمِ فِي الْهَوَا يَتَغَرَّرُ
وَمَا هُمْ بِهُمْ إِلَّا عَظَّانٌ فَرِسَمُ
وَمَا حَمْدُهُمْ إِلَّا لَعْنَانٌ فَرِسَمُ

Yaani:

*Namstaajabia kipofu: hayatibu macho yake,
Lakini anampindikia na kumcheka kila mwenye macho.
Nayaona majira ya dhalala katika usingizi wa batili,
Na kila mjinga mkubwa anaringa katika matamanio yake.
Nao hawakusudii ila kustarehesha nafsi zao;
Nao hawajitahidi ila kwa kupata mlo unaoongezeka.*

Waongo thelathini

Sh. Abdallah amesema katika uk. 27 wa kijitabu chake ya kuwa Mtume s.a.w. alisema ya kuwa kutakuja waongo thelathini watakaodai utume.

Ni wazi ya kuwa hadithi hii inatuhadharisha na Manabii wa uwongo; lakini haisemi kuwa hatakuja Nabii mkweli. Mtu anapoambiwa yakuwa mji fulani utaingiwa na wanyang'anyi thelathini siyo maana yake kuwa katika mji huo hawatafika watu wanaotoa sadaka. Kadhalika Mtume aliposema kutakuja waongo thelathini watakaodai kuwa Manabii, asingekuwa na haja ya kuhadharisha hivyo kama kusingekuwa Nabii

ye yote wa haki atakayetokea. Maana kama kulikuwa hakuna kabisa utume, hilo tu lingetosha kumfanya kila Mwislamu asisadiki utume wa mtu ye yote, wala pasingekuwa na haja ya kuhadharishwa na waongo thelathini. Zaidi ya hayo ilibashiriwa kuwa Nabii Isa atafika, je tutasema ya kuwa naye atakuwa katika kundi la waongo thelathini?

Kadhalika ilipotajwa idadi ya thelathini ilionyeshwa ya kwamba ni idadi hiyo tu watakaokuwa waongo, na kutakuwa wakweli pia, na itakuwa juu ya Waislamu kufanya bidii kupambanua wakweli katika waongo.

Isitoshe idadi hiyo ya waongo thelathini waliodai utume baada ya Mtume s.a.w. ilitimia zamani kabla ya Seyidna Ahmad. Sh. Abdallah naaangalie kitabu kiitwacho Ikmaalul Ikmaal jalada 7 uk. 258 chapa ya Misri mmeandikwa juu ya waongo 30 maneno haya:

هَذَا الْعَدِيْثُ ظَهَرَ صَدِيقُهُ فَإِنَّهُ لَوْمَدَ مَنْ تَبَأَّ مِنْ ذَمَنِهِ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِلَى الْآنَ لِبَلَةٍ هَذَا الْعَدْدُ وَيَعْرِفُ ذَلِكَ
مَنْ يُطَاوِلُ التَّارِيْخَ . (إِكْمَالُ الْإِكْمَالِ جِلد٧ ص٢٥٣ مصري)
وَإِذَا قَوَى الَّذِينَ أَمْنَوْا قُلُوا أَمْتَأْنًا وَإِذَا أَخْلَقُوا إِنَّ شَيْئَنِهِمْ
قَاتُلُوا إِنَّا مَعْكُمْ إِنَّمَا نَعْنُ مُسْتَقْرِئُونَ (الْبَقْرَةُ ٥١)

Yaani, “Hadithi hii umedhihirika ukweli wake, maana lau wakihesabiwa waliodai utume toka wakati wa Mtume s.a.w. mpaka sasa itatimia idadi hii. Na jambo hili analijua anayesoma historia.”

Aliyeandika kitabu hiki alifariki mwaka 828 Hijriyya. Huu tulio nao ni mwaka 1373. Kutoa katika hii mwaka 828 tunabakiwa na miaka 545 ambayo imekwisha pita toka ilipoandikwa na mwandishi wa kitabu hicho kuwa waongo hao 30 walikwisha tokeea. Lakini Sh. Abdallah amejilalia foo! usingizi mzito, kisha anazindukana na kusema, tuliambiwa watafika waongo thelathini, hana habari kama walikwisha pita miaka mamia kabla Seyidna Ahmad hajazaliwa.

Majinni

Sh. Abdallah, kama ambavyo imekwisha onekana katika kila lawama aliyoleta, haelewi na maneno yaliyojaa elimu na hekima yaliyomo katika Tafsiri yetu. Anasema ya kwamba “tumekanusha kuweko viumbe wanaoitwa majinni”. Maneno yake haya si kweli. Ni husuda tu inayomfanya atapetape hivi na maneno ya uwongo.

Katika uk. 974 tumeandika katika maelezo ya aya 2 maneno haya, “Ingawa tunakiri ya kuwa vile Malaika ni viumbe pia kuna viumbe wanaoitwa majinni” Maneno haya yanaonyesha ya kuwa majinni wako kama vile malaika wako.

Kisha tukaonyesha katika uk. 273 kifungu cha (2) maneno haya, “Katika Kurani Ibilisi anaonyeshwa kwamba alikuwa ni mmoja katika Jinn (majinni), yaani viumbe wasioonekana (sura 18:51).” Maelezo haya yanaonyesha wazi wazi ya kuwa kuna majinni walioumbwa kwa moto, nao ni viumbe wasionekana na Ibilisi ni mmoja wa hao majinni. Tuseme Sh. Abdallah hakuona maelezo haya? Au anafikiri husuda yake inaweza kuondoa hadhi ya kuutumikia Uislamu tuliyopewa na Mungu? Au anafikiri uwongo wake utazuia kazi hii ya dini tufanyayo isiendelee mbele? Wallahi anadanganya:

Apewaye hapokeki,
 Mja huyo akipewa;
Wallahi haadhiriki,
 Japo taka adhiriwa;
Wa sitara hasumbuki,
 Viumbe mwajisumbua.

Shetani

Sh. Abdallah anasema ya kuwa sisi tunakanusha “hao viumbe wanaoitwa mashetani.” Maneno haya pia ni uwongo. Sh. Abdallah hapa pia hakuelewa maneno yetu ambayo ameyavamia tu katikati uk. 275, kisha asiyatoe kama tulivyooyaandika wenywewe. Habari hii ni maelezo ya aya 12 ya sura 7 yaliyoanza uk. 272. Katika uk. 273 kifungu cha (2) msitari wa 6 tumesema, “Hili laonyesha ya kwamba neno Shaitaan (shetani) limetumiwa katika Aya ifuatayo kwa namna ya mfano, bila

ya kukusudia yule Shetani anayewazengea watu kindanindani.” Je, maneno haya hayaonyeshi kuwa tunasadiki kwamba yuko Shetani asiyeonekana, anayezengea watu kindanindani? Funueni wenyewe kurasa hizo mwone.

Sehemu ya mwisho ya Aya 28 ya sura 7 inasema hivi, “Hakika yeye (shetani) anawaoneni pamoja na kabilia lake kwa mahali msipowaona.” Sh. Abdallah pia amekiri tafsiri hii katika uk. 31 wa kijitabu chake mstari wa 12. Sasa katika sura 7 aya 21 inasemwa ya kuwa “Shetani” alizungumza na Adamu na mkewe ana kwa ana. Hivyo Shetani huyu aliyeonekana ni mbali na yule anayesemwa na Mwenyezi Muungu haonwi na watu. Hivyo tunasema ya kuwa huyo anayeonekana alikuwa ni mtu mwovu kama ambavyo watu waovu wanaitwa mashetani katika karibuni kila lugha. Hata Kurani yenyeche imetumia neno “Shetani” kwa ajili ya watu wabaya mahali pengine vile vile, kwa mfano katika sura 2:15:

وَلَدُ الْقَوْمِ الَّذِينَ أَمْرَأْتَنَا بِعَيْنَيْهِمْ
كُلُّ أَبْرَاجٍ مُّهْبَطٍ مُّهْبَطٍ

yaani, wanafiki “wanapokutana na walioamini, husema: Tumeamini; na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao, husema: Hakika sisi tu pamoja nanyi; sisi tunafanya dhihaka tu.” Sasa ni nani isipokuwa mjinga wa ujingani atakayesema kuwa hapa neno “shetani” si muradi wake watu wabaya: wakubwa wa uovu? Je, kusema hivyo kuwa hao ni watu waovu ambao wameitwa mashetani, kutamfanya mtu na akili zake kusema ya kuwa aliyesema hivyo haamini mashetani? Je, hatukuandika katika ukurasa wa pili tu kifungu cha mwisho ya kuwa Waislamu tumelazimishwa na Kurani (sura 16: 99) tusome, Audhu billahi minash-shaitani-rajiim, yaani, “Najikinga kwa Mwenyezi Mungu anilinde na shetani anayepigwa mawe?” Sasa Sh. Abdallah anatafuta nini kwa uwongo huu anaotukusanya toka mashariki mpaka maghaaribi ya kijitabu chake?

Adamu

Tena Sh. Abdallah ameleta mashtaka mengine juu ya Nabii Adamu. Ubishi wote alioleta umekwisha jibiwa ndani ya maelezo ya tafsiri na kadhalika uwongo wake pia umekwisha jibiwa. Msomaji naasome mwenyewe habari yote toka ukurasa 30 wa Tafsiri yetu.

Nabii Isa Hakufa Juu ya Msalaba

Tena Sh. Abdallah ameleta maneno mengine ya kuwa tunasema Nabii Isa kasulubiwa. Sisi hatukusema hivyo. Neno kusulibiwa ni la Kiarabu, na maana yake ni “kufisha msalabani” kama linavyoelezwa na Aqrabul Mawaarid (kitabu cha kamusi). Nasi tumefasiri, “Hawakumfisha msalabani.” Habari zaidi watu wafunue kurasa hizo waone wenyewe wasitegemee kusikia. Mtume s.a.w. alisema:

لَيْسَ الْغَيْرُ كَالْمُعَائِنَةُ

“Kusikia si kama kuona.” Sh. Abdallah anasema ya kuwa ni mtu mwininge aliyeuawa msalabani. Sisi tunasema Nabii Isa hakuuawa msalabani wala hakuna mtu mwininge ye yote aliyeuawa badala yake. Aya aliyoandika anaikosea ovyo kuifasiri. Nyote mnakumbuka ya kuwa tumekwisha onyesha katika mlango wa nane ya kuwa Sh. Abdallah anasadiki kuwa Nabii Isa alikufa na akazikwa. Angeeleza kwanza hili neno kubwa badala ya kutuletea lawama za unafiki.

Miujiza ya Nabii Isa

Anasema ya kuwa sisi tunaikataa miujiza ya Nabii Isa.

Lo! uwongo ulioje huu? Tuna uadui gani na Nabii Isa hata tukatae miujiza yake? Mbona miujiza ya Manabii wengine hatuikatai, ya Nabii Isa tutaiatalia nini? Na ni wapi tulipoandika kuwa Nabii Isa hakufanya miujiza? Wasomaji wetu hawatafaidi habari hii ila wajisomee wenyewe tafsiri tulivoandika, maana maneno ya Sh. Abdallah si ya kusadiki. Kijicho kimemsambakiza uwongo usiokadirika.

Mti aliokatazwa Adam ni upi?

Kama ilivyo desturi yetu hatupendi kuwaficha watu ilmu; na hafichi ilmu na kuogopa kuisema ila mtu mwenye ujuzi kidogo wenyewe shakashaka, usio na hakika. Kila ukimwuliza neno, anakwambia fulani alisema hivi, fulani alisema hivi; naye hatoi fikira zake mwenyewe kwa kuwa hajui, amefanana na santuri (gramafoni). Watu wa namna hii hubabaika sana wanapoona mtu amewazidi ilmu anayeeleza kila neno waziwazi na kufunua ilmu za undani walizokuwa hawazijui. Wanafikiri ya kuwa wananyang'anywa ukubwa, na wanafunzi watawahama wafuate kwenye elimu nydingi. Basi hofu yao hii bila shaka itatimia. Wanafunzi watawahama na watafuata kwenye elimu nydingi. Kurani imekwisha toka sasa watawadanganya wapi? Wanafikiri hawawajui? Wanawajua; na wote wenyewe pesa zao wanunuwa Tafsiri na kuisoma.

Ama habari ya mti aliokatazwa Nabii Adam na mkewe, kuwa ni mti wa aina gani, tumeeleza maneno ya namna mbalimbali yanayoweza kuwa tabiri ya habari hiyo. Sh. Abdallah hakusoma vizuri habari hii katika Tafsiri yetu, nasi twamwomba arejee kusoma kurasa na mistari aliyoiruka katika maelezo ya sura 2 aya 36 na sura 7: 12-26, kisha, akitaka, alete upinzani kwa dalili kamili, nasi tutamtazama.

Ama maana ya neno *auraaq* (majani), kuwa “vijana” ni maana wanayotoa Waarabu wenyewe kama tulivyokwisha onyesha hapo hapo kuwa maana hii inaelezwa katika Aqrabil mawaarid, Lisanul Arab na Lane's Arabic-English Lexicon, nayo ndiyo maana iliyoyamkini katika maelezo hayo. Tunamwomba kila msomaji ajipatie tafsiri yetu ye ye mwenyewe aangalie habari zote kama tulivyozandika. Ama kuamini jambo lolote au kutoliamini ni kхиari ya mtu, lakini ilmu lazima ibainishwe ili kuwasaidia watu wanaotaka kupanua mawazo yao, nasi tumebainisha ilmu nydingi za ajabu katika maelezo hayo na hata hivyo hatukufika mwisho hata wa elimu yetu, wacha mbali mwisho wa elimu ya maneno ya Kurani yenye ambao haufikiki; kwani ni Kitabu cha Mungu, na elimu zilizomo ndani yake ni za Kiungu, zisizo na kikomo, na hakuna atakayejidai kuwa ye ye ndiye amejua mwisho wa maana zote au mradi wa maneno yote ya Mungu ila mtu mwongo tu. Basi Sh. Abdallah, kama anayo elimu yo yote, na aionyeshe, ili iwafae watu sio kukalia ubishi wa husuda na kijicho. Naye atoe tafsiri yake na maelezo

yake ayajuayo, kisha watu watazidi maarifa na watapima wenyewe kuona ni nani atoaye yanayotosheleza haja za sasa.

Kuomba dua katika sala

Katika maelezo ya sura 13:23 kuna maneno ya Mujaddid wa zama zetu hizi, Seyidna Ahmad (amani ya Mungu juu yake) yasemayo: “Lakini ninyi mnaposali si vibaya kuomba dua zenu kwa unyenyekevu katika lugha zenu, isipokuwa Kurani ambayo ni maneno ya Mungu na dua zilizobainishwa katika Hadithi ambazo ni maneno ya Mtume s.a.w. Ili athari ya kuomba na unyenyekevu iwe katika miyo yenu.”

Mtu ye yote hata mwenye ujuzi kidogo anajua ya kwamba maombi yote ya lazima kwa ibada yako katika sala kwa maneno ya Kurani au kwa maneno aliyofundisha Mtume s.a.w. Na kama mtu asome hayo hayo tu sala yake itatimia. Nasi tumeambiwa ya kuwa maombi hayo yasemwe kwa Kiarabu chenyewe.

Baada ya maombi hayo, kuna haja anazoweza kuwa nazo mtu za namna mbalimbali, na maadamu amekwisha hudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu wakati wa sala, anapenda aweke maombi yake kwa adabu na unyenyekevu mbele ya Mwenyezi Mungu kwa wakati huu ulio bora kabisa. Sasa hapa ni lazima aruhusiwe kutumia lugha yake kwa kusema maombi yake hayo yasiyokuwa na Kurani na Hadithi. Pengine anaomba kupata mtoto, au anaomba biashara yake ifanikiwe, au anaomba kazi zake za mashamba zimwendee sawa, au anaomba fitina ya adui zake ofisini isimdhuru, au anaomba ugonjwa wa mkewe au wa mumewe upone. Je, asiombe yote hayo mpaka akajifundishe Kiarabu cha kuyaombea? Au Mwenyezi Mungu hasikii lugha za Waafrika ila za Waarabu peke yao? Ingefaa Sheikh Abdallah, Sheikh mkubwa wa Unguja, akatufunulia jambo hili sawasawa. Anasema, “Na walikubalisha kuwa inajuzu kumwomba Mwenyezi Mungu ndani ya Sala kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu ila Kurani na Hadithi Si wanataka kuwaharibia watu sala zao hawa Makadiyani!” Ama ni maneno ya kuchekesha. Ila maskini hajatuambia bado sala hiyo huharibikaje mtu anapoomba dua kwa lugha yake; je, lugha zetu Waafrika zimekuwa najisi, au lugha za makabila mengine, Mungu hataki kusikia hizo ila lugha ya Waarabu? Fafanua maneno Sh.

Abdallah, usiumeume. Tunakungoja kukusikiliza.

Tafsiri yetu imesafisha taka taka nyangi

Hakika tafsiri yetu imesafisha takataka nyangi zilizoandikwa hata na Waislamu wenyewe kumsingizia maovu hata Mtume wetu na pia baadhi ya Mitume wengine wa zamani. Ilikuwa mahali pa Sh. Abdallah kwanza kuwahadharisha watu na tafsiri hizo za Kiarabu kama Jalaleni na nyinginezo zenye maneno mabaya sana juu ya Mtume wetu. Nitaeleza mifano michache; na kwa ajili ya kuhofia nafasi nitatoa tafsiri tu ya maneno ya Kiarabu au muradi wa maneno yao, nanyi yachukueni maneno haya mwazungukie kina Sh. Abdallah mwaambie wafunue Jalaleni kutazama hatari ya maneno haya wanayoyafuata.

Jalaleni kinapoeleza kisa cha Mtume na Zainab bint Jahash aliyekuwa mke wa Zaid bin Harith ambaye alikuwa akiitwa Zaid bin Muhammad kwa kuwa Mtume s.a.w. alimpanga utoto, kinasema, “Mtume s.a.w. akamposa Zainab kwa Zaid. Kisha baada ya muda, Mtume akamwona Zainab na mahaba yakaingia katika nafsi ya Mtume, na katika nafsi ya Zaid ikaingia chuki kumchukia Zainab. Kisha Zaid akamwambia Nabii s.a.w., Nataka kumwacha. (Nabii) akamwambia, Shikamana na mkeo (Na ukaficha katika nafsi yako ambayo Mungu alitaka kuyatoa) (yaani Mtume alificha) kudhihirisha mahaba aliyokuwa nayo kwa mwanamke yule, na ya kwamba, lau Zaid akimwacha yeye. (Na ukawaogopa watu) yaani wasiseme amemwoa mke wa mwanae. (Na Mwenyezi Mungu ana haki zaidi ya kwamba umwogope Yeye) katika kila jambo, nawe mwote (Zainab) wala usiogope maneno ya watu. Kisha Zaid akampa talaka, na eda ya yule mwanamke ikaisha; basi Mwenyezi Mungu akasema, (Basi alipokwisha Zaid haja yake na mwanamke yule, Tulikuozaye) Nabii s.a.w. akaingia kwa mwanamke kule bila idhini, na Waislamu wakashiba mikate na nyama.”

Maneno haya yote tumeyanakili toka Tafsiri ya Jalaleni. Waambieni wafunue Jalaleni sura Ahzab waone maneno hayo. Je, inawezekana Mtume wa Mungu amtamani mke wa mtu kwamba amwote yeye, na atamani ya kuwa lau mumewe amwache nimwote mimi, na alipoachwa, mara baada ya eda akaingia kwa mwanamke yule bila idhini ya wazazi wake, na akawashibisha Waislamu mikate na nyama! !

Maneno haya ya uwongo anayosingiziwa Mtume wetu na Waislamu wenyewe yanawafanya Wakristo waidharau sana dini yetu ya Kiislamu, na kusema, Muhammad (Mungu apishe mbali) alikuwa si Mtume, bali mtu mbaya mwenye tamaa. Maneno haya yote yamekaririwa sana katika vitabu vya Wakristo. Nawe fikiri kama Mkristo aje kukuta hata Waislamu wenyewe wanasadiki kuwa Mtume wao alikuwa mtu wa namna hiyo, je watamwamini? Kama si ujinga wa hawa Waislamu kazi yetu ya kuwasilimisha Wakristo ingekuwa nusu tu kuliko ilivyo sasa. Hii ndiyo sababu watu kama Sh. Abdallah wanaosadiki vitabu vyenye maneno mabaya kama haya wanashindwa kuwajibu Wakristo. Kisha wanatugeukia sisi Waislamu wenzao tunaojua vizuri ni taabu gani zinazoukabili Uislamu kwa kuwa tunashughulika kuuhubiri kila mahali duniani. Wanatupinza na kutulaumu tunapotoa vitabu vya kubatilisha kufuru chungu chungu za namna hii. Kisha wanasema kama alivyosema Sh. Abdallah katika uk. 29 wa kijitabu chake mstari wa 3, “Lazima wahadharishwe Waislamu ubaya wa tafsiri hiyo (ya Waahmadiyya) au itawatoa Uislamuni - wawe murtadi - wakiamini baadhi ya yaliyomo katika maelezo ya tafsiri hiyo”. Je, watu kama yeze wanaoamini baadhi ya maelezo ya Jalaleni hawawi nje ya Uislamu na kuwa wenye kurtadi?

Je, watu kama yeze wanaoamini baadhi ya haya ya Jalaleni alipata kuwatangazia Waislamu kuwa wajihadhari nayo?

Maneno ya namna hiyo ya Jalaleni yameelezwa na baadhi ya wafasiri wengine wa Kiarabu. Nayo yanapunguza heshima ya Mtume wetu na hali mambo sivyo yalivyo katika Kurani wala sivyo yalivyokuwa hivyo wanavyooleza wao. Funueni tu tafsiri yetu mjionee wenyewe namna tunavyoulinda Uislamu na tunavyoangalia heshima ya Mfalme wa Manabii - Muhammad s.a.w.

Kadhalika tafsiri hizi za wafasiri zimeleta aibu nyingi juu ya Manabii, na sababu yake ni kuwa badala ya wao kutegemeza tafsiri zao juu ya maneno ya Kurani yenyewe, wao wakategemeza juu ya visa vya uwongo walivyosikia huko na huko kwa Mayahudi na Wakristo. Hivyo wakasema Nabii Yusuf alikusudia kumwingilia mke wa Waziri, lakini baba yake Yakubu akamithilishwa kwake, akampiga kifuani, naye Nabii Yusuf akatolea shahawa yake vidoleni (Jalaleni). Je,

inawezekana Nabii wa Mungu anuie mambo mabaya kama hayo?

Wamesema Nabii Dawud alikuwa na wake tisini na tisa, naye akamtamani mke wa mtu, na mtu yule hakuwa na mke mwengine ila huyo, Nabii Dawud akamwoa yule mwanamke na akamwingilia; kisha Mungu akampelekea malaika wawili kumsuta dhambi hii (Jalaleni). Je inawezekana Nabii wa Mungu kufanya jambo hili linalofanya watu mashetani?

Mambo haya ya aibu juu ya Manabii yaliyomo katika vitabu anavyokubali Sh. Abdallah hayamtoi katika Uislamu na kumfanya murtadi? Walioyaandika mambo hayo Sh. Abdallah atawasemaje, hawakuwa Waislamu? Sh. Abdallah aeleze ni aibu gani katika Tafsiri yetu juu ya nabii ye yote wa Mwenyezi Mungu? Je, Sh. Abdallah alipata kuwahadharisha Waislamu na baadhi ya maelezo ya vitabu hivyo vyaa kinahita kwa yatawatoa katika Uislamu?

Husuda imempindua sasa

Hivyo maneno ya Sh. Abdallah juu yetu hakuyaandika ila kwa kuonea kijicho tafsiri yetu, kwani yeye toka zamani anajua kuwa anahitilafiana nasi baadhi ya mambo. Kabla hajijatoka tafsiri hii ya Kiswahili Sheikh Abdallah alinunua kwetu tafsiri yetu ya Kiingereza yenyе sura tisa alipofika Tabora. Baada ya muda akatuandikia kutuuliza kama sehemu ya pili ya Tafsiri ile ya Kiingereza imekwisha toka. Maelezo yaliyomo tulioandika katika tafsiri hiyo ya Kiingereza hayakupinzana na yaliyomo katika hii ya Kiswahili. Baada ya muda kadha sisi tulimjibu Padre Kaholwe wa Tabora alipoandika maneno ya kuupinga Uislamu. Na Sheikh Abdallah tulimpelekea nakala ya kigazeti “Haki ndiyo inayoshinda” kilichoandikwa na Sheikh Jalalud-Din Qamar H.A. kumjibu Padre Kaholwe. Majibu yaliyotoka kwa Sh. Abdallah ni haya:

“Bwana mtukufu Jalalud-Din Qamar; Assalamu alaikum warahmatullahi wa barakatuh. Nakuhani kwa makala “Haki Ndiyo inayoshinda”, Mungu atakujazi kheri na amjazi kheri kila anayepigania haki.

“Ingawa mimi siwafikiani na baadhi chache ya mambo wanayoyasema Waahmadiyya lakini nakiri mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya waja wake kuwa napendezwa sana na GHAIRA yao juu ya Uislamu. Hawakubali kumwona anayeuponda (japokuwa haupondeki) wakamnyamazia - khasa hawa Wakristo wa Afrika ambao wamefanya ndiyo ibada yao kubwa kuutukana Uislamu pasina haki yoyote. Washikeni koo, msiwape pumzi. Wallahi! Mtawashinda kwani wanatumia batili.

وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ ذَهْوًا

(Haki imefika na uwongo umetoweka. Hakika uwongo ni wenye kutoweka) na Mungu yuko pamoja na nyinyi.

لَا يَأْتِيهَا الظُّنُمَّ إِمْمُوْلَانْ تَسْفَرُوا إِلَيْهِ اللَّهُ يَعْلَمُ كُمْ دَشِّيْشَتْ أَقْدَهُ أَدْكَنْ

(Enyi mliaoamini! Mkimsaidia Mwenyezi Mungu Atawasaidieni na Ataimarisha miguu yenu).

“Napenda unisalimie bwana mkubwa Mubarak na bwana Saadani Abdu Kandoro na wengineo.

“Inshallah mtakuwa mkono mmoja na jamaa wa Kisunni wa Tabora na wengineo katika hili jambo la kuzuilia fitina ya Wakristo. Na Kenya huko wanazidi kutoa magazeti kama hayo ya kupoteza watu kusudi. Na tuwe mkono mmoja katika jambo hili au itakuwa hatari kubwa mbele yetu.

“Naomba tutenge mbali kwanza khitilafu yenu na yetu tushughulikie sote pamoja hivi vita vya Wakristo.

Abdallah Saleh.”

Barua hii ya Sh. Abdallah inaonyesha waziwazi kuwa anajua vizuri toka zamani kuwa kuna mambo machache ambayo ye ye anahitilafiana

nasi, maana alikuwa kisha pata tafsiri yetu ya Kiingereza. Juu ya hayo haonyeshi hapa kuwa hitilafu hizo zinamfanya aliye nazo kuwa murtadi na kumtoa katika Uislamu kama anavyoeleza sasa katika kijitabu chake. Bali, anatuita kuwa waaminio tunaohusika na Aya ya Kurani aliyoitaja, anatuambia “Mungu yuko pamoja nanyi”. Anaasema, anapendezwa sana na ghera yetu juu ya Uislamu; anasema, sisi Waahmadiyya hatukubali kumwona mtu anajaribu kuuponda Uislamu; na zaidi ya haya anaomba tuwe mkono mmoja tusiingiliane katika hizi hitilafu zetu na zao tuzitenge kwanza mbali.

Haya ni mawazo safi ya Mwislamu mwema. Lakini ole maskini husuda imempindua sasa, akaanza kutuita “Makadiani” badala ya kutuita Waahmadiyya kama alivyotuita mbele, akisahau ya kuwa Mwenyezi Mungu amesema:

وَلَا تَنْبِهُ رَبِّكَ بِالْأَنْقَابِ

watu wasiitane kwa majina ya namna hii; na pia akaanza kutuzushia uzushi wa namna nydingi. Je, vita vya Wakristo alivyosema kwanza tushughulike navyo tuache hizi hitilafu zetu na zao vimekwisha? Mbona bado vinaendelea. Hizi hitilafu zetu sisi na yeye zimeanzia katika Tafsiri hii au ni za toka zamani? Basi kama si husuda na kijicho ni nini tena kilichomtuma kutupinza kinyume na ahadi zake, kisha na upinzani wenyewe usiwe na hoja za maana, bali uliojazwa uwongo na masingizio na maneno ya kijahili. Aibu yote hii inamshukia Sh. Abdallah kwa ajili ya husuda. Mtume Muhammad s.a.w. hakusema bure alipotuambia tujiepushe na husuda akisema:

إِيَّاكُمْ وَالْعَسَدُ فِإِنَّ الْحَسَدَ يَعْكُلُ الْخَسَنَاتِ كَمَا
تَعْكُلُ النَّارَ الْحَطَبَ -

‘Jiepusheni na husuda, maana husuda inakula mema (ya mtu) kama moto unavyokula kuni.’

MLANGO WA KUMI NA MOJA

WAISLAMU WENYE ROHO SAFI WAMEIPOKEA TAFSIRI YETU KWA SHANGWE

Kwa hiyo, husuda ya Sh. Abdallah inamdhuru mwenyewe, maana Waislamu wenye roho safi wako macho, nao wameipokea tafsiri yetu kwa shangwe na kwa shukrani, hata hatuna nafasi ya kupiga shukrani zao nyingi chapa katika gazeti letu zitujiaavyo kwa wingi. Wako walioituandikia ya kuwa maelezo ya tafsiri yetu ni mwujiza, na maneno hayo tumekwisha yatangaza katika gazeti. Wako walioituambia kuwa hoja zinazotolewa kwa ajili ya kuurudi Ukristo hazipinziki, na maneno yao tumekwisha yatangaza katika gazeti letu. Sheikh Ghazali wa Mombasa akatangaza kuwa tafsiri hii ni nzuri haina kosa lo lote, na maneno yake tumekwisha yatangaza katika gazeti. Wako walioituandikia kuwa wangekufa bila kuona Tafsiri nzuri ya namna hii, na maneno yao tumeyatangaza katika gazeti hilo hilo la Mapenzi ya Mungu. Wako walioituandikia ya kuwa wamezitoa hoja zetu mbele ya Wakristo watukutu zikawatahayarisha na kuwafurahisha Waislamu. Wako waliokwisha linganisha tafsiri yetu na tafsiri ndogo ndogo za Sh. Abdallah na za watu wa Mombasa, nao wamekwisha hakikisha ya kuwa tafsiri yetu ni safi sana. Wakristo wanatetemeka ovyo kwa tafsiri hii kana kwamba Malaika wa mauti anawapigia hodi milangoni. Ah! Sheikh Abdallah, huachi? Huoni haya? Basi kijicho huendeshwa hivyo? Baabaa, hii ni kazi ya Mungu, jihadhari na maneno yako, utakuja lia!

Kukamilisha maneno haya nitaandika habari za waungwana wachache Waislamu wenye roho safi zisizofunikwa na kijicho kama Sh. Abdallah na jamaa yake Ali Muhsin.

(1) Sheikh Alghazali wa Mombasa

Tafsiri ya Msahafu ilipofika Mombasa mtu mmoja aliipeleka darasani pa Sheikh Muhammad Abdullah Al-Ghazali. Watu wengi walihudhuria na wote walifurahi mno kwa kuona tafsiri ya Kurani katika Kiswahili. Baadaye Sheikh Ghazali alitangaza siku ya Ijumaa juu ya mimbari ya kuwa tafsiri hii ni safi sana wala haina kosa lo lote. Na sheikh

huyo wa Mombasa alipofika Nairobi aliulizwa tena juu ya tafsiri hii. Aliwaambia watu wa Nairobi ya kuwa ameisoma tafsiri hiyo nayo ni sahihi kabisa. Naye kwa kuishangilia kazi hii kubwa ametutakia heri na baraka.

(2) **Bwana Ibuni Saleh wa Zanzibar.**

Baada ya kutuandikia kuwa Khatamannabiyin imeleta ubishi akasema kwa Kiingereza fasihi maneno ambayo tunayafasiri hapa:

“Juu ya hayo nimeitalii barabara hii Kurani Tukufu uliyoniletea, nami nalazimika kukubali ya kwamba sioni tofauti yo yote katika matini kuhitilafiana na tafsiri nyingine za Kiingereza nilizosoma, yaani ya Maulana Muhammed Ali, Abdullah Yusuf Ali na Marmaduke Pickthall. Lakini jambo lililoniathiri na kunivuta niisifu kwa moyo wangu wote ni maandiko ya maelezo yanayohusu hoja kadha wa kadha - kwa hakika hoja zinazokubalika - za kuvunja upotovu wa namna nyingi uliomo katika maandiko kadha wa kadha ya Biblia - Agano la kale na jipya, na uliomo katika tafsiri ya Kurani Tukufu ya Sale (ya Kiingereza) na ya Dale (ya Kiswahili). Kwa kazi hii bila shaka mnastahiki kusifiwa na kushukuriwa na Waislamu wote, kwa kuwa hakuna Mwislamu katika Afrika Mashariki amepata kukusanya hoja za namna hii kabla ... Lazima niseme kwa kweli bila kusita ya kuwa nimeathiriwa sana na Kiswahili kisicho na kosa ulichotumia ambacho hata marehemu Sheikh wetu mtaalamu Al Amin bin Ali hakujali au hakujishughulisha kukitumia katika tafsiri yake ya Kiswahili ya Juzu Al Bakara “

(3) **Bwana A. Abdullah wa Mombo**

Ameandika: “Ahsante sana kwa kazi yako tukufu. Mungu akujalie umri mrefu sana. Bwana, tumepata kitabu hiki kitakatifu. Ni haki yangu leo kukujulisha na kukupeni pole kwa kazi kubwa kama hii. Oo, Mungu awazidishie maarifa, awape riziki halali, awaondolee maradhi, husuda, bughudha, mwendelee kwa mambo ya dini kama hivi” (Mwandishi huyu mwenye busara alitabiri mbele kuwa kutakuwa husuda na bughudha kwa ajili ya kazi hii tukufu. Basi si ajabu kumwona Sh. Abdallah amekazana na maneno ya uwongo kuilaumu kwa sababu ya kwamba ingawa yeeye anadhaniwa ni sheikh mkubwa lakini hajaweza

kutoa tafsiri ya namna hii. Kadhalika inachekesha kumwona rafiki yake All Muhsin akisema ya kuwa tafsiri hii nzuri inayosifiwa sana na watu na kushukuriwa kuwa haifai hata pesa mbili. Basi kama si husuda ni nini kingemsemesha maneno haya ambayo yanaonekana waziwazi kuwa ya kijicho).

(4) Bwana Omari Arubeti wa Iringa

Ameandika: "Sina budi kutoa shukrani nyingi mno pasipo kiasi. Tena nimeshukuru sana mapenzi yako na wema wako. Natoa ahsante sana juu ya kupata Msahafu wangu, yaani Kurani Karim. Tena natoa pongezi kwa kazi kubwa kama hiyo mliyoifanya."

(5) Bwana D. A. Lawson.

Mwingereza wa Nairobi ambaye ni Mwislamu toka miaka kumi na tano ambaye ana ujuzi mwingu, tafsiri yetu imemwathiri sana hata ameingia katika Jumuiya ya Ahmadiyya sasa ili naye aweze kuwa na sehemu katika hii jihadi ya kuutetea Uislamu. Yeye alituandikia akasema, "Nitapenda kuruhusiwa kuwapeni pongezi juu ya kuweka kazi nzuri sana mbele ya watu wa Afrika Mashariki. Tafadhali sana pokea cheque ya Shs. 100/- ambayo ni zawadi ndogo utakayopenda kuitumia katika kuwagawia bure watu nakala chache za tafsiri hiyo."

(6) Mwalimu M. T. Ramadhani Hayeshi wa Ujiji.

Akaandika: "Mimi ni mtu wa pili Ujiji kupata Msahafu huu. Ama sina la kusema. Nimeshangaa. Leo najiona hali yangu njema. Maisha yangu nisingeona tafsiri kama hii. Sasa nakupa sifa ya Msahafu huu: Nilipoupara tu, nikaupambanisha na tafsiri ndogo za baadhi ya sura nilizopata Mombasa na Unguja. Naam, hapana shaka tafsiri safi kabisa kabisa. Tena aya zimefasiriwa ndani kwa mukhtasari wa matini, lakini nje zake zimekunjuliwa kwa hekima kubwa sana, na ithbatil nyingi kabisa. Sijaona mahali palipofundishwa mirathi kama katika Msahafu huu."

(7) Mwalimu Songoro Marjaney Lwano wa Kasulu.

Ametuandikia kutoka Kasulu akasema, “Namshukuru Mungu kwa kuwafanya ndugu zangu Waahmadiyya kuvumbua roho ya maombi yangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kufasiri Kurani kwa Kiswahili ambamo ndani mmepambwa hoja kali kali zisizojibika za kumrudi padre Dale na wensiwe wenye uadui juu ya dini ya Islam. Msahafu huu ni silaha kubwa ya kila Mwislamu po pote alipo. Leo nimecheka kidogo. Alhamdu lillahi rabbil'aalamiin.”

(8) Bwana Mohamedi Kalufya wa Uvinza.

Ametuandikia, akasema, “Hasa mimi nakuhakikishia kweli kuwa wewe ni Mtume hasa uliyetumwa na Mungu, yaani kuja kutuinua sisi Waafrika, kutufufua katika kifo kikubwa. Na kuja kutuondolea giza lililo kubwa. Na kutuletea taa isiyozimika.

Nami toka leo ni pamoja na wewe. Hasa tulikuwa hatujui lipi bayna na lipi zuri, sababu toka kufika Kur'ani Afrika ilikuwa pazia nyeusi. Na Mwenyezi Mungu amekutuma kuja kuondoa hiyo pazia nyeusi. Basi Mungu asimamishe utume wako, mpaka siku ya Kiyama.”

(9) Bwana Nassor Shariff wa Pemba.

Ametuandikia akasema, “Ama kwa jinsi nilivyofurahi hata nimezieneza habari kwa mara moja kwa kuzigawanya karatasi hizo. Muda tu wengine katika tulio nao katika jengo moja wamenijia na maneno ambayo yanamwunga mkono Bwana H. Rashidi Ong'era wa Kamagambo ambayo hayakuachana kabisa na maneno niliyoyasema moyoni mwangu tokea nilipoipata habari hii mara ya kwanza. Ama hakika kwa hamu ya siku nyingi sana juu ya Msahafu huo ninafikiri labda sikufanya jambo bayna kwa kuuagiza kutoka hapa karibu nami ambapo nitaupata kwa upesi ili kushibisha njaa yangu, kwa hivyo mimi na baadhi ya wenzangu humu katika jengo la “Administration” tumetuma pesa zetu katika Duka la Unguja.”

(10) Bwana H. Rashidi Ong'era wa Kamagambo.

Amesema, "Aidha tafsiri hii itatufaa sana sisi tulio Waislamu kwani mionganini mwetu wako wanaojua kusoma Kurani (kama mimi) lakini hawajui tafsiri yake na sasa tutajionea sisi wenyewe tafsiri fasihi na maana yake."

(11) Bwana Khamis Mahmood wa Rujewa.

Akaandika, "Nimefurahi sana kuipata Tafsiri ya Kurani Tukufu uliyofasirii kwa Kiswahili, na imenipendeza sana Tafsiri yako zaidi inapiga vita juu ya Wakristo na hii ndio inavyofaa kwa wakati wetu huu tulionao, sababu tumezungukwa na uadui wao pembe zote za Afrika ya Mashariki."

(12) Bwana Adam Ndamanje wa Natal, South Afrika.

Ameandika: "Nimefurahi sana kwa kupata Misahafu tarehe 18.6.53. Nakushukuru sana sana. Sitasahau msaada wenu milionitolea kwa ukarimu mwingi kwa kuniletea Msahafu upesi. Natumai nitaweza kuagiza misahafu mingine katika mwezi ujao."

(13) Bwana Snow White wa Kigoma.

Ameandika: "Ninashukuru mmo na ninaipa mkono wa baraka juhudii na kazi kamilifu iliyofanywa kwa uhodari na mkuu wa Jumuia ya Islamu ya Afrika Mashariki Ahmadiyya Muslim Mission kwa kazi kubwa iliyofanya katika kupiga chapa kitabu cha mara ya kwanza katika Afrika nzima juu ya Tafsiri yote ya Kurani tukufu, yenye herufi zilizo nzuri bayana za Kizungu na zisizoisha kiu kusomwa.

Nakubali hayo pamoja na kuhakikisha kuwa tafsiri hiyo haina shaka ni njema tena safi ikienda hatua bega kwa bega katika lingano moja ya inavyotaka Kiarabu kwa Kiswahili na bila kuharibu maana wala Kiarabu chenyewe jinsi kinavyotakiwa.

Waidha maelezo mengi yaliyomo yanamfunulia mjuzi na ambaye si mwerevu wa Kiarabu (Kurani). Maelezo yaliyomo yanaweza kumfundisha mtu ye yote akawa mtaalamu kwa sababu Kiswahili chake kilichomo ni baraka hakina tofauti baina ya watu kwa watu.

(14) Sheikh H. J. Lipenga wa Nyasaland.

Ameandika, "Ahsante sana bwana Mas'hafu nimepata kwa furaha sana na mno nimeshituka kuona fasaha ya tafsir ya Kur'an kuliko niliyonunua zamani 1932, Dar es Salaam Bookshop ambayo ilitungwa na Bwana G. Dale wa Unguja. Ama tafsiri hii imekuwa kama "Atomic Bomb". Na hiyo nina furaha nayo zaidi maana kila neno limo na maelezo hasa vile katuonyesha aya ya Taureti na Injili. Hapana mfano tena wa kufananisha na tafsir hii. Mungu awape baraka watungaji. - Amin."

(15) Bwana A. A. Kaindu wa Kigoma.

Kwa kumwunga mkono Bwana H. Rashid Ong'oti anaandika:

Tafsiri hii iliyofanywa na Waislamu wa Ahmadiyya ina uzuri wa ajabu. Maelezo yake yamejaa maarifa na usitadi mkubwa. Tafsiri ya "matini" ya Kiarabu ni tamu sana na nyepesi, na inatupa neno kwa neno. Habari za mirathi, ambayo ni elimu ngumu katika Uislamu, katika tafsiri hii imepangwa kwa ustadi na kurahisishwa sana. Majina ya vitabu walivyorejea yanatubainishia kuwa tafsiri hii ni sahihi na yenye thamani sana. Wanaojua Kiarabu ingawa kidogo, hawatakosa kukiria ubora wa tafsiri hii ya ajabu na watajiongezea maarifa mengi ya lugha. Tunawashukuru mabwana wa Ahmadiyya kwa kazi ya tafsiri tuliyokuwa na haja nayo sana."

**(16) Bwana K. I. S. Milimba wa Veterinary Office,
Dar-es-Salaam.**

Ameandika: "Ingawa watu wengi wamekwisha andika ya sifa na ubora wa Kurani Tukufu kwa Kiswahili, nami pia juu nazidi kuyatilia mkazo maneno ya wasomaji hao wa Msahafu huu Naam, msahafu huu ni mzuri sana tafsiri yake na ilio wazi kabisa. Maelezo na mafundisho ya msahafu huu ni zaidi ya mwujiza.

Hivyo sina budi ya kutoa shukrani nyingi kwa E.A. Ahmadiyya Mission kwa juhudhi yao kubwa ya kutafsiri Kurani Tukufu kwa ajili ya watu wote wa Afrika Mashariki. Kazi hii ya kutafsiri Kurani Tukufu kwa Kiswahili iliwashinda masheikh wote na wanachuoni wakubwa wa Kiislam kwa miaka mingi. Kwa kushindwa kwao kutafsiri Kurani basi walisema haiwezi kutafsirika, eti wakiogopa kukufuru. Sasa

yanionyesha wazi wazi kwamba Waahmadiyya tu peke yao ndio wanaofuata njia safi ya Mtume s.a.w. na ninawaaombea baraka na rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya Chama cha Ahmadiyya - Amina.”

Kazi ya Mungu itakwenda mbele

Hayo juu ni maneno ya Waislamu wema waliopendezwa na tafsiri hii ya ajabu. Na kitu kizuri ndicho hufanyiwa husuda, hivyo kijicho cha Sh. Abdallah na Ali Muhsin wa Unguja kikawika, lakini maskini kimewaunguza wenyewe na kuwafedhehesha bure. Barua zilizotufikia ni nyingi za kuisifu tafsiri hii. Na hii ni kazi ya Mwenyezi Mungu itakayowainua Waislamu na kuwatia nguvu mbele ya maadui zao, nasi hatujali lawama ya mtu ye yote mwenye kijicho kama cha Sh. Abdallah. Kazi ya Mungu itakwenda mbele, nasi tumo katika kuandaa silaha na mipango ya namna nyingi nyingine ya kuulinda Uislamu na kuzibomoa dini za uwongo, ili Uislamu peke yake utawale katika dunia. Na nuru ya Mtume Muhammad s.a.w. ing’ae kila mahali. Hivyo, ni juu ya ndugu zetu Waislamu wenye akili safi kama hao walioandika barua hizo kuarifiana nasi mara kwa mara na kujuua njia bora bora za kuilinda dini ya Mtume Muhammad s.a.w.

**Na mwisho wa maneno yetu, Sifa zote njema zinamhusu
Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote.**